**KIRINYANGA**
**SCHOOL BASED FORM 4 EXAM - 2017**
**HATI YA KUHITIMU ELIMU YA SEKONDARI KISWAHILI**

**102/1**
**KISWAHILI**
**KARATASI 1**
**INSHA**
**JULAI/AGOSTI 2017**
**MUDA: SAA $1^3/_4$**

1. **LAZIMA**
   Mwandikie barua mhariri wa Gazeti la Baraka ukimweleza sababu za watoto wengi katika kauti yako kuacha shule na kujiingiza katika ajira za mapema.
2. Vipakatalishi vimeleta manufaa mengi nchini.
   Fafanua.
3. Andika insha itakayothibitisha ukweli wa methali:
   Mcheka kilema hafi bila kumpata.
4. Andika kisa kitakachoanzia kwa maneno yafuatayo:
   Kushoto kulikuwa na jitu la miraba minne ambalo lilitema cheche za matusi ungedhania ni karakana …

for free revision past papers visit: www.freekcsepastpapers.com

**SCHOOL BASED FORM 4 EXAM - 2017**
**HATI YA KUHITIMU ELIMU YA SEKONDARI KISWAHILI**

**102/2**
**KISWAHILI**
**KARATASI 2**
**JULAI / AGOSTI 2017**
**MUDA: SAA 2 ½**

1. **UFAHAMU (alama 15)**

**Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali.**

Ponografia ni tendo, maandishi, picha au michoro inaoonyesha au kueleza uchi wa mtu au vitendo vya ngono kwa ajili ya kuchochea ashiki ya kuifanya. Mambo haya machafu huwasilishwa ana kwa ana kupitia sinema, magazeti, vitabu, muziki, televisheni, tovuti na kanda za kunasia picha na sauti.

Ponografia imekuwepo tangu jadi, hasa katika nchi za magharibi. Lakini sasa limekuwa tatizo sugu. Hii ni kwa sababu imeenea kote ulimwenguni mithili ya moto mbugani wakati wa kiangazi. Kuenea kwake kumechangiwa na mambo kadha wa kadha. Mchango mkubwa zaidi ukiwa umetokana na kuimarika kwa vyombo vya teknolojia ya habari na mawasiliano. Hata hivyo, kazi hii hubuniwa au kutengenezwa na makundi mbalimbali ya watu. Miongoni mwa hawa ni watu wasiojali maadili. Pili, kuna wale wenye matatizo ya kisaikolojia na kijamii. Wao hutengemea na kueneza uchafu huu kwa lengo la kuvuruga maadili katika jamii au kuchukiza wanajamii waadilifu. Kundi lingine ni lile la wanaoichukulia ponografia kama nyenzo ya kutosheleza ashiki zao. Kwa mfano, baadhi ya wanamuziki hutumia **ponografia** kuvutia wateja na hivyo kuzidisha mauzo yao.

Kushamiri kwa wimbi na uonyeshaji wa ponografia kuna athari kubwa kwa jamii hasa watoto. Ingawa watu wengine hudai picha hizi haziwaathiri, upo ushahidi kuonyesha kuwa wale wanaotazama picha za ngono hupata matatizo. Lazima ieleweke kwamba kinachoonekana kwa jicho au kusikika kwa sikio huathiri fikira au hisia. Picha za matusi zinachangia kwa kiasi kikubwa kuharibu akili. Badala ya kuzingatia mambo muhimu kama vile masomo, watu huanza kutafakari mambo machafu.

Vijana wengi ni kama bendera, huyaiga wanayoyaona na kuyasikia. Hili ni tatizo linalowafanya kuacha mkondo wa maadili. Hivyo basi wengi hushawishiwa kuingilia shughuli za ngono mapema kabla hawajakomaa kimwili, kiakili na kihisia. Matokeo yake ni ukahaba, utendaji mbaya shuleni, mahudhurio mabaya darasani na mimba zisizotarajiwa. Vijana wengi huacha shule kabisa huku wengine wakiambukizwa magonjwa ya zinaa ambayo yanaweza kuwaletea mauti.

Yasemekana kuwa akili za binadamu hunasa zaidi mambo yanayowalishwa kwa picha na hivyo basi matusi haya yaweza kudumishwa katika kumbukumbu zao. Tabia mbaya kama vile ushoga, ubasha na usagaji huwa matokeo yake na hata matokeo ya vijana hugeuka wanapoanza kuiga mitindo mibaya ya mavazi yanayoanika uchi wao. Hali kadhalika, lugha, ishara na miondoko inayohusiana na ngono huibuka. Yote haya yanakinzana na desturi za mwafrika. Si ajabu visa vya ubakaji vinaongezeka kuchapo. Utazamaji wa picha chafu aghalabu huandamana na maovu mengine kama vile unywaji pombe na matumizi ya vileo ambavyo huchochea uchu wa ngono na kuibua tabia za kinyama.

Kuendelea kuzitazama picha hizi huzifanya nishai na hisia za watu kuwa butu, huondoa makali kiasi kwamba hata katika uzima mtu hupoteza mhemko na kugeuzwa kuwa mtegemezi wa ponografia. Tatizo hili linaenea kwa vishindo mjini na vijini. Ipo haja ya dharura kuikinga jamii kutokana na malezi haya yasiyo na kizuizi.

Kuuongeza ufahamu wa umma wote kuhusu uovu wa picha hizi, watu wazima kuwajibika kwa kuwalinda na kuwahimiza vijana kuhusu maovu haya na wale wenye midahilishi, video na sinema kutowaruhusu vijana kutazama uchafu huu kunaweza kuwa maana ya kuyakinga au hata kuyaepuka madhara ya ponografia. Ni sharti pia sheria izuie na kupiga marufuku utengenezaji na uenezaji wa upungufu huu. Bila shaka, sheria na hatua kali ziweze kuchukuliwa dhidi ya

waivunjao. Hali kudhalika, wazazi wasijipweteke tu bali wawaelekeze watoto wao ipasavyo na kila mtu alitekeleze jukumu lake.

**Maswali**

(a) Yape makala uliyosoma anwani mwafaka. (alama 1)
(b) Toa sababu za kusambaa kwa uchafu unaozungumziwa katika taarifa. (alama 2)
(c) "Bendera hufuata upepo." Thibitisha ukweli wa kauli hii kulingana na makala. (alama 1)
(d) Ponografia huchangia madhara mengi hasa miongoni mwa vijana. Taja **manne**. (alama 4)
(e) Ni hatua zipi zinazofaa kuchukuliwa dhidi ya aina ya uozo unaozungumziwa na mwandishi? (alama 4)
(f) Fafanua msamiati huu kimuktadha. (alama 3)
(i) Uchu
(ii) Wasijipweteke
(iii) Kuwa butu

2. **UFUPISHO (alama 15)**

**Soma makala yafuatayo kasha ujibu maswali.**

Sisi vijana wa Kenya inatupasa tuwajibike kufanya kazi kwa bidii, na kwa dhati ya mioyo yetu ili tuweze kupata ufanisi, uwezekano wa kuinua nchi yetu katika kiwango cha juu. Tukumbuke, "Ajizi, ni nyumba ya njaa." Kwa hivyo basi haifai kulaza damu ikiwa matatizo nchini mwetu yametuzonga. Lazima tufanye kazi kwa busara, adabu njema na jitihada kwa moyo mmoja. Sharti tutilie maanani zaidi elimu ya vijana na watu wazima, kilimo, uchumi na amani katika nchi yetu. Tunahitaji taifa lenye watu walioelimika, kwani bila elimu itakuwa vigumu sana kuweza kutekeleza mipango mbalimbali ya maendeleo. Tupende tusipende lazima tuzidishe mazao shambani, kwani kila kukicha idadi ya watu inaongezeka. Ni sharti tuweze kujitosheleza katika vyakula. Zaidi ya hayo pia lazima tujishughulishe na biashara ambapo kwa sasa ni wakenya wachache sana ambao wanatambua umuhimu wa biashara. Wengi ni wale wenye mawazo ya kwamba, lazima kila mmoja aajiriwe maishani. Yatupasa tujitahidi kuleta uchumi katika mikono ya wananchi wa Kenya badala ya kuwaachia wengine ambao hawahusiki.

Mafunzo tunayopata majumbani, shuleni na hata katika jamii, lazima yatuwezeshe kutambua mbinu za kupitia. Tunahitaji elimu tambuzi ambayo itamfanya mwanakenya kujua wajibu wake katika jamii. Tumesinywa na elimu pumbao; inayotupumbaza na kutufanya tusione mbele. Sisi vijana tukiwa viongozi wa siku zijazo, "Utengano ni uvundo!! Lugha ya taifa ndicho chombo cha pekee ambacho kinatuunganisha na kuweza kutuwasilishia mapendeleo, mawaidha na hisia zetu. Kukosa ndiko kibinadamu, wakati tunapokosea, lazima tukubali tumekosa na kufanya masahihisho mara moja kwani, "Usipoziba ufa, utajenga ukuta." Tusikasirike kwa sababu tumesahihishwa makosa yetu na wenzetu. Lazima tujitoe mhanga na kupigania nchi yetu tukiwa wazalendo halisi.

Sisi tukiwa vijana sharti tujihusishe na kuyangalia matatizo ya nchi, pia kutafuta njia za kutatua matatizo hayo. Siku zote tutekeleze nidhamu. Ni jambo la kusikitisha kwamba sisi vijana twashitumiwa mara kwa mara kwa kutokuwa na nidhamu shuleni na manyumbani mwetu. Utamaduni wa asili unakariri sana tuwe na nidhamu shuleni na majumbani mwetu. Ili watu waweze kuishi maisha bora na kuwa na maendeleo, amani na upendo, lazima tuwe na bidii, ushirikiano mwema na kuchagua viongozi wenye mioyo ya maendeleo. Tukiwa na viongozi ambao hawajishughulishi na maendeleo, basi tutabaki nyuma kama mkia siku zote. Bahati mbaya ni kwamba wananchi wengi siku hizi huchagua viongozi wao kwa kufuata ukoo ama kama kwa utajiri wake. Kwao hivyo basi ni vyema kuwachagua viongozi kutokana na ufanisi wanaoweza kuleta bali si kwa kutegemea utajiri ama ukoo.

**Maswali.**

(a) Katika aya ya kwanza mwandishi anawahimiza vijana kufanya nini ili kuleta maendeleo? (maneno 50) (alama 7)
(b) Kwa mujibu wa taifa ni mambo gani yaliyochangia kuzorota kwa maendeleo nchini Kenya?(maneno 60) (alama 8)

3. **MATUMIZI YA LUGHA. (alama 40)**

(a) Taja na utofautishe vipasuo vya ufizi. (alama 2)
(b) Fafanua maana ya istilahi **neno** kama kipashio cha lugha. (alama 1)
(c) **Eleza matumizi ya 'ku' katika sentensi:** (alama 2)
Sikumweleza alivyoeleza namna ya kuwatanza mbwa wake.
(d) **Tambua na ueleze aina za vivumishi katika sentensi ifuatayo.** (alama 2)
Mwanafunzi mkongwe amepewa tuzo kwa kuwa hodari masomoni.
(e) **Tofautisha vitale hivi kwa kuvitungia sentensi.** (alama 2)
Jua
Chua
(f) **Andika katika ukubwa wingi.** (alama 2)
Mzee huyu ana wake wengi.
(g) **Andika kwa kinyume ukizingatia maneno yaliyopigiwa mstari.** (alama 2)
Hamusi alikunja nguo alizokuwa ameanika.
(h) **Andika tena sentensi ifuatayo ukifuata maagizo uliyopewa.** (alama 2)
Kama wanafunzi hawamthamini mwalimu hawawezi kufaulu katika masomo.
(Anza: Ni vigumu …)
(i) **Andika sentensi ifuatayo katika kauli ya kutendewa.** (alama 2)
Mavu hawa wamemsumbua Nyatogo kwa muda mrefu.
(j) Tunga sentensi ukitumia nomino dhahania inayotokana na neno jengo**.** (alama 2)
(k) **Onyesha maana ya 'Po' katika sentensi hii:** (alama 2)

for free revision past papers visit: www.freekcsepastpapers.com

Nilipofika nilimwona pale alipokuwa amesimama.

(l) **Yapange maneno haya katika ngeli zake.** (alama 1)
Neno
Mate

(m) **Akifisha sentensi ifuatayo.** (alama 2)
baba alimwambia asha utaenda shuleni utake usitake.

(n) **Changanua sentensi ifuatayo ukitumia muundo wa jewali:** (alama 4)
Mkulima ambaye ni mzembe amepata hasara kubwa.

(o) Herufi kubwa hutumiwa mwanzoni mwa sentensi: Onyesha matumizi mengine mawili ya herufi kubwa huku ukitolea mifano. (alama 2)

(p) **Tumia – ndi pamoja na viashiria vya ngeli kujaza mapengo.** (alama 1)
Wewe ______________________ ninayekutafuta.
Nyinyi ______________________ mnaoongoza

(q) **Bainisha vishazi katika sentensi ifuatayo.** (alama 2)
Mkulima aliyepanda wakati ufaao amepata mavuno mazuri.

(r) **Tofautisha maana:** (alama 2)
(i) Ningekuwa na uwezo ningesafiri kwenda nga'mbo.
(ii) Ningalikuwa na uwezo ningalisafiri kwenda nga'mbo.

(s) **Ainisha viambishi katika neno:** (alama 2)
Kujidhiki

(t) Bainisha shamirisho katika sentensi ifuatayo: (alama 3)
Asha alimbebea mwalimu mzigo kwa gari.

4. **Isimu Jamii. (alama 10)**
(a) Eleza maana ya sajili. (alama 2)
(b) Fafanua umuhimu wa sajili, katika jamii. (alama 8)

for free revision past papers visit: www.freekcsepastpapers.com

**KIRINYANGA**
**SCHOOL BASED FORM 4 EXAM - 2017**
**HATI YA KUHITIMU ELIMU YA SEKONDARI KISWAHILI**

**102/3**
**KISWAHILI**
**KARATASI 3**
**FASIHI**
**JULAI / AGOSTI 2017**
**MUDA: SAA 2 ½**

**SEHEMU A**
**MSTAHIKI MEYA (TIMOTHY M. AREGE)**
**SWALI LA LAZIMA.**

1. 'Hawa wanaotaka uwasikilize ni mzizi wa vizazi vya kesho!' …
   (a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
   (b) Eleza tamathali ya usemi iliyotumika katika dondoo hili. (alama 2)
   (c) Mstahiki Meya anatumia hila kujiimarisha uongozini. Dhibitisha. (alama 14)

**SEHEMU B**
**KIDAGAA KIMEMWOZEA (K. WALIBORA)**
**Jibu swali la 2 au 3.**

2. "… akadhukuru jinsi alivyopigwa na kibuhuti… Akakumbuka jinsi yule banati alivyoendelea kusimulia mambo yaliyokuwa yamejiri tangu ..."
   (a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
   (b) Eleza tamathali ya usemi iliyotumika katika muktadha huu. (alama 2)
   (c) Changanua changamoto zinazowakabili wanafunzi vyuoni na watoto walio na umri wa kuwa shuleni. (alam 14)

3. Umasikini ni donda sugu linaloathiri wahusika viwayani.
   Jadili changamoto zinazotokana na umaskini. (alama 20)

**SEHEMU C**
**DAMU NYEUSI NA HADITHI NYINGINE (KEN WALIBORA NA SAID A. MOHAMED)**
**Jibu swali la 4 au 5.**

4. Mwana wa Darubini (Kristina Mwende Mbai)
   "Ulijuaje alikuwa anaangalia kwetu?"
   (a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
   (b) Hadithi hii inaonyesha matatizo ya kijamii. Fafanua. (alama 8)
   (c) Mwanamke amesawiriwa kama kiumbe duni. Dhibitisha kauli hii kwa mujibu wa hadithi hii. (alama 8)

5. Ukidokeza mifano mwafaka, fafanua mambo yanayowatumbukiza vijana katika matatizo kwa kurejelea diwani ya Damu Nyeusi. (alama 20)

**SEHEMU D - USHAIRI.**
**Jibu swali la 6 au 7.**

6. **Soma ushairi ufuatao kasha ujibu maswali.**

Nakutubu maandiko, yafike hadi mliko,
Musomeni kwa mwamko, ujumbe uwe zinduko,
Shereheni pa maviko, ama kokote mwendako,
Kuna watu vitokoko, hawendi ela kwa mboko.

Huku kwetu tuliko, hatuishi unguliko,
Tuna watu wa vituko, watutiao sumbuko,
Wanao utundu foko, na ufakiri wa mbeko,
Kuna watu vitokoko, hawendi ela kwa mboko.

Yaletayo sikitiko, kwao ni mitimbwiriko,
Hata kuvuta tumbako, wakukalia kitako,
Wape nasaha zako, watasema 'nenda zako,
Kuna watu vitokoko, hawendi ela kwa mboko.

Ungawambia waliko, kuna moto na muwako,
Wataangu kicheko, 'kisema 'shauri yako',
Hadi yajiri mauko, nadama na fadhaiko,
Kuna watu vitokoko, hawendi ela kwa mboko.

Wanena michavuko, maneno yaso mashiko,

for free revision past papers visit: www.freekcsepastpapers.com

Wakizua gawanyiko, kwayo mawio matamko,
Hawajali sokomoko, ziletazo hangaiko,
Kuna watu vitokoko, hawendi ela kwa mboko.

Kumanga huku na huko, kama majibwa koko,
Na kuiba kwenye soko, ndiko wakugitariko,
Wachapwechapwe viboko, wapate misawajiko,
Kuna watu vitokoko, hawendi ela kwa mboko.

Msingoje ongezeko, huna ndo' wangu mfiko,
Sijanena miropoko, nimenadi badiliko,
Tuwe waso tukutiko, tusipende machafuko,
Kuna watu vitokoko, hawendi ela kwa mboko.

**Maswali.**

(a) Shairi hili ni la aina gani? (alama 2)
(b) Eleza toni la ushairi huu? (alama 2)
(c) Taja sifa **tatu** za kiarudhi katika shairi hili. (alama 3)
(d) Shairi hili ni la bahari gani? Taja **mbili**. (alama 2)
(e) Andika ubeti wa pili kwa lugha ya nathari. (alama 4)
(f) Huku ukitoa mifano **mitatu** eleza uhuru wa ushairi katika shairi hili. (alama 3)
(g) Tambua nafsi neni katika ushairi huu. (alama 2)
(h) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumika katika shairi. (alama 2)
(i) Mawi
(ii)Misawajiko

for free revision past papers visit: www.freekcsepastpapers.com

7. **Soma ushairi ufuatao kasha ujibu maswali.**

Nina tungo iso fumbo, wala sio tutumbi,
Sijapamba kama wimbo, sina raha na siimbi,
Nayaamba hayo mambo, kukuhaza zenye umbi,
Hatutaki usombombi, koma siasa za vumbo.

Toka miyaka ya kitambo, twakuona tu mlumbi,
Tena una majigambo, kwamba wewe ndiwe jimbi,
Hali miji na viambo, barabara ni za vumbi,
Hatutaki usombombi, koma siasa za vumbo.

Siku zote wenda ng'ambo, watumia ngwenje tumbi,
Hili 'sielewe kombo, hela zako hatuombi,
Tuchimbie hata lambo, tupe maji si vitimbi,
Hatutaki usombombi koma siasa za vumbo.

Kwetu sisi kuna mwambo, ya chakula tuna ngambi.
Nawe hapo una jambo, kama samaki mnyimbi,
Sipojifunga masombo, likungojalo siambi,
Hatutaki usombombi, koma siasa za vumbo.

Kubuniwa kwa majimbo, ni tulizo kwa kitambo,
Utazuka mwenye tumbo, ahadi nazo kivumbi,
Ukikwisha tega chambo, cha kufwata ni unyambi,
Hatutaki usombombi, koma siasa za vumbo.

Hino mbiu ya mgambo, na kisogo sikurambi,
Tendo liwe ndo' ulimbo, sio pombe za uhambi,
Situpe hata kilimbo, tumeshazira ugimbi,
Hatutaki usombombi, koma siasa za vumbo.

Nimekwisha jaza gombo, kwa uneni uso dhambi,
Fikiria haya mambo, kwani si usakubimbi,
Jua kura ndiyo fimbo, achezaye hula mumbi,
Hatutaki usombombi, koma siasa za vumbo.

*(Malenga wa Ghuba. Fred Obondo)*

(a) Taja na ueleze bahari mbili za shairi hili. (alama 2)

(b) Eleza umbo la shairi hili. (alama 4)

(c) (i) Kwa kutolea mifano eleza aina mbili za uhuru wa kishairi katika shairi hili. (alama 3)

(ii) Onyesha jinsi kibali ulichotaja hapo juu kulivyotumika kukidhi mahitaji ya kiarudhi. (alama 3)

(d) Eleza toni ya ushairi. (alama 2)

(e) Kwa kutolea mfano eleza tamathali ya usemi iliyotumika. (alama 2)

(f) Tambua nafsi neni katika ushairi huu. (alama 2)

(g) Eleza maana ya maneno haya kama yalivyotumika katika shairi: (alama 2)

(i) Usombombi

(ii)Lambo

**SEHEMU E**

**FASIHI SIMULIZI**

**Jibu swali la 8.**

8. (a) Eleza maana ya ngomezi. (alama 2)

(b) Eleza udhaifu wa ngomezi. (alama 4)

(c) Linganisha na ulinganue ngoma na ngomezi. (alama 8)

for free revision past papers visit: www.freekcsepastpapers.com

**MTIHANI WA PAMOJA WA SHULE ZA NAKA**

**102/1**
**KISWAHILI**
**Karatasi ya kwanza**
**Insha**
**MACHI 2017**
**MUDA:SAA 1 ¾**

1. Umeteuliwa kuwa miongoni mwa watakaohutubia wananci kuhusu hali ya usalama nchini Kenya.Andika hotuba utakayowasilisha siku hiyo kuhusu visababishi vya ukosefu wa usalama na upendekeze hatua zinazofaa kuchukuliwa ili kukabiliana na hali hii.
2. Katiba mpya nchini Kenya haijabadilisha maisha ya wananchi. Jadili
3. Ukiona cha mwenzako kikinyolewa na chako tia maji.
4. Andika insha itakayomalizikia kwa maneno haya:
   ……………………………..nilitamani ardhi ipasuke na nitumbukie humo nisionekane tena.

**MTIHANI WA PAMOJA WA SHULE ZA NAKA**
***Hati ya kuhitimu kisomo cha sekondari Kenya(K.C.S.E)***

**102/2**
**KISWAHILI**
**Karatasi ya pili**
**Lugha**
**MACHI 2017**
**MUDA:SAA 2 ½**

**UFAHAMU (Alama 15)**
***Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali.***

Mwanamke wa kisasa anazaliwa na kukulia katika mazingira yaliyobadilika mno. Matazamio yake maishani ni tofauti na yale ya wanawake walioishi mapote mawili yaliyopita; wanawake makamu ya nyanyake na mamake mkuu.

Yeye hutarajia kuzaliwa, kukua, kuolewa, kuwa mke wa bwana, kumzalia watoto na daima dawamu kuwa **‘mwendani wa jikoni’** akawapikia watoto na bwanake chakula; na akitoka jikoni aelekee shambani kulima, kichakani kuchanja kuni, mtoni kufua nguo na kuteka maji ya kutumia nyumbani. Mwanamke wa kisasa huandamana na mwanamume. Akanyagapo **mume naye papo huutia wayo wake.**

Mwanamke wa kisasa huenda shule na kujifunza yote yafunzwayo huko. Hushindana na wanawake kwa wanaume na kuibuka mshindi si mara haba. Huibuka mshindi katika masomo ya lugha, Historia, Jiografia, Hesabu, Sayansi na mengineyo, sawa na mwanamume.

Mwanamke wa kisasa hutaka kufanya kazi za kibega, akazifanya. Akataka kuwa mwalimu, akawa. Akataka kuwa daktari, akafanikiwa. Almuradi, siku hizi mwanamke hufanya kazi yoyote ile afanyayo mwanamume. Kuna wanawake marubani wa ndege, masonara, waashi, wahandisi, madereva wa magari, mawakili mahakimu, mawaziri wakuu na hata marais wa nchi Hakuna kazi isiyofanywa na mwanamke siku hizi.

Mwanamke wa kisasa **hateswi akafyata ulimi.** Anapohiniwa yeye hupigania haki yake kwa dhati na hamasa. Katu hakubali ‘mahali pake’ katika jamii alipotengewa na wanaume wenye **mawazo ya kihafidhina** yaliyopitwa na wakati.

Siku hizi mwanamke huolewa tu wakati amepata kazi ya kumwezesha kujikimu maishani au pale anapokuwa na hakika kwamba biashara yake iwapo ni mfanyi biashara, imepiga hatua ya kutomrudisha **ukatani.**

Mwanamke wa kisasa haamuliwi katika jambo, lolote, bali hufanya maamuzi yake mwenyewe. Kwa upande mwingine, mwanamume wa ‘kisasa’, ambaye bado amefungwa pingu na taasubi za kiume, hapendezwi na mwanamke huyu. Huuma kidole akatamani ya kale, lakini wapi! Analazimika kumkubali mwanamke huyu kama mshiriki sawa maishani, na kuishi naye, apende asipende. Shingo upande analazimika kukubali kwamba mabadiliko haya sio mithili ya kiwingu kipitacho, bali ni ya **aushi.**

**Maswali**

a) i) Msemo ‘mwendani wa jikoni’ unadhihirisha hali gani ya mwanamke katika jamii? (alama1)
   ii) Thibitisha hali uliyotaja hapo juu kwa kutoa hoja nne. (alama 2)
b) Mwandishi ana maana gani anaposema ‘akanyagapo mume naye papo huutia wayo wake’ (alama 1)
c) Tofautisha mwanamke wa kiasili na wa kisasa ukizingatia maswala ya ndoa na elimu. (alama 4)
d) Eleza hoja sita zinazoonyesha kuwa wanaume wana ‘mawazo ya kihafidhina’ dhidi ya mwanamke. (alama3)
e) Fafanua athari zinazotokana na mabadiliko ya mwanamke wa kisasa katika jamii kulingana na mwandishi. (alama2)
f) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumika katika taarifa. (alama 2)

for free revision past papers visit www.freekcsepastpapers.com

i. Ukatani
ii. Aushi

**UFUPISHO (alama 15)**

***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali yanayofuata.***

Katika karne hii na ya kesho, urafiki ni ngome kuu duniani amabayo huhifadhi maslahi ya kila rafiki. Rafiki mwema humpenda mwenzake si kwa sababu ni tajiri ama ana cheo kikuu nchini. Rafiki mwadilifu huridhika na hali aliyonayo rafikiye; akiwa ni tajiri au ni masikini, ana cheo, hana. Rafiki mwema huwa mwadilifu wakati wowote. Wakati wa neema hushirikiana na rafikiye katika furaha na wakati wa shida hushirikiana naye katika huzuni na taabu zote zinazomkabili.

Sahibu mwema hutoa alichonacho kumkomboa rafiki yake, huwa radhi kabisa kufilisika kwa ajili yake. Mahali pa finyo hujasiri kuingia ili kumkomboa rafikiye, hushughulika zaidi kuliko wana ndugu wa toka nitoke. Kwa vyovyote hula naye tamu na chungu pamoja, mkono kwa mkono katika maisha yao yote hadi mmoja wao akaitoka dunia. Urafiki wa namna hii ndio uletao Baraka ya Mungu, kuwashukia viumbe hao kama umande wa asubuhi.

Urafiki ni lazima sana katika maisha ya wanadamu. Urafiki ni mfano wa mishipa ipitishayo damu mwilini ili kurutubisha kila sehemu ya mwili. Ingawa ni bora kuwa na marafiki wengi lakini kila marafiki wanapozidi, ni hatari ya kuangukia kwenye marafiki wadanganyifu hasidi. Pasi na shaka, ni heri maadui kuliko marafiki wadanganyifu. Hivyo basi, tukiwa na rafiki walio kinyume cha wema na upole wa kulinda haki za wanadamu na wasiomcha Mungu ni lazima tuwaepuke. Ingawa ni hivyo, vile vile sheria inatukataza tusisikilize na kujali ubaya wa mtu yeyote pasipo kuhakikisha. Huenda ikawa ni uvumi tu usiokuwa na msingi wowote. Ikiwa rafiki ni mbaya, haikosi atajulikana kwani mtungi mbovu haukawi kuvunjika. Lazima tuwapende watu wote ili kutimiza haki za kibinadamu na kuchukia matendo maovu. Rafiki waovu si vema kuwaacha katika maangamizi ya ubaya wao bali ni lazima tuwaambie waziwazi ili wapate kuokoka. Ukimsamehe rafiki, unaponya donda lake moyoni. Hivyo ni bora kuliko kumtazama na hali anazidi kukosa.

for free revision past papers visit: www.freekcsepastpapers.com

**Maswali**

a) Fupisha aya ya kwanza na ya pili kwa kutumia maneno yasiyozidi 60. (alama 7, 1 ya utiririko)

b) Fupisha mambo muhimu kama yalivyoelezwa na mwandishi katika aya ya mwisho. Tumia maneno kati ya 60 – 65.(alama 8, 1 ya utiririko)

**MATUMIZI YA LUGHA (alama 40)**

a) i) Eleza dhana ya kiambishi (alama 1)
ii) Ainisha viambishi na utoe mifano (alama 2)

b) Taja vitamko vyenye sifa zifuatazo: (alama 2)
i) Vokali ya nyuma, juu
ii) Nazali ghuna cha mdomo

c) Huku ukitoa mfano, eleza maana ya sentensi sahili. (alama 2)

d) Tunga sentensi ya masharti yasiyowezekana. (alama 2)

e) i) Taja sifa mbili za nomino za pekee. (alama 2)
ii) Dhihirisha nomino ya pekee katika sentensi. (alama 1)

f) Ainisha kiunganishi katika sentensi hii. (alama 2)
Japo Kiptoo ni dereva hodari, hana leseni ya kuendesha gari

g) Tunga sentensi moja kuonyesha maana mbili tofauti za neon 'bana' (alama 2)

h) Fuata maagizo kwenye mabano. (alama 2)
Tafadhali hakikisha Jane ameelimika vizuri (andika katika kauli ya kutendesha)

i) Eleza maana mbili za sentensi hii. (alama 2)

j) 'Kwa' imetumika vipi katika sentensi zifuatazo? (alama 2)
i) Tumealikwa kwa Chebet.
ii) Alipata alama ishirini kwa mia.

k) Tunga sentensi kubainisha muundo ufuatao. (alama 2)
KN(W+V)+KT(T+E)

l) Andika kwa ukubwa wingi. (alama 2)
Mwizi aliiba nguo na kiti

m) i) Tofautisha shamirisho kipozi na shamirisho kitondo. (alama 2)
ii) Onyesha shamirisho kipozi na kitondo katika sentensi moja. (alama 2)

n) Tunga sentensi ukitumia kirejeshi 'O' kuonyesha uzoefu. (alama 2)

o) Eleza matumizi ya kiambishi /ji/ (alama 1)
Alijikata mguu.

p) Andika sentensi ifuatayo katika hali isiyodhihirika. (alama 1)
Kibofu hupaa angani.

q) Andika katika usemi wa taarifa. (alama 2)
"Kwa nini unampiga ndugu yako? Nyanya alimuuliza.

r) Pambanua kwa kielezo cha matawi. (alama 4)
Mkufunzi hodari amepita mtihani rahisi.

**ISIMU JAMII (alama 10)**

a) Eleza mambo matano yaliyochangia maendeleo ya Kiswahili kama lugha ya mawasiliano nchini Kenya kabla ya Uhuru.

b) Kwa nini watu huchanganya msimbo wanapozungumza. Toa hoja tano. (alama 5)

**MTIHANI WA PAMOJA WA NAKA**
***Hati ya kuhitimu kisomo cha sekondari Kenya(K.C.S.E)***
**102/3**
**KISWAHILI**
**Karatasi ya tatu**
**FASIHI**
**MACHI 2017**
**MUDA:SAA 2 ½**

**SEHEMU YA A: USHAIRI**

Linatushangaza, twashangaa dhidi ya kushangaa!
Kwa mangamizi ya kila leo.
Tunayotekelezewa na kiumbe razini zaidi,
Binadamu!

Hatujui sababu,
Mzinga na mazega yetu kuteketezwa,
Yetu asili kuvinwa kwa mababu na waritimba,
Binadamu wasiojua madhila yetu
Kudamka kutafuta nekta, na kukesha kulinda mzinga!
Lakini kinachotushangaza, twauliza: mwatuchomeani?

Twafedheka jamani!
Masaibu ya tajiri
Tajiri mwema kuwatajirisha wasio na faidha
Badala ya wakatilia moto daraja la fanaka,
Wasijue kesho, kesho kutwa, mtondo…. Watavuna wapi?
Baada ya kutuangamiza, sie vitega chumi vyao.

Tuma haki, kama nyinyi,
Ya kuwaona watoto na wetu vijukuu
Wakikua na kufaidi, jasho letu wazazio
Ingawa hili halijawa faradhi,
Ila kwa mapenzi yenu ya dhati

Kumbuka binadamu,
Hata sisi tuna hisia, tusichomwe,
Japo wajinga tunayo manufaa
Sie hatuwahi, mbona nyie?
Na safari yetu sote, japo njia tofauti.
Twende pole pole!

for free revision past papers visit: www.freekcsepastpapers.com

**Maswali**

a) Eleza dhamira ya mtunzi wa shairi hili. (ala. 2)
b) Hili ni shairi la aina gani? Toa sababu. (ala.4)
c) Taja na utoe mifano miwili ya tamathali za semi zilizotumiwa katika shairi hili. (ala. 4)
d) Huku ukitoa mifano mwafaka eleza idhini za utunzi zinazojitokeza katika tungo. (ala. 4)
e) Eleza maana ya msamiati ufuatao:
i) Razini
ii) Masaibu
f) Andika ubeti wa pili kwa lugha nathari. (ala. 4)

**SEHEMU YA B: TAMTHILIA: MSTAHIKI MEYA:**
***Timothy Arege***

2. "Hawa ndio watu muhimu katika ulimwengu wa sasa".
 a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (ala. 4)
 b) Fafanua mchango wa mrejelewa katika kusambaratisha baraza la cheneo. (ala. 4)
 c) Cheneo imekandamizwa kutokana na wakazi wake kutotumia akili. Fafanua hii kwa kurejelea tamthilia nazima. (ala. 12)
3. Unafiki na tamaa ndio chanzo cha dhiki ya wanacheneo. Thibitisha kwa kurejelea matukio katika tamthilia nzima. (ala. 20)

**SEHEMU YA C: HADITH FUPI: DAMU NYEUSI NA HADITHI NYINGINE:**
***Ken Walibora na Said A. Mohamed***

4. Jadili kwa kina maudhui ya uozo wa kijamii na kutowajibika huku ukirejelea hadithi zifuatazo

i. Damu nyeusi
ii. Maeko
iii. Samaki wa nchi za joto
iv. Kanda la usufi (ala. 20)

5. "Asanteni sana kwa kuja. Sisi kama wazazi na walimu hukabiliana na mengi".
   a) Weka dondoo hili katika muktadha wake. (ala. 4)
   b) Fafanua matukio yaliyosababisha mkutano huu. (ala. 4)
   c) Eleza changamoto zozote sita zinazoikumba jinsia ya kike katika hadithi husika. (ala. 12)

**SEHEMU YA D:RIWAYA: KIDAGAA KIMEMWOZEA NA Ken Walibora**

6. "Moyo ulimpapa na kijasho chembamba kumtekenya juu ya mwanzi wa pua. Akahisi uchungu wa mwiba kujidunga".
   a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (ala. 4)
   b) Fafanua kwa tafsiri namna mrejelewa alivyojidunga mwiba. (ala. 6)
   c) Huku ukitumia wahusika wowote wawili eleza namna walivyojidunga mwiba. (ala. 6)
   d) Tambua na ueleze mbinu za lugha zilizotumika katika dondoo hili. (ala.4)
7. Taja na ueleze ujumbe muhimu unaojitokeza katika kila barua riwayani. (ala. 20)

**SEHEMU YA E: FASIHI SIMULIZI**

8. a) Eleza tofauti kati ya maghani na mighani. (ala.2)
   b) Eleza jinsi utakavyowasilisha utanzu wowote wa fasihi simulizi. (ala. 8)
   c) Je, ni vipi jamii ya kisasa inaendeleza fasihi simulizi. (ala. 6)
   d) Eleza mambo manne ambayo huchangia kubadilika kwa fasihi simulizi. (ala. 4)

for free revision past papers visit: www.freekcsepastpapers.com

**MTIHANI WA PAMOJA WA MOSTA 2017**
HatiyaKuhitimuKisomo cha Sekondari

**102/1**
**KISWAHILI**
**Karatasiya 1**
**INSHA**
**2017**
**Muda: Saa 1¾**

1. **LAZIMA**
   Wewenimhaririwagazeti la **ChanukaUendelee**. Andikataharirikuhusukueneakwatatizo la ubadhirifuwamaliyaummakatikamagatuzimbalimbalinakupendekezanjiambalimbalizakukabiliananalo.
2. Mradiwaserikaliwavipakatalishikwashulezamsinginchiniutakuwanamanufaasihaba. Jadili.
3. Tungakisakitakachodhihirishamaanayamethaliifuatayo:
   Fimboyambalihaiuinyoka.
4. Tungakisakitakachomalizikakwamanenoyafuatayo:
   ........nilishushapumzikwahisiazashukrani, safari hiihaikuwarahisinawengihawakutarajiakuwaningefaululichayawingu la simanzinamisukosukolililoniandamatarikinzima.

**MTIHANI WA PAMOJA WA MOSTA 2017**

**KISWAHILI**
**KARATASI YA 2**
**LUGHA**
**2017**
**MUDA: SAA 2½**

**UFAHAMU (alama 15)**
Idara ya polisi nchini imelaumiwa kwa muda mrefu kutokana na visa vya mauaji ya kiholela, **utepetevu** na ufisadi miongoni mwao.Ni kutokana na kilio cha mwananchi pamoja na mashirika yasiyo ya kiserikali ambapo serikali **imejitolea sabili** kubadili hali katika idara hiyo huku tume mbali mbali zilizobuniwa zikitoa mapendekezo muhimu ya kurekebisha idara hiyo. Matokeo ya hivi punde kutoka kwa shirika la Transparency International liliorodhesha idara ya polisi kama idara fisadi zaidi nchini,maoni ambayo yalisisitiziwa na shirika la kutetea haki za kibinadamu .Ufisadi bado umekita mizizi katika idara ya polisi tangu mabadiliko yaanze upande wa trafiki na hata ndani ya polisi,.

Serikali imejitolea kupambana na ufisadi unaonekana kuwa kidonda ndugu katika idara ya polisi. Wananchi wanasema kuwa polisi ni mafisadi na kusahau kuwa ufisadi unashirikisha watu wawili na wote wanapaswa kufunguliwa mashtaka,lazima raia na polisi wazingatie hili.Na ili kuleta mabadiliko muhimu katika idara ya polisi,mapendekezo yote pamoja na ya tume zingine za hapo awali lazima yatekelezwa na kwa mujibu wa katiba mpya.Lazima mabadiliko yaanze kuanzia juu kwani maafisa wadogo hulazimiswa kuchukua hongo ili wapelekee wakubwa wao,ni lazima shughuli ya kuwachagua maafisa waliobora ifanyike kisheria ili mabadiliko yaanze kutoka kwa wakuu wa maafisa wa polisi.

Polisi kidogo wameweza kubadili ile lugha yao ya matusi na ukali kwa rai.Raia nao hawajabadilika,bado wana uwoga dhidi ya polisi na itachukua muda kwani wanadhania kuwa kikosi ni kile kile cha kitambo.Kwa upande wa polisi, hakuna mageuzi yamefanyika.Unaposafiri kuja mjini polisi wangali wana chukua hongo kutoka kwa wenye matatu na kuwaruhusu kubeba kupita kiasi, pia usalama umedorora sana kwani kumekuwa na visa vingi vya mauaji hapa mjini.ukiangalia maafisa wa polisi hakuna mageuzi makubwa yameshuhudiwa haswa kwa upande wa maafisa wa trafiki bado ni wale wale na ufisadi ungali upo.

Mabadiliko ambayo tunataka ni ile polisi wasikae mahali kwa muda hadi wanajuana na mafisadi na majambazi.Maafisa wa polisi wanafaa kuhudumu katika kituo kimoja kwa muda usiozidi miaka mitatu.Kwa kufuata njia hiyo mabadiliko yatapatikana.Juhudi nyingi zikielekezwa katika kubadili kikosi cha polisi wananchi wanapaswa kuhamasishwa ili nao wawezakubadilikahaswa kuhusuiana na mtazamo wao kwa maafisa wa polisi **.Na huku tukijaribu kubadili maafisa wa polisi wananchi pia wanapaswa kuelimishwa ili waweze kubadili mtazamo wao kuhusu maafisa hao.**Ni bayana kuwa ili kuweza kuleta mabadiliko ya kutamanika katika kikosi cha polisi na haswa katika kupambana na ufisadi uliokita mizizi wananchi sawia na maafisa wa polisi wanajukumu la pamoja kuleta mabadiliko hayo yatakayopelekea kuwepo kwa mlahaka mzuri kati ya maafisa wa polisi na raia.Hatimaye kuwepo kwa huduma bora itakayochangia pakubwa kuboresha uchumi wa taifa na kuafikiwa kwa ruwaza ya mwaka 2030.

for free revision past papers visit: www.freekcsepastpapers.com

**Maswali**

a) Kipe kifungu hiki kichwa mwafaka. (alama 1)
b) Thibitisha kwamba ufisadi ni kidonda ndugu ukirejelea makala haya. (alama2)
c) Ni vipi ufisadi katika idara ya polisi unaweza kuzikwa katika kaburi la sahau? (alama2)
(d) 'Wananchi ndio wanapaswa kulaumiwa kwa ufisadi."Thibitisha. (alama 3)
(e) "Serikali imepiga hatua katika kuleta mabadiliko katika idara ya polisi".Onyesha kinaya cha usemi huu. (alama 2)
(f) Taja manufaa yoyote mawili yanayotokana na mabadiliko katika idara ya polisi (alama2)
(g) Eleza maana ya:
(i) Mlahaka.
(ii) Utepetevu.
(iii) Kujitolea sabil. (alama 3)

**UFUPISHO (Alama 15)**

**Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali yanayofuata**

Kwa miaka na dahari, nchi nyingi za Asia, Amerika Kusini na Afrika, zimekuwa na mamilioni ya watoto wanaoteseka. Matatizo huwakumba kwenye hali nyingi. Si kielemu, si kiafya, si kiutamaduni na kimakuzi tu, bali hata kiuchumi. Nguvu zao na uwezo wao hufujwa kwa njia zinazokirihisha nyoyo. Wale wanaopenda maendeleo na kutilia nguvu haki za kibinadamu huudhiwa kupindukia.

Wazazi wengi wa sehemu hizo wamekuwa wakiamini mambo kipuuzi. Wamekuwa wakidhani kuwa wingi ni hoja, lakini wazazi hawa huwapata watoto wengi wasioweza kuwatunza. Isitoshe, huwachukulia watoto kama sehemu ya mali yao badala ya kuwachukulia kuwa ni binadamu wenzao. Akili haziwapigi na kutambua kuwa, hata nao 'vinyang'arika', wakitunzwa vizuri na kupewa nafasi mwafaka za kuwainua kimaendeleo, wataweza kuwa watu wa kutajika katika jamii. Wazazi kama hao wanadhania ya leo ni leo tu, msema kesho ni mwongo. Dhana hizo finyu na potovu zimewapelekea kuthamini uzaaji wa watoto wengi ili watoto hawa wawe punda wa dobi. Wazazi hawa wanajihisi matajiri wa kupindukia wanaopata vijana wengi wa kuwasaidia katika kazi zao bure bilashi.

Baadhi ya watoto hunyimwa nafasi ya kwenda shule. Wale wanaonjeshwa masomo kidogo, huachishwa kisomo hicho mapema. Sababu za kuhinishwa huko kwa kisomo zinafahamika vizuri na wahusika hao. Mara nyingi, huachishwa shule ili wawe mayaya wa watoto wenzao au wakafunge mifugo, kulima shambani, kusaidia biasharani na katika sekta za juakali. Watoto hawana nguvu za kukataa kwani ni kinyume cha utamaduni kuwapinga wazazi. Isitoshe, watoto hawa wanawategemea wazazi hao kwa kila kitu. Utiifu huu, ingawa una uzuri wake unazorotesha maendeleo kupindukia.

Unyonge wa aina hii umefanya mashirika ya viwanda, ya mashamba kama ya chai, kahawa, ya pamba na ya juakali kuwatumia watoto vibaya bila ya kujali maslahi ya watoto hao. Baadhi ya watu wameanzisha mashirika ya uasherati na utumwa. Watoto wanateswa na kuingizwa kwenye majanga yanayotokana na ukimwi na mengine ya uzinifu. Kutokana na dhuluma hizi, watoto hukandamizwa na kupewa posho duni ya kuwapa uhai tu. Matajiri wamezidi kufutuka kiuchumi kutokana na jasho la watoto hao. Watoto hawapewi kinga zozote za kemikali wala kuonyeshwa jinsi ya kuzitumia kemikali hizo. Wakuu wao hutumia saikolojia duni za watoto kuwawezesha kujikuza kiuchumi. Huwapa viperemende hafifu na viungo ovyo ili watoto waimbe na kucheza ngoma za watu hao. Watoto, kwa kutojua, huwasifu wakuu wao badala ya kuwalaani kwa kuwanyonya hadi mifupani na kupewa vijipesa tu. Kwa kuwa ni watoto hawatambui kuwa wanahiniwa.

Matajiri nao husahau kuwa watoto hao wakisoma vizuri hadi mwisho, wanaweza kutoa huduma bora nchini. Inadhihirika kuwa lengo potovu la watu hao ni kukwepa kulipa mishahara mikubwa kwa watu wazima. Lakini nasema si sawa kuwanyonya watoto. Matajiri hawa wangehisi vipi kama watoto wao nao wangefanyiwa hivyo? Ama ni yule ya mkuki kwa nguruwe, kwa mwanadamu uchungu? Serikali zina mikono mirefu. Inafaa ziwachukulia hatua kali wazazi na maafisa wanaotumia watoto kama matambara mabovu. Watoto nao wanafaa kuzinduka na kutaka kusoma kinyuki. Inafaa wajue kuwa vipesa vya ujakazi ni sumu.

Mashirika ya aina hiyo, inafaa yakipatikana na hatia, yapewe adhabu kali. Yalazimishwe kuwasomesha na kuwakimu watoto hao vilivyo, bila kuwanyanyasa ndipo wasome, kadri ya uwezo wao.

for free revision past papers visit: www.freekcsepastpapers.com

**Maswali**

(a) Bila kupoteza maana iliyokusudiwa fupisha aya mbili za mwanzo kwa maneno (45-50) (al. 6, 1 utiririko)
(b) Kwa kuzingatia taarifa hii eleza namna maonevu dhidi ya watoto yameendelezwa.. tumia maneno (50-55) al. 9, 1 utiririko)

**MATUMIZI YA LUGHA (alama 40)**

a) Kutokana na kigezo cha jinsi hewa inavyozuliwa,taja aina mbili za konsonanti na utolee mifano kila moja (alama 2)
b) Bainisha muundo wa silabi katika neno (alama 2)
Gongwa
c) Eleza maana ya mofimu funge na kutoa mfano mwafaka (alama 1)
d) (i) Eleza maana ya kiarifu. (alama 1)
(ii) Onyesha kiarifu katika sentensi ifuatayo (alama 1)
Mtoto aliyezungumza na nyanyake ameingia darasa lililochafuliwa na watundu.

e) Bainisha shamirisho katika tungo lifuatalo. (alama 2)
Mwanafunzi alipewa dawati na mwalimu jana jioni

f) Bainisha matumizi ya kiambishi **'ku'** katika sentensi hii (alama 2)
Naomi atakupikia chai halafu aende kule uwanjani

g) Tambua aina ya kivumishi na kihusishi katika sentensi ifuatayo (alama 2)
Kijana mgeni amekaribishwa na mgeni

h) Tunga sentensi ukitumia kitenzi '**-nywa'** katika kauli ya kutendeka. (alama 1)

i) Tunga sentensi iliyo na kitenzi kishirikishi kilicho na kiambishi nafsi na wakati (alama1 )

j) i) Eleza dhana ya kishazi. (alama 1)
ii) Onyesha aina za vishazi kwa kutumia sentensi moja. (alama 1)

k) Changanua sentensi ifuatayo kwa kutumia vishale (alama 4)
Alimwona mamba majini alipopiga mbizi.

l) Yakinisha (alama 2)
Mgonjwa huyo hakupona wala kurejea nyumbani

(m) Sahihisha sentensi ifuatayo (alama 2)
Mgeni ambaye aliyekuja atarudi jana.

(n) Akifisha sentensi ifuatayo (alama 2)
Juma Maria ulimwona Farida Maria la hakuwepo jana

(o) Andika sentensi ifuatayo katika wingi. (alama 1)
Ua unaozunguka nyumba una ua lililopandwa.

(p) Weka nomino hizi katika ngeli zake (alama 1)
i) Mbalungi.
ii) Mturuki.

r) Andika katika hali ya udogo (alama 2)
Alishikwa na jipu ambalo lilivimbisha kidole chake cha mguu mithili ya pera.

(s) Andika katika usemi wa taarifa (alama 2)
"Lo! Kumbe wazuri hawajazaliwa," Omari alisema baada ya kumwona kisura huyo.

(t) Andika misemo inayoafiki hali zifuatazo (alama2)
i) Kubahatika.
ii) Ubahaili.

(u) Eleza maana tatu za sentensi ifuatayo (alama 3)
Mama alimwimbia mwanawe.

(v) Tunga sentensi moja kutofautisha maana mbili ya neno **ziwa** (alama 2)

**ISIMU JAMII (ALAMA 10)**

(a) Eleza maana ya istilahi hizi; (alama 2)
(i) Usanifishaji.
(ii) Lahaja.
(b) Taja sifa zozote nne za lugha yoyote ile. (alama 4)
(c) Eleza mambo yanayochangia makosa ya kisarufi na ya kimatamshi katika lugha ya Kiswahili (alama4)

for free revision past papers visit: www.freekcsepastpapers.com

**MTIHANI WA PAMOJA WA MOSTA 2017**
**Hati ya Kuhitimu Kisomo cha Sekondari – Kenya**
**102/3**
**KISWAHILI**
**Karatasi ya 3**
**FASIHI**
**2017**
**Muda: Saa 2½**

**A. HADITHI FUPI: DAMU NYEUSI NA HADITHI NYINGINE**

**1. Swali la lazima**

***Kanda la Usufi***

"Hakujua maisha yake yangechukua mkondo upi. Mzo wa majuto ulimwandama. Ulimwengu wake ulivurugika, akawa kama tiara inayopeperushwa na upepo ikaenda arijojo"

(a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
(b) Taja na kueleza tamathali ya usemi kwenye dondoo hili. (alama 4)
(c) Kwa kutolea mifano, onyesha jinsi anwani Kanda la Usufi inavyoafiki hadithi husika. (alama 12)

**B. SEHEMU YA RIWAYA**

**Kidagaa Kimemwozea:** *Ken Walibora*

***Jibu swali kla 2 au la 3***

2. "Nyamaza boza wewe. Wadhani sisi kazi tunaanza leo? Tumekutana na wauaji wangapi?
a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
b) Dondoo hili linadokeza maudhui gani? Kwa kutoa mifano saba kwenye riwaya, bainisha jinsi maudhui hayo yanavyojitokeza. (alama 16)
3. Riwaya ya *Kidagaa Kimemwozea* imesheheni hali zinazotukia bil kutarajiwa. Fafanua. (alama 20)

for free revision past papers visit: www.freekcsepastpapers.com

**C. SEHEMU YA TAMTHILIA**

**MSTAHIKI MEYA**: *Timothy Arege*

4. Hayawezi kulinganishwa na tendo hili ndogo. Walifanya vizuri kuja.
(a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
(b) Fafanua nafasi ya wanaorejelewa kuwa " walifanya vizuri kuja" katika tamthilia hii. (alama 4)
(c) Migogoro katika tamthilia hii hazikusuluhishwa vyema. Jadili. (alama 12)
5. Jadili matumizi ya mbinu ya ishara katika tamthilia hii. (alama 20)

**D. SEHEMU YA USHAIRI**

6.

Nitafukuzwa mbinguni
Kwa ushairi wangu mbaya
Lakini hata motoni nitaimba:
Wanasema
Wanasiasa ni kama jizi
Lililosukuma mtoto pembeni
Na kunyonya ziwa la mama
Wakati amelala usingizi usiku.

Wanasema
Mwanasiasa afapo
Tumejikomboa na domo
Moja pana lizibwalo na mchanga
Na kilima cha simenti ngumu
Lisikike tena hadharani.

Wanasema pia
Kusema haki
Kwa kawaida
Wanasiasa hatuwapendi.
Kupiga kura ni hasira za mkizi
Ni basi tu. Ni Ah!
Ah!
Wanamalizia
Nchi mmefiilisi waacheni walimu
Wakajenga taifa jipya.

Kama hamwezi kuona mbali
Bure kuweka mkono usoni,

Bure hakuna kichwa
Kama hamwezi kufikiri.

Ng'ombe amekamuliwa na wazungu
Waarabu, wahindi na wao
Sasa anatoa damu
Vilivyobaki ni chai ya rangi
Na madomo mapana zaidi
Yaliyo bado hai.
Kuimba nimeimba

**Maswali**

(a) Mshairi ana dhamira gani? (alama 2)
(b) Shairi hili ni la kukatisha tama, tetea rai hii. (alama 2)
(c) Onyesha matumizi mawili ya mishata. (alama 2)
(d) Eleza mbinu zozote nne za lugha zilizotumika katika shairi hili. (alama 4)
(e) Andika ubeti wa mwisho katika lugha tutumbi. (alama 4)
(f) Fafanua umbo la shairi hili. (alama 3)
(g) Eleza maana ya mafungu ya maneno ya maneno yafuatayo: (alama 3)
(i) kupiga kura ni hasira ya mkizi
(ii) kuweka mkono usoni
(iii) ng'ombe amekamuliwa.

for free revision past papers visit: www.freekcsepastpapers.com

**7. SABUNI YA ROHO**

Ewe tunu ya mtima, kwa nini wanikimbia?
Ndiwe suluhu za zama, waja wakukimbilia,
Waja wanakutazama, madeni wakalipia,
Ndiwa sabuni ya roho, ndiwe mvunja mlima.

Ndiwe mafuta ya roho, walisema wa zamani,
Utanunua majoho, majumba na nyumbani,
Umezitakasa roho, umekuwa mhisani,
Ndiwe sabuni ya roho, ndiwe mvinja mlima.

Matajiri wanakujua, wema wako wameonja,
Nguo zao umefua, wakupata kwa ujanja,
Sura zao 'mefufua, wanazuru kila njanja,
Ndiwe sabuni ya roho, ndiwe mvunja mlima.

Ndiwe mvunja mlima, onana na maskini,
Watazame mayatima, kwao kumekua duni,
Webebe waliokuwa, wainue walio chini,
Ndiwe sabuni ya roho, ndiwe mvunja mlima.

Ndiwe mvunja mlima, wapi kapata uwezo,
Umezua uhasama, waja kupata mizozo,
Ndiwe chanzo cha zahama, umewatia vikwazo,
Ndiwe sabuni ya roho, ndiwe mvunja mlima.

Umevunja usuhuba, familia zazozana,
Waliokuwa mahabuba, kila mara wagombana,
Roho zao umekaba, majumbani wachinjana,
Ndiwe sabuni ya roho, ndiwe mvunja mlima.

Nakutafuta kwa hamu, sabuni unirehemu,
Sinilipue ja bomu, sije kawa marehemu,
Niondoe jahanamu, ya ufukara wa simu,
Ndiwe sabuni ya roho, ndiwe mvunja mlima.

Naondoka wangu moyo, nikuitapo itika,
Fulusi wacha uchoyo, tatua yalonifika,
Nichekeshe kibogoyo, nami nipate kuwika,
Ndiwe sabuni ya roho, ndiwe mvunja mlima.

**Maswali**

(a) Taja nafsi nenewa. Thibitisha. (alama 2)
(b) Eleza toni ya nafsi neni. (alama 1)
(c) Eleza arudhi zozote nne zilizozingatiwa katika utunzi wa shairi hili. (alama 4)
(d) Mshairi anawasilisha ujumbe gani katika mleo wa ubeti wa sita? (alama 1)
(e) Ukitoa mfano eleza mbinu zozote tatu za lugha alizotumia mshairi. (alam 3)
(f) Andika ubeti wa nne katika lugha nathari. (alam 4)
(g) Jadili jinsi mshairi anatumia ruhusa ya mshairi. (alama 2)
(h) Kwa kurejelea mpangilio wa vina eleza bahari ambamo shairi hili linaweza kuainishwa. (alama 1)
(i) Fafanua maana ya : (alama 2)
i) ndiwe sabuni ya roho, ndiwe mvunja mlima
ii) jehanamu

**C. FASIHI SIMULIZI**

8. (a) Eleza maana ya mivigha. (alama 2)
(b) Fafanua sifa zozote nne za mivigha. (alama 8)
(c) Taja hasara zozote nne zinazohusishwa na mivigha. (alama 4)
(d) Eleza njia zozote tatu unazoweza kutumia kukusanya data kuhusu mivigha. (alama 6)

for free revision past papers visit: www.freekcsepastpapers.com

**TRIAL 102/1**
**KISWAHILI**
**Karatasi ya 1**
**INSHA**
**JULY/AUGUST**

1. Wewe ni kiranja anaye husika na masomo shuleni mwako. Mwandikie kiranja anayehusika na masomo katika shule jirani ukiwaalika wanafunzi wake katika mjadala shuleni mwako. Ambatanisha ratiba itakayofuata siku hiyo.
2. Jadili chanzo, madhara na jinsi ya kukabili tatizo la vita vya wenyewe kwa wenyewe barani Afrika.
3. Andika Mtungo unaothibitisha ukweli wa methali: Jitihada haiondoi kudura.
4. Andika insha itakayomalizikia kwa: . . . Na katika uchaguzi wa marudio uliofanywa baada ya kisa hicho, Hidaya akapata ushindi mkubwa na kuwa mbunge wa eneo bunge la Kubali.

**TRIAL 102/2**
**KISWAHILI**
**Karatasi ya Pili**
**JULY/AUGUST**

**UFAHAMU (ALAMA 15)**

**Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali.**

for free revision past papers visit: www.freekcsepastpapers.com

Mabadiliko ya hali ya anga ni suala nyeti katika ulimwengu mzima. Suala hili sasa limetoa msukumo wa kulazimu kupanua nafasi ya hifadhi ya mazingira. Kwa sasa, ni bayana kuwa waja wakiendelea na mtindo wa maisha ya kibepari ya kutumia mali asili kwa ulafi wa kukidhi tu haja zao bila kujali maslahi ya wengi, basi dunia itahiliki hatimaye. Lazima tufahamu fika kuwa tunapaswa kutumia mazingira yetu kwa manufaa ya leo na kwa vizazi vya kesho.

Tayari athari za mabadiliko ya hewa yameanza kuathiri kila sehemu ya nchi yetu ya Kenya. Mvua hainyeshi jinsi ilivyokuwa awali, kilimo kinafeli kwa sababu ya kuzidi kwa kiangazi, maelfu ya mifugo wamekufa kwa kukosa malisho na maji. Jamii za wafugaji sasa zinakosa lishe bora kwa sababu ya dhiki na ufukara. Bei za bidhaa za kimsingi zimepanda mijini na mashambani kutokana na ukame ulioko sehemu nyingi. Isitoshe chemchemi za maji zinapotea huku mito ikikauka, wanyama pori wanakufa kwa njaa na kiu, makabiliano kati ya binadamu na wanyama pori yameongezeka, nao ufukara unaongezeka kila siku miongoni mwa umma. Hali hii sasa inachangia kuzorota kwa usalama hasa katika sehemu kame. Kuna visa vingi vya kuibiana mifugo na kubishiana chemchemi za maji na maliasili. Asilimia kubwa ya mito imekauka, chemchemi za maji zinapotea na vinamasi vya milima ya taifa havipo tena kutokana na uharibifu wa misitu na utumiaji mbaya wa maliasili.

Ndiyo maana hatujasita kukariri kuwa mabadiliko ya hali ya anga ni mtikisiko wa kitaifa kwani ni hali ya hatari na kuwa kila mtu ana jukumu kujitahidi kiasi cha uwezo wake kuchangia uhifadhi wa mazingira. Mvua ikinyesha tupande miti, tuhifadhi chemchemi za maji na sehemu za unyevunyevu; tulinde mito na maziwa yetu; tulime huku tukihifadhi udongo wetu, tufuge, si kwa haja ya kuwa na mifugo wengi bali kwa kukidhi mahitaji na pia kulinda mazingira; tujitarishe kuhifadhi maji ya mvua kwa ajili ya matumizi ya nyumbani na kilimo; tuzidishe juhudi za kupanda mimea mbalimbali ya chakula huku pia tukifufua ile ya kienyeji.

Harakati za kupambana kuhifadhi msitu wa Mau, ambao ni chanzo kikubwa zaidi cha maji na mito nchini na hata Afrika Mashariki zinajullikana. Kutokana na vitendo vya ulafi wa viongozi wetu msitu huu umevamiwa na kuharibiwa na hata unaitishia maisha ya mito, maziwa, mbuga za kuhifadhi wanyama pori na mamilioni ya watu wanaotegemea msitu huu kwa njia moja au nyingie. Tunatambua kwamba juhudi nyingi zinafanywa na serikali kutokana na shinikizo zawakereketwa na wadau wa mazingira. Lakini lazima serikali itumie uwezo wake wote kuilinda misitu ya Mau, Mlima Kenya, Mlima Elgon na misitu mingine kwa jumla. Tusipuuze misitu na mazingira kwa sababu ya siasa duni.

Isiwe ni shughuli ya serikali kulinda misitu pekee bali wananchi pia wajitume kwani mazingira yanahusu uhai wa kila mmoja wetu. Kuntu umoja ni nguvu utengano ni udhaifu. Ndiyo maana tunachukua fursa hii kuwapongeza wakazi wa malava katika kaunti ya Kakamega ambao hivi majuzi walijitokeza mzomzo kupinga uharibifu wa msitu huo na kuungana pamoja kupanda miche takriban hamsini elfu. Watu waharibifu wasiruhusiwe kuangamiza misitu, mazingira, mandhari na maisha kule Malava.

Serikali pia inapaswa kutenga hela kulinda misitu inayofunika milima. Milima ya taifa ni mandhari yanayopendeza nchini na lazima kila juhudi za kulinda uhai katika milima hii zifanywe. Ni jukumu la maafisa wa ardhi, wa mazingira na wa misitu kutoa ushauri kwa serikali kwamba kuna hatari ya misitu kumalizwa na watu wabinafsi. Sheria ihimizwe na wananchi wahamasishwe kuhusu umuhimu wa kulinda na kuimarisha mazingira.

**Maswali**

1. Toa kichwa mwafaka kwa taarifa. (alama 1)
2. Mabadiliko ya hali ya anga husababishwa na nini? (alama 2)
3. Toa athari tatu zinazosababishwa na kubadilika kwa hali ya anga. (alama 3)
4. Kwa nini mwandishi hatasita kukariri kuhusu hali ya hatari? (alama 3 )
5. Ni sababu gani iliyopelekea kuharibiwa kwa msitu wa Mau? (alama 1)
6. Kwa nini mwandishi anasema **umoja ni nguvu utengano ni udhaifu**. (alama 1)
7. Eleza maana ya vifungu vifuatavyo kama vilivyotumika katika taarifa. (alama 4)

**i).** vizazi vya kesho
**ii).** mitikisiko wa taifa
**iii).** hatujasita kukariri
**iv).** kienyeji

**UFUPISHO**
**MUKHTASARI (ALAMA 15)**
***Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali yatakayofuata.***

Binadamu hupenda kujivika vilemba vingi mno. Tunapenda kuheshimiwa na kutukuzwa na kila mtu. Tunapenda kuombwa ushauri na wote ambao wanahitaji ushauri. Tunapenda kutambuliwa popote tuendapo.

Watu wengi hukataa kufanya jambo la halali kwa kuhofia kuitwa wajinga. Mfano mzuri ni pale ambapo mtu amekosea kidogo katika kutenda jambo; utaona kuwa mtu huyo anaona ugumu wa kuomba radhi au samahani ati kwa sababu ataonekana mjinga.

Je, ni mara ngapi mkurugenzi ameita mkutano na katika barua yake akatisha kuwaadhibu watakaochelewa na mwishowe ni yeye mwenye anayechelewa? Tena huwa haombi msamaha. Ataulaumu usingizi uliomchukua, au gari lililomleta.

Aghalabu tunapowakuza watoto wetu, tunawafunza maadili mema. Tunawahimiza wale wadogo kwamba n vizuri kuomba radhi kwa wakubwa wako unapowakosea. Lakini kumbuka kwamba kukosea ni kwa binadamu wote. Mtu anaweza kukukosea kwa makusudi au kwa bahati mbaya. Kwa hivyo tunapaswa kufahamu kwambia, tunapofanya makosa ni lazima tuombe msamaha, iwe ni kwa wakubwa au kwa wadogo, ili kuondoa kero.

Waja wengi huogopa kusimama mbele za watu na kuwasilisha au kutenda jambo Fulani. Kisa na maana, mtu hataki kutenda jambo fulani halafu akosee. Hajiamini na anaogopa kuwa huenda watu wakaona kasoro yake. Lakini, kukosa njia ndiko kujua.

Huenda ikawa watu wanajadili maswala ibuka kama vile ufisadi, kuavya mimba, matumizi ya dawa za kulevya, ukimwi, uzuiaji wa kizazi na kadhalika… labda huyaungi mkono maoni ya watu wengine kwa sababu ya imani na maadili yako. Hata hivyo, hutaki kusimama ukatoa msimamo wako mbele za watu ingawa dhamiri yako imekwazika. Baadaye utasikika ukiwalaumu watu wengine ilhali ulikataa kusimama na kutetea msimamo wako.

Wengi wetu hujichukua kuwa watu muhimu sana. Wanaona kuwa sherehe au mkutano wowote hauwezi kufaulu ikiwa wao hawako. Wanapokuwa kwenye hiyo mikutano wao hutaka watambuliwe. Hupenda maji na yao yatajwe. Haya huwaridhisha, lakini swali ni je, kuwepo kwao ni muhimu kiasi hicho? Kumbuka kwamba ungeendelea vizuri bila kuwepo kwao. Kwa hivyo, tusiwe watu wa kutaka kutambuliwa kila tunapoenda mahali. Pia, tusilalamike ikiwas hatukuhusishwa katika jambo fulani.

Unaposhuhudia jambo fulani, kama wizi au ajali usiwe na woga wa kutoa usadizi kwa kutoa ushuhuda. Wengine hata huogopa kutoa usaidizi huo, hata kwa manusura wa ajali za barabarani, eti kwa sababu wanahofia kuitwa mahakamani kutoa ushuhuda. Kuna shida gani kuenda kusema yale uliyoyashuhudia bila kuongeza au kutoa chochote?

for free revision past papers visit: www.freekcsepastpapers.com

**<u>MASWALI</u>**

a) Bila kupoteza maana, fupisha aya ya kwanza hadi ya nne ( maneno 60 ) *(alama 8)*
b) Fupisha aya nne za mwisho (maneno 50 ) *(alama 7 )*

**SARUFI**
**MATUMIZI YA LUGHA** **(ALAMA 40)**

a) **Taja sauti za viyeyusho.** (alama 2)
b) **Yakinisha sentensi hizi.** (alama 2)
i) Mwanafunzi hachezi mpira leo.
ii) Chakula hakipikiki vizuri.

c) **Tumia vihusishi mwafaka kukamilisha sentensi zifuatazo.** (alama 2)
i) Tulisafiri kuelekea kwetu________ basi.
ii) Alikuwa _____________ wale walionusurika.

d) **Jibu maswali yafuatayo ukizingatia maagizo yaliyo kwenye mabano.** (alama 2)
i) Malipo ambayo anapewa ni yale ambayo yanaridhisha. ( Tumia 'o' rejeshi tamati)
ii) Mtu huyu amenitumia zawadi nzuri ambayo sitaisahau. (Bila kutumia 'amba' anza kwa Sitasahau).

e) **Changanua sentensi ifuatayo kwa njia ya matawi.** (alama 4)
**Dereva Yule stadi anaendesha gari uwanjani.**

f) Pamabanua viambishi katika neno 'aliyewapenda' na uonyeshe ni vya aina gani. (alama 3)

g) **Akifisha kifungu hiki.** (alama 2)
Nilipomwendea aliniangalia kisha akaniambia siamini kuwa ni wewe uliyeandika insha hii

h) **Eleza tofauti iliyopo katika jozi hii ya sentensi.** (alama 2)
(i) Alimpatia soda kwa chupa.
(ii) Alimpatia chupa ya soda.

i) **Kwa kutungia sentensi tumia nomino <u>mume</u> kama kielezi.** (alama 1)

j) **Bainisha aina ya vitenzi katika sentensi hizi.** (alama 2)
i) Wewe u mwanafunzi wa Marekani.
ii) Jana nilinunua mkate na maziwa.

k) **Tumia kiambishi 'po' kutunga sentensi itakayoonyesha** (alama 2)
i) Mahali
ii) Wakati.

l) **Andika kwa udogo.** (alama 2)
Mbwa Yule alimuuma mtoto.

m) **Eleza matumizi ya 'ni' katika sentensi zifuatazo** (alama 3)
i) Wanasoka wanaucheza mpira uwanjani.
ii) Kiptoo ni mkulima hodari.
iii) Halima alinitembelea kwetu juzi.

n) **Bainisha shamirisho katika sentensi ifuatayo.** (alama 3)
Mwalimu atawasimulia wanafunzi hadithi kwa kipaza sauti.

o) **Toa vitenzi vinavyotokana na maneno haya.** (alama 2)
i) Hasidi…………………………………………………………………………………….
ii) Kifaa ……………………………………………………………………………………..

p) **Andika kivumishi kitokanacho na vitenzi vifuatavyo.** (alama 2)
i) Nyooka ………………………………………………………………………………….
ii) Ng'aa …………………………………………………………………………………

q) **Andika wingi wa sentensi ifuatayo.** (alama 1)
Aliambiwa anunue ndizi na nazi.

r) **Nyambua vitenzi katika kauli zilizo kwenye mabano.** (alama 3)
i) Andaa (kutendama)……………………………………………………………………….
ii) Paa (kutendeka)…………………………………………………………………...
iii) Fumba (kutendata)……………………………………...……………………….

for free revision past papers visit: www.freekcsepastpapers.com

**ISIMU JAMII**

1. Fafanua maana ya dhana zifuatazo (alama 4)
i) Lugha rasmi
ii ) Lugha ya taifa

2. Krrrri! krrrrri! Hallo! Hallo! Hapo ni Sunshine? Name! Mimi …….. sawa! Kwa hivyo? Ala! Mbona ikawa …………… No, no ! Sina time.
i) Tambua sajili hii ya mawasiliano (alama 1)
ii) Taja mbinu za lugha katika muktadha huu (alama 2)

3. Wananchi wenzangu, nitahakikisha kila mtoto anapata elimu, matibabu na chakula. Mimi nina wajibu wa hawa wengine ambao wameanza utetezi walikuwa wapi mimi nilipoleta umeme? Wao in watu bure kabisa! -------------
Kwa kurejelea kifungu hiki, taja sifa zozote zinazotawala sajili hii. (alama 3 )

**TRIAL 102/3**
**KISWAHILI**
**FASIHI**
**KARATASI YA 3**
**JULY/AUGUST**

**SEHEMU A - USHAIRI**
**LAZIMA**

**1. SHAIRI (ALAMA 20)**

Ana siku mwizi, hata awe nani
Wake ubazazi, watu kuwahini
Atajuta wazi, hili ni yakini.

Hili ni yakini, aone taabu
Aseme kwa nini, mimi sikutubu
Awe mashakani, kwa yalomsibu.

Kwa yalomsibu, yatamtatiza
Apate dharubu, waja kumwumiza
Dola imwadhibu, ndani ya gereza.

Ndani ya gereza, awe atadumu
Waja kumwapiza, na kumshutumu
Mola kumtuza, moto jahanamu.

Moto jahanamu, utamuadhibu
Ni adhabu ngumu, ilo na dharubu
Hapati naumu, wala cha sharabu.

Wala cha sharabu, maji kujinywia
Hakuna sahibu, wa kumtetea
Ila kukusibu, dhiki ya Jalia.

Dhiki ya Jalia, kuingia motoni
Hapa nafikia, pangu kituoni
Na mwizi sikia, mwepuke shetani.

for free revision past papers visit: www.freekcsepastpapers.com

**Maswali**
a) Lipe shairi hili anwani mwafaka. (alama 2)
b) Taja na ufafanue bahari tatu zinazodhihirika katika shairi hili. (alama 3)
c) Eleza muundo wa shairi hili. (alama 6)
d) Fafanua namna mshairi alivyozingatia uhuru wa ushairi. (alama 3)
e) Jadili ujumbe wa mshairi huyu. (alama 4)
f) **Eleza maana ya maneno haya.** (alama 2)
   (i) Ubazazi
   (ii) dharubu

**SEHEMU YA B: RIWAYA**
**T. Arege: *Mstahiki Meya***
Jibu swali la 2 au la 3

2. “Wafanyakazi katika bohari ya mafuta wamegoma.”
   (a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
   (b) Toa sababu **nne** kwa nini wafanyakazi wanagoma kulingana na muktadha huu. (alama 4)
   (c) Wafanyakazi walifanya kazi kwa masaibu mengi kule Cheneo. Fafanua. (alama 12)
3. Jadili mbinu zinazotumiwa na uongozi wa cheneo kukandamiza raia wake na kuendelea kutawala. (alama 20)

**SEHEMU YA C**
**RIWAYA: Kidagaa kimemwozea**
Jibu swali la 4 au la 5

4. Jadili jinsi mwandishi alivyofanikisha matumizi ya mbinu zifuatazo. (alama 20)
   i) Barua

   ii) Kinaya

   iii) Taswira

5. Uhuru wa Kiafrika ni wa bendera ipepeavyo mlingotini tu! Jadili kauli hili kwa kurejelea riwaya ya Kidagaa Kumemwozea. (alama 20)

**SEHEMU YA D**
**HADITHI FUPI: Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine**
Jibu swali la 6 au la 7

6. Kwa kurejelea hadithi zozote tano eleza mafunzo ya waandishi kuhusu ndoa. (alama 20)
7. "Badala ya kijihisi salama niliingiwa na wazo la kuwa debe tupu."
   a) Weka dondoo hili katika muktadha wake (alama 4)
   b) Ni tamathali ya usemi gani iliyotumika kwenye dondoo na kwa maana gani? (alama 2)
   c) Bainisha sifa za mhusika anayerejelewa kwenye dondoo. (alama 4)
   d) Onyesha uozo wa kijamii kama unavyodhihirishwa na mhusika katika hadithi (alama 10)

**SEHEMU YA E: FASIHI SIMULIZI**
8. a). Fanani huwa na nafasi mbili katika usimulizi wa hadithi. Taja na uelezee kila hizo nafasi. (alama 4)
   b). Toa maelezo na utaje mfano mmoja wa aina hizi za ngano za kimafumbo (alama 4)
      I. Istiara
      II. Mbazi
   c). Methali na vitendawili hufanana kwa kiwango Fulani. Toa mifano sita inayo-dhihirisha kauli hii. (alama 12)

for free revision past papers visit: www.freekcsepastpapers.com

**CEKENA**
**KISWAHILI**
**102/1**
**INSHA**
**JULAI/AUGOSTI 2017**
**TATHMINI YA MWISHO WA MHULA WA PILI**
**KINDATO CHA NNE – 2017**

1. Insha ya lazima:
   Njaa imetangazwa kuwa janga la kitaifa nchini. Andika mahojiano kati yako na waziri wa kilimo kuhusu namna bora ya kukabiliana na janga hili ili kuhakikisha kuwa taifa lina chakula cha kutosha. (Al 20)
2. Watu wanapojihushisha na ufisadi husukumwa na sababu mbalimbali. Thibitisha. (Al 20)
3. Andika kisa kinachodhihirisha maana ya methali hii:
   Gae huwa chombo wakatiwe.
4. Tunga kisa kitakachoanza kwa maneno haya
   "Nilikuwa nimeanza kupata usingizi nilipogutushwa na mlio mkubwa kama risasi. Nilijivuta na kuketi kitandani. Mara…………………….

**CEKENA**
**102/2**
**KISWAHILI LUGHA**
**KARATASI YA PILI**
**JULAI/AUGUST 2017**
**MUDA : SAA 2 ½**
**TATHMINI YA MWISHO WA MUHULA WA PILI 2017 KIDATO CHA NNE**

for free revision past papers visit: www.freekcsepastpapers.com

**UFAHAMU : (Alama 15)**
**Soma kifungu kifuatacho kasha ujibu maswali.**

Tokea muundo mpya wa serikali ya ugatuzi uanze kutekelezwa miaka miwili iliyopita, kumeendelea kushuhudiwa matatizo mengi hali iliyopelekea kushuhudiwa kwa msururu wa migomo na maandamano ya raia. Fujo za karibuni kabisa ni zile zinazoshuhudiwa katika miji mikubwa za wachuuzi na wafanyi biashara wakipinga hatua za serikali za kaunti kuwatoza ushuru takribani kwa kila huduma na bidhaa ikiwemo wanyama, kuku na ndege. La kuhuzunisha zaidi katika baadhi ya majimbo imeripotiwa kuwa raia wamelazimishwa kulipa ushuru kwa kutaka tu kuona maiti za jamaa zao kwenye vyumba vya kuhifadhia maiti!

Wanasiasa wameonekana kuwa na wakati mgumu kutetea mfumo huu mpya wa ugatuzi huku baadhi wakisema kwamba matatizo yanayoshuhudiwa kwa sasa yametokana na ugeni wa mfumo huo. Wengine wameinyoshea kidole serikali ya kitaifa kwamba ndiyo inayosambaratisha muundo huu. Wengine wanahoji kuwa bado ni mapema na kwamba kunahitajika muda mrefu ili kufaulu.

Ni wazi kwamba kumekosekana nidhamu biora ya kusimamia maisha ya raia nchini Kenya. Matatizo yanayokumba raia kwa sasa ni dalili kuwa mfumo wa serikali ya ugatuzi umeongezea chumvi kwenye kidonda badala ya kutibu. Swali ni je, hadi lini nidhamu ya kusimamaia raia itakuwa ni suala la majaribio na makosa?

Hatua ya kuwarundikizia raia ushuru mkubwa ni kitendo cha unyonyaji na cha dhuluma kinachofaa kupingwa. La kufahamishwa hapa ni kwamba ushuru ndio njia kubwa ya kuzalisha mapato ya serikali zinazojifunga na mfumo wa kimagharibi wa kiuchumi wa kibepari ikiwemo Kenya. Asilimia 90 ya mapato ya serikali za kibepari huegemea ushuru. Kwa hivyo hatua ya serikali za kaunti katika kuwanyonya raia kwa kuwalipisha ushuru si ajabu bali ni thibitisho kuwa jamii ya Kenya inaongozwa na nidhamu ya kiuchumi ya ubepari-mfumo wa unyonyaji na ukandamizaji. Ukweli unabakia kuwa ndani ya serikali za kibepari raia ndio hubebeshwa mzigo wa ushuru unaoishia matumboni mwa viongozi!

Miito ya mabadiliko ya katiba nay a miundo mipya ya kiutawala si lolote ila ni moja tu ya hatua za mfumo wa kibepari kujipa muda wa kuishi na kuziba aibu zake za kushindwa kusimamia maisha ya watu. Kufeli huku kwa mfumo huu kunashuhudiwa hadi kwenye nchi kubwa za kibepari kama Marekani na Uingereza hivyo nazo zimekumbwa tele na maandamano na fujo za raia wakilalamikia hali ngumu ya maisha.

**MASWALI**

a) Yape makala haya anwani mwafaka. (alama 1).
b) Eleza mtazamo wa wanasiasa kuhusu utepetevu wa mfumo huu. (alama 3)
c) "Ugatuzi nchini Kenya ni mfumo wa kibepari" Thibitisha kauli hii kwa kurejelea makala (alama 3)
d) Toa sababu zinazosababisha migomo na maandamano katika serikali za ugatuzi (alama 2)
e) Thibitisha jinsi mfumo wa ugatuzi umeongeza chumvi kwenye kidonda badala ya kutibu (alama 3)
f) Eleza maana ya maneno yafuatayo (alama 3)
i). Ugatuzi
Ii). Kibepari
iii). Ushuru

UFUPISHO (Alama 15)

Soma makala yafuatayo na ujibu maswali.

Mojawapo kati ya misingi na nguzo za maendeleo ulimwenguni ni viwanda. Viwanda ni muhimu kwa kuwa ndivyo vinavyoigeuza malghafi yanayopatikana na kuwa bidhaa zinazoweza kutumiwa na watu. Katika nchi zinazoendelea, ambazo hazina uwezo mkubwa wa mitaji, viwanda hivi vidogo kunatokana na sababu mbalimbali.

Nchi zinazoendelea huwa na masoko finyu hasa kwa kuzingatia uwezo wa ununuzi wa wanaolengwa na bidhaa za viwanda. Katika msingi huu, viwanda vikubwa vitawiwa vigumu kufanya biashara katika mazingira ambako masoko yake ni finyu au utashi wa bidhaa zake sio mkubwa. Viwanda vidogo pia vina uwezo wa kuwaajiri wafanyakazi wengi hasa kwa kuwa havina uwezo wa kugharamia mashine. Uajiri huu wa wafanyakazi wengi ni muhimu katika maeneo mengi ambako tatizo la uajiri ni mojawapo wa matatizo sugu. Tofauti na mataifa ya kitasnia, mataifa yanayoendelea hayana mifumo imara ya kuwakimu watu wasiokuwa na kazi utegemezi wa jamaa wanaofanya kazi kwa hivyo unakuwa nyenzo ya pekee ya kuyamudu maisha.

Kuanzisha viwanda vidogo vidogo hakuhitaji mtaji mkubwa tofauti na viwanda vikubwa. Hali hii inasahilisha uwezekano wa watu wengi kujasurisha shuughuli yoyote ile. Sambamba na suala hili ni kuwa ni rahisi kujaribisha bidhaa mpya kwa kiwango kidogo cha kiwanda kidogo. Ikiwa mzalishaji bidhaa mpya kwa mapana, kwa mfano kama ilivyo kwa viwanda vikubwa, pana uwezekano wa kupata hasara kubwa. Huenda utashi wa bidhaa hizo uwe mdogo ukilinganishwa na ugavi wa bidhaa zenyewe.

Majaribio mazuri huwa ni kwa kiwango kidogo. Kuwepo kwa viwanda vidogo huwa ni chocheo kubwa la usambazaji wa viwanda hadi maeneo ya mashambani. Hali hii inahakikisha kuwa nafasi za ajira zimesambazwa nchini hali ambayo inasaidia kuhakikisha kuwa pana mweneo mzuri wa kimapato nchini. Mweneo huu wa mapato unachangia katika kuboresha uwezo wa kiununuzi wa umma. Huu ni msingi muhimu wa maendeleo. Upanuzi na ueneaji wa viwanda vidogo vidogo ni msingi mkubwa wa kujitegemea kiuchumi. Aghalabu viwanda vikubwa huegemea kwenye mitaji ya mashirika ya kimataifa na huwa msingi wa kuendelezwa kwa utegemezi wa kiuchumi.

Licha ya faida zake, ueneaji au kutanda kwa viwanda hukabiliwa na matatizo mbalimbali. Tatizo la kwanza linahusiana na mtaji. Lazima pawepo na mbinu nzuri za kuweka akiba ili kuwa na mtaji wa kuanzishia biashara. Njia mojawapo ya kufanya hivi ni kwa kutegemea masoko ya mitaji ambayo katika mataifa mengi hayajendelezwa vyema. Inakuwa vigumu katika hali hii basi kupata pesa kwa uuzaji wa hisia kwenye masoko hayo.

Tatizo jingine linatokana na ukosefu wa mikopo ya muda mrefu ya kibiashara kwa wenye viwanda vidogo vidogo. Mikopo ya aina hii huwa muhimu hasa pale ambapo anayehusika ana mradi wa kununua vifaa kama mashine. Mikopo ya miuda mfupi binayop[atikana kwenye mabenki huweza kuwahinda wengi kutokana na viwango vya riba kwa juu. Haimkinikikwa viwada kama hivio kukopa kutoka nje ya nchi zao. Juhudi za kuendeleza vi2wanda hivi huweza pia kukwamizwa na tatizo la kawi kama vi;le umeme. Gharama za umeme huenda ziwe juu sana. Isitoshe, si maeneo yote ambayo yana umeme. Matataizo mengine huhusiana na ukosefu wa maarifa ya kibiashara, ukosefu wa stadi za ujasirimali au kuwa na ujasiri wa kujingiza kwenye shughuli Fulani na miundo duni.

Ili kuhakikisha kuwa viwanda vimekuzwa na kuwndelezwa pana haja ya kuchukua hatua kadha.Kwanza, kuwepo na vihamasisho kwa wanaoanzisha viwanda vidogo kama vile punguzo la kodi, kuhimiza kuanzishwa kwa viwada vidogo vidogo na kusaka kuyapanua masoko kwa ajili ya bidhaa zinazozalishwa na viwanda hivyo. Aidha kuanzishwa na kupanuliwa kwa taasisi za kuendeleza upanuzi huo. Pana haja ya kuwekeza kwenye raslimali za binadamu; kuelimishwa na kupanua uwezo wao wa kuyaelewa mambo mbalimbali. Miundo mingi haina budi nayo kupanuliwa na kuima5rishwa. Upo umuhimu pia wa kuongeza kasima inayotengewa maendeleo na ukuzaji wa viwada ili kuharakisha maendeleo yake pana umuhimu wa kupambana na ufisadi unaoweza kuwa kikwazo kikubwa. Inahalisi kutambua ikiwa viwanda nchini, uchumi wa nchi nao utawanda.

a) Kwa maneno 90 – 100, eleza ujumbe muhimu unaopatikana katika aya ya pili hadi ya nne. (alama 8,1 utiriko)
b) Kwa maneno (50 – 55) fafanua mambo yanayotinga ukuaji wa viwanda (alama 5, 1 utiririko)

**SARUFI NA MATUMIZI YA LUGHA – ALAMA 40**

a) i) Toa mfano wa konsonanti ambayo ni kipasuo kwamizo. (Alama 1)
ii) Taja kikwamizo ghuna cha kaakaa laini. (Alama 1)
b) Andika neno lenye muundo wa silabi ifuatao. (Alama 1)
I + KI + KKI +KI + KI
c) Tumia kivumishi kimilikishi cha nafsi ya pili wingi katika sentensi. (Alama 2)

for free revision past papers visit: www.freekcsepastpapers.com

d) Akifisha (alama 4)
aisee yale mawimbi ya tsunami yalipotokea bahari hindi yaliangamiza biashara nyingi sana alisema bomet

e) Changanua sentensi hii kwa njia ya msitari. (Alama 4)
Rais alihutubu lakini walipuuza.

f) Tofautisha kati ya kirai na kichazi. (Alama 2)

g) Bainisha yamnbwa na chagizo katika sentensi hii. (Alama 3)
Baba alimjengea nyumba ya matofali mwaka jana.

h) Nyambua vitenzi vifuatavyo katika kauli zilizowekwa katika mabano. (Alama 2)
i) Lia (Kutendea)
ii) ja (kutendea)

i) Onyesha kilalizo katika sentensi hii (Alama 1)
Mtoto huyu wangu amekuwa mwizi

j) Andika sentensi kwa msemo wa taarifa (Alama 2)
"Ah! Barabara hii hatari. Je, utaweza kuivuka? Lemashon aliuliza.

k) Andika kinyume cha maneno yaliyopigiwa mstari. (Alama 2)
Mama aliinjika chungu mekoni mvua iliponyesha.

l) Tambua matumizi ya kiambishi ji' katika sentensi ifuatayo. (Alama 3)
Kono la jitu hilo lililiwezesha kujilia chakula kingi kuliko mkimbiaji Yule

m) Ziweke nomino hizi katika ngeli zake (Alama 2)
i). Saa
ii). Nyasi

n) Andika sentensi ifuatayo katika hali ya ukubwa umoja. (Alama 2)
Nguso za vijana wale zilichujuka walipoanguka.

o) Unda nomino kutokana na vitenzi vifuatavyo. (Alama 3)
i). Zozana
ii). Saka
iii).Teta

p) Panda ni kuatika mbegu ardhi au kuparaga mti. Andika maana nyingine mbili. (Alama 2)

q) Andika sentensi hii upya bila kubadilisha maana ukitumia 'o' rejeshi. (Alama 1)
Mwanafunzi alitumwa nyumbani juzi na hajapata karo hadi leo.

r) Kwa kutumia shadda, onyesha maana mbili tofauti za neneo 'ala' (Alama 2)

for free revision past papers visit: www.freekcsepastpapers.com

**ISIMUJAMII – ALAMA 10**

1. Fafanua istilahi zifuatazo: (Alama 4)
   i) Lahaja
   ii) Lingua Franka
   iii) Misimu
   iv) Rejesta
2. Soma kifungu kifuatacho kasha ujibu maswali
   Sera : Hello. Ningependa kuongea na Mika.
   Sauti : Subiri kidogo nimpatie simu
   Sera : Hello.
   Mika : Hello. Sema Sera. Niko kwa mkutano…
   Sera : Pole kwa kukusumbua. Unakumbuka safari yetu ya kesho?
   Mika : Siwezi kusahau mrembo wangu. Si unakumbuka zile plan zetu?
   Sear : Nakumbuka. Siku poa.
   Mika : Bye.

   **Maswali**

a. Aina hii ya rejista huitwaje? (Alama 1)

b. Toa sifa za rejista ya aina hii. (Alama 5)

**CEKENA**
**KARATASI YA TATU /3**
**102/3**
**(Fasihi)**
**Muda: Saa 2 ½**
**TATHMINI YA MWISHO WA MUHULA WA PILI 2017 KIDATO CHA NNE**

**SEHEMU A**: **Kidagaa kimemuozea**

1. Lazima
   Wanyonge ndio wanyongwao ni kauli inayodhihirika vyema kupitia wahusika tofauti katika riwaya ya kidagaa kimemwozea. Jadili (Alama 20)

**SEHEMU B: Mstahiki meya**

Jibu swali la pili au la tatu

2. 'Lazima kwanza mnihakikishie kuwa huyo sumu hapati fununu ya jambo hili. Hii ni bomu inayo weza kutulipukia usoni'
   a) Eleza muktadha wa dondoo hili (Alama 4)
   b) Onyesha umuhimu wa mhusika anayerejelewa katika mazungumzo haya (Alama 4)
   c) Tambua tamathali inayojitokeza kwenye dondoo hili kisha uonyeshe mifano mingine Minne kwenye tamthilia hii. (Alama 10)
3. Ufisadi na tamaa ndio chanzo cha dhiki ya wanacheneo. Thibitisha kwa kirejelea matukio katika tamthilia nzima. (Alama 20)

**SEHEMU YA C** : **Hadithi fupi :- Damu nyeusi**

Jibu swali la 4 au la 5

4. "…………nilipiga dambini nyuma huko mambo yalianzia kiasi changu kujipata katika hali hii, takriban miaka saba ya nyuma………."
   a) Eleza muktadha wa dondoo hili (Alama 4)
   b) Miaka saba iliyopita hali ya anayerejelewa ilikuwaje? (Alama 5)
   c) Mambo yanayorejelewa ni yepi na yalianzaje? (Alama 5)
   d) Anayerejelewa qalifanya uamuzi gani kuhusu hali anayojikuta? (Alama 2)
   e) Eleza sifa za mrejelewa (Alama 4)
5. Huku ukirejelea hadithi tano katika diwani ya Damu Nyeusi, fafanua changamoto zinazowakumba vijana (Alama 20)

**SEHEMU YA D**: Ushairi

Jibu swali la 6 au 7

6. Kua.
   Sikia.
   Angalia.
   Bongo tumia.
   Hadaa dunia.
   Mwerevu hutulia.
   Mwenye pupa huumia.
   Papariko zinaudhia.
   Sura si kitu kujivunia.
   Ukiwa hujafa hujatimia.
   Mcheza na tope humrukia.
   Asiyetosheka mtumwa wa dunia.
   Roho mtoro ipendapo kukimbilia.
   Sudi si ya kulilia, siku ye huwadia.
   Watu wote ni sawa hakuna duni kwa Jalia.
   Achekapo mwenye meno kibogoyo huungulia.
   Zaidi mtu apatavyo ndivyo tama huzidia.
   Uangaliapo mbele ya kona kando yako angalia.
   Katika kuishi na wenzetu, sharti tuwe twavumilia.
   Hakuna motto wa haramu vitendo ndivyo haramia.
   Pasi na viganja viwili kofi haliwezikulia.
   Sikiliza ya wengi bali lako peke shikilia.
   Binadamu ni wa ila hapana alotimia.
   Asiyeridhika ni fukara kupindukia.
   Uongo sawa, ukweli watu hususia.
   Hakujna raha kamili kwenye dunia.
   Ajali huwezi kuitambikia.
   Ungali hujatenda fikiria.
   Maishani ya kuyanyatia.

for free revision past papers visit: www.freekcsepastpapers.com

Mali siyo ya kuringia.
Utu bora ni tabia.
Dhiki kuvumilia.
Sipende kulia.
Fikiria.
Wazia.
Tua.

**Maswali**

a) Shairi hili ni la aina gani? (alama 1)
b) Taja lengo la mshairi (alama 2)
c) Kwa nini utungo huu unachukuliwa kuwa shairi? (alama 3)
d) Eleza jinsi mshairi alivyoshughulikia dhana zifuatazo:
   i). Tamaa
   ii). Bahati
   iii). Umaskini (alama 3)
e) Kwa kutoa mifano, onesha mbinu mbili za kifasihi zilizotumiwa na mshairi (alama 4)
f) Ni ipi hadhira lengwa ya shairi hili? (alama 2)
g) Kwa kutoa mfano eleza maana ya dhana hizi:
   Mishororo Mishata
   Mishororo Kivu (alama 4)
h) Eleza maana ya msamiati
   'Jalia" (alama 1)

7. Shuleni nimechelewa, sababu kaelezea,
Gari meharibikiwa, saa tatu metimia,
Mwalimu hakuelewa, adhabu kanipatia,
Majira ndo badilika, sio utu Waafrika.

Mama ana mzigowe, na amebeba pachawe,
'Naomba nisaidiwe, mia mbili poa mamawe!'
Mzigo ndo asaidiwe, lazima pesa atowe,
Majira ndo badilika, sio utu Waafrika.

Chamani wamekutana, wanawake waongea,
Mwenzao anaungana, nao wamuondokea,
'Mwizi unaye ka bwana', mmoja amuambia,
Majira ndo badilika, sio utu Waafrika.

Wazazi wanaingia, magari wanatumia,
Mamangu namgonjea, kwa miguu aingia,
Wenzangu wanichekea, kisha wananibagua,
Majira ndo badilika, sio utu Waafrika.

Swali akaniuliza, jibu nikampatia,
Kaanza kunijibiza, eti kamuongopea,
Mbona basi kauliza, jibu kanikaripia,
Majira ndo badilika, sio utu Waafrika.

Akakosa cha kulambwa, hana hata huo unga,
Wewe hata ukiombwa, unakataa kwa ngenga,
Wasahau tumeumbwa, naye Mungu si mganga,
Majira ndo badilika, sio utu Waafrika.
Waafrika tupendane, ja zama za wetu babu,
Kwa umoja tushikane, kwa shida na kwa taabu,
Kikosa tukosoane, kihaki kistaarabu,
Majira ndo badilika, sio utu Waafrika.

Watu tusaidiane, raha ni tukipeana,
Binadamu tufunzane, tuishi tukifaana,
Chakula na tupeane, ndo vidonda vitapona,
Majira ndo badilika, sio utu Waafrika.

for free revision past papers visit: www.freekcsepastpapers.com

**MASWALI**

a. Nafsi- neni ametumia toni gani? (alama 2)
b. Tambua walengwa wa shairi hili (alama 3)

c. Ni kwa jinsi gani Wafrika wamebadilisha utu? (alama 4)
d. Malenga ana ushauri upi kwa Wafrika katika ubeti wa saba? (alama 3)
e. Hku ukitoa mifano, onyesha idhini ya mshairi katika shairi hili (alama 6)
f. Tambua tamathali mbili za lugha zilizotumika katika shairi hili (alama 2)

**SEHEMU YA E**

8. a) Huku ukionyesha udhaifu na uzito wa kila njia fafanua njia mbalimbali za kuhifadhi kazi za fasihi simulizi. (Alama 9)
b). Eleza maana ya maigizo (Alama 4)
c). Eleza vizingiti vinne vinavyokumba fani ya ngomezi (Alama 4)
d). Eleza dhima ya Miriga (Alama 5)

for free revision past papers visit: www.freekcsepastpapers.com

**JARIBIO LA TATHMINI YA KIGUMO 2017 KIDATO CHA NNE.**
**102/1**
**KISWAHILI**
**KARATASI 1**
**KIDATO CHA NNE**
**JULAI/AGOSTI 2017**

1. **Lazima**
   Swala la matumizi ya pombe haramu limekuwa tatizo sugu nchini Kenya. Mwandikie barua mhariri wa gazeti la Mzalendo ukitoa sababu za uraibu huu na suluhu mwafaka.
2. Jadili hatua zinazoweza kuchukuliwa kukabiliana na ukabila nchini Kenya.
3. Siku ya kufa kwa nyani, miti yote huteleza.
4. Nilijaribu kuuinua mguu wangu uliojaa maumivu……

**JARIBIO LA TATHMINI YA KIGUMO 2017 KIDATO CHA NNE.**
**102/2**
**KARATASI YA PILI**
**LUGHA**
**JULAI 2017**
**MUDA: SAA 2–**

1. **UFAHAMU** (Alama 15)

**Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali**.

Gari lake kuukuu lilikuwa linapambana na barabara yenye mashimo yaliyoshiba na kutapika maji ya mvua ambayo sasa ilikuwa inaanza kupusa. Japo daima alipambana na usukani kunako mashimo haya yaliyotosha kuitwa magenge, alishukuru kwa hali hii. Vipi angeweza kulidhibiti gari lake hili kwenye barabara iliyosakafiwa nayo ikahitimu? Magurudumu haya yaling'ora kama upara wa shaibu aliyekula chumvi hadi ikamwogopa yangetii uelekezi wake? Mara ngapi hili limetaka kumwasi barabarani? Haya yalikuwa baadhi ya maswali yaliyompitikia akilini. Hakujitakilifu kutaka **kuyapa mji** maana mara ile mawazo yake yalitekwa na kubwagwa katika nchi ya mbali – nchi ambayo sasa aliiona kama sinema akilini mwake.

Alipofika nyumbani aliliegesha gari lake na kufululiza ndani. Siku mbili zilikuwa zimepita akiwa pale kazini. Madaktari kama yeye hawakuwa wengi. Alikuwa miongoni mwa madaktari wenye ujuzi katika hospitali hii ya kitaifa. Wenzake wengi walikuwa wamehamia ughaibuni walikokwenda kutafuta maisha. Mshahara wao mkia wa mbuzi uliwasukuma na kuwatema nje ya nchi yao. Wengi wa waliohamia ng'ambo waliona vigumu kubaki katika ajira ambayo kivuno chake kilishindwa kumvusha mtu hata nusu ya kwanza ya mwezi. Malalamishi ya kulilia ujira wa heshima yaligonga kwenye maskio yaliyotiwa zege. Na kweli wanavyosema, mwenye macho haambiwi tazama. Basi walitazama hapa na pale wakaona penye mianya ya matumaini, nao wakaiandama.

Hadi leo hii hamna la mno lililofanyika. Ndiyo maana Daktari Tabibu anarudi nyumbani tangu kuingia kazini hiyo juzi alfajiri. Hafanyi kwa kuwa katosheka, maana pia yeye ana dukuduku.

Ana shaka ya mustakabali wake ikiwa mazingira ni haya ya kumsoza, maana umri nao unazidi kumla. Japo anatia na kutoa, mizani ya hesabu yake imeasi ulinganifu.

Daktari Tabibu waama ni mfungwa. Ametekwa na kuzuiwa katika kupenda na kuchukia mambo. Ni kama mti ulioduwaa. Anatamani barabara nzuri za lami. Anatamani mshahara wa kumwezesha kukidhi mahitaji yake na kutimiza majukumu yake ya kimsingi. Jana amesema na rafiki yake aliye ng'ambo kwa simu ambayo sasa imetulia mkabala naye. Ingawa mwenzake huyu alikuwa mchangamfu na kumkodolea hali maisha ya kuridhisha kule ugenini kama vile wanataaluma kuenziwa, yapo vilevile yaliyomtia unyonge moyoni. Upweke ndio uliomtia **fukuto** kuu. Licha ya hela zote hizo za kupigiwa mfano, watu hawana muda wa kutembeleana na kujulikana hali au hata kukutana tu mkahawani wakashiriki mlo. Eti ni kila mtu na hamsini zake. Halafu ipo changamoto ya hali ya hewa. Baridi ya ng'ambo haifanyi mzaha katika kumtafuna mtu. Ni hali tofauti na ile aliyoizoea.

Daktari Tabibu alizitia kauli za rafiki yake kwenye mizani ya moyo wake. Akawaza ikiwa kweli si bora kulemazwa na mzizimo ugenini badala ya kuishi katika kinamasi cha kuumbuliwa nyumbani. Kisha punde lilimjia wazo la marehemu nyanyake na wengine kama yeye waliofadhili masomo yake kupitia kwa serikali na njia ya kodi. Je, si usaliti huu? Vipi aikimbie nchi kabla ya kuihudumia ilihali imemjengea hadi kuwa daktari? Na je, wafanyakazi wake wa nyumbani watakwenda wapi? Atawaambiaje kuwa sasa hahitaji huduma zao kwa kuwa anakimbia nchi yake?

for free revision past papers visit: www.freekcsepastpapers.com

Mawazo yake yalikatizwa na simu iliyolia na kumshtua. Alipoitazama aliiona imeng'ara kwa mwangaza ulioweka wazi jina la mpigaji. Alifahamu kuwa leo hii tena dharura nyingine ilikuwa inamwalika hospitalini. Mwili wake ulimsaliti ingawa moyo wake ulimkumbusha kuwa lisilo budi hutendwa. Hapo ndipo alipoiinua ile simu tayari kusema na mwenzake upande wa pili.
"Haloo!" Sauti nyororo kutoka upande wa pili iliita.
"Haloo!"
"Naam! Dharura nyingine tena daktari. Unaombwa kuokoa maisha mengine tena!"
"Haya. Ila mwanzo nitahitaji kujimwagia maji", na pale pale akaikata ile simu.
Daktari Tabibu aliingia hamamuni huku kajifunga taulo kiunoni tayari kuoga. Aliyafungulia maji lakini ule mfereji uligoma kutapika maji. Ulikuwa umekauka kabisa. Daktari Tabibu aliduwaa pale. Aliufunga ule mfereji kabla ya kuiaga bafu.

**Maswali.**

a) Eleza sababu nne zinazowafanya wataalamu kuhamia nchi za kigeni (al. 4)
b) Hakuna masika yasiyokuwa na mbu. Thibitisha kwa kurejelea hali ya waliohamia ng'ambo. (al. 3)
c) Taja athari tatu zinazokumba nchi ya msimulizi kupitia uhamiaji wa wataalamu katika mataifa ya kigeni. (al. 3)
d) Kwa nini Daktari Tabibu akapitisha siku mbili mfululizo pale kazini. (al. 3)
e) Fafanua mafungu yanayofuata kama yalivyotumika katika taarifa (al. 2)
   I. Kuyapa mji
   II. Fukuto

2. **UFUPISHO**

**Soma Makala yafuatayo kisha ujibu maswali yatakayofuata.**

Watoto wa mitaani ni watoto wanaorandaranda kwenye barabara za mji au mitaa wakitafuta vyakula na usaidiziwa aina yoyote kutoka kwa wakazi wa maeneo hayo. Watoto hawa wamepachikwa lakabu maarufu 'chokora'. Watoto hawa hutoka wapi? Je, wanazaliwa mitaani?
Kuna vyanzo mbalimbali vya watoto hawa: ikiwa ni ukahaba, baadhi ya wazazi wa watoto hawa ni makahaba ambao kwa bahati mbaya wanapotungwa mimba na wakashindwa kuavya huishi kuzaa wanaharamu ambao huwalea kwa muda wa miaka mitatu na kisha kuwarusha mitaani.
Asili nyingine ya watoto wa mtaani ni kuvunjika kwa ndoa: wazazi wanapotengana watoto hukosa mihimili na hivyo kushika hamsini zao hadi mtaani kutafuta usaidizi. Sababu nyingine ni watoto wanaoachwa na wazazi wao (mayatima) baada ya wazazi hawa kuaga dunia. Hawa hukosa mtu wa kuwashughulikia na hatimaye hujipata mitaani.
Asili nyingine ni familia maskini ambazo hushindwa kutimiza mahitaji ya kimsingi ya watoto na hatimaye watoto hawa wakaishia mitaani. Vilevile kuna watoto wanaozaliwa mitaani kutokana na wanaume na wanawake ambao wameishi mitaani hadi wakawa wazazi.
Watoto wa mitaani hukumbwa na matatizo chungu nzima. Wao hukosa chakula, mavazi na malazi. Hawana mahali pa kulala hivyo basi wanajinyata kwenye mitaro ya maji taka na kwenye mijengo ambayo haijakamilika kujengwa au magofu ya nyumba huku wakibugunywa na baridi na hatimaye hupata maradhi ya kila aina. Usalama kwao ni msamiati usioweza kugonga vichwa vyao.
Suala la watoto wa mitaani ni kero kwa kila anayetumia huduma za mjini. Watoto hawa hupamba mji kwa sura mbaya ambayo huchora taswira ya jamii katili isiyothamini ubinadamu. Baadhi ya 'chokora' hutumia lugha chafu na vitisho katika kuomba usaidizi kutoka kwa adinasi wapitanjia. Swali linalopita kwenye akili ya watu wengi ni je, hali hii itakomeshwa vipi?
Uwepo wa watoto mitaani ni tatizo la kijamii hivyo basi linahitaji kila mwanajamii kuhakikisha ametoa mchango madhubuti kukomesha tatizo hili. Wanajamii wanafaa kuwa waadilifu, wajiepushe na ukahaba na ngono za kiholela. Aidha, kila mtu anafaa kutia bidii kutafuta riziki na pia kupata idadi ya watoto anaoweza kuwalea bila usumbufu. Watoto mayatima nao walelewe na jamaa wa mzazi wao. Wasio na jamaa wapelekwe kwenye mashirika ya kutunza watoto. Watoto ambao tayari wako mitaani wasaidiwe na serikali kupata makao na ajira. Tukifanya hivyo mitaa yetu itakuwa nadhifu, salama na mahali pazuri pa kuishi.

a. Ukiangazia mambo muhimu pekee, fupisha aya tatu za kwanza. Tumia maneno 70. (al. 6) (utiririko al. 1)
b. Eleza matatizo ya watoto mitaani na uonyeshe jinsi ya kukabiliana na kero hili. Tumia maneno 70-80. (al. 7) (al. 1 utiririko)

3. **MATUMIZI YA LUGHA.** (Alama 40)

a. Bainisha sifa mbili kwa kila mojawapo ya sauti zifuatazo. (al. 2)
   /e/
   /th/
b. Eleza maana ya silabi mwambatano na utoe mfano. (al. 2)
c. Bainisha mofimu katika fungu linalofuata sikumtibia (al. 3)
d. Eleza matumizi ya **kwa** katika sentensi zifuatazo. (al. 2)
   Nilisafiri kwa kuhudhuria mkutano.
   Alisoma kitabu kwa haraka sana.
e. Eleza matumizi mawili ya kiambishi ji- (al. 2)
f. Yakinisha:
   Hatacheza wala kutuzwa. (al. 2)
g. Kwa kuitoa mfano taja miundo miwili ya ngeli ya LI – YA (al. 2)
h. Andika kinyume cha sentensi ifuatayo.
   Mwafrika anapenda kutii maagizo. (al. 2)

for free revision past papers visit: www.freekcsepastpapers.com

i. Taja visawe viwili vya neno <u>uzembe</u> (al. 2)

j. Changanua sentensi ifuatayo kwa kutumia jedwali. (al. 4)
Alisoma kitabu kilichokuwa mezani.

k. Andika sentensi ifuatayo katika udogo wingi. (al. 3)
Uichukue hiyo nguo yako pamoja na kiatu kichafu na uondoke hapa.

l. Tambua vitenzi katika sentensi hii na utaje ni vya aina gani. (al. 2)
Mwizi alijaribu kujinasua.

m. Onyesha aina za shamirisho katika sentensi ifuatayo. (al. 3)
Seremala alimtengenezea baba kiti kizuri kwa mbao.

n. Andika katika msemo wa taarifa. (al. 3)
"Mimi nitawakaribisha wageni leo jioni kisha nitaondoka kwenda kwangu kesho." Maria alimwambia Njeru.

o. Amrisha katika wingi. (al. 1)
Nywa-

p. Andika katika hali ya –a- (al. 1)
Kitabu hupatikana maktabani.

q. Tambua virai katika fungu linalofuata. (al. 2)
Mkubwa mno anacheza vizuri.

r. Unda nomino moja kutokana na kitenzi <u>tafakari</u>. (al. 1)

s. Kamilisha methali ifuatayo. (al. 1)
Mwenye shoka ………………………………………………………………………………..

4. **ISIMU JAMII.**

a. Ni nini tofauti kati ya kuchanganya msimbo na kubadili msimbo. (al. 2)

b. Eleza sababu zinazochangia kubadili na kuchanganya msimbo. (al. 8)

for free revision past papers visit: www.freekcsepastpapers.com

**JARIBIO LA TATHMINI YA KIGUMO 2017 KIDATO CHA NNE.**
**102/3**
**KISWAHILI**
**KARATASI YA TATU**
**FASIHI**
**JULAI/AGOSTI 2017**

1. **SEHEMU A: USHAIRI** (LAZIMA) (Al. 20)

Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali yanayofuata.

**Mwanangu sikubali.**
Mwanangu, wenye dhambi vishawishi, vikejeli
Mwanangu, katu wasikusawishi, bilikuli
Mwanangu, aushi nawe uishi, kama mwali
Mwanangu sikubali!

Mwanangu, sherati sikuperembe, kakubali
Mwanangu, usiwache wakubembe, kwa sali
Mwanangu, mithiliyo mapembe, ya fahali
Mwanangu sikubali!

Mwanangu, wajeuri siwe nao, ni shubili
Mwanangu, usifwate njia zao, pita mbali
Mwanangu, ujeuri sera yao, mazohali
Mwanangu sikubali!

Mwanangu, waongo usiwasifu, kulihali
Mwanangu, uongoubatilifu, si amali
Mwanangu, ndimi zao hazikufu, si manzili
Mwanangu sikubali!

Mwanangu, wafisadi siwe nao, kemikali
Mwanangu, tamaa ndo utu wao, si injili
Mwanangu, wahepe kila uchao, kiakili
Mwanangu sikubali!

Mwanangu, wote waliowabaya, wanadhili
Mwanangu, usije ukawapeya, ikibali
Mwanangu, katika hino duniya, kaa mbali
Mwanangu sikubali!

for free revision past papers visit: www.freekcsepastpapers.com

**Maswali**

a) Taja kwa ufafanuzi bahari nne zinazobainika katika shairi hili. (al. 4)
b) Andika ubeti wa tatu katika lugha tutumbi. (al. 4)
c) Fafanua umbo la ubeti wa 6. (al. 4)
d) Tambua toni ya shairi hili. (al. 2)
e) Tambua huru tatu za kishairi zilizotumika katika shairi. (al. 3)
f) Fafanua dhamira ya shairi hili. (al. 2)
g) Tambua nafsi neni na nenewa. (al. 1)

**SEHEMU YA B: RIWAYA – KIDAGAA KIMEMWOZEA – KEN WALIBORA.**
Jibu swali la pili au la tatu.

2. "Kitanda usichokilalia hukijui kunguni wako"
    a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (al. 4)
    b) Onyesha ukweli wa kauli hii kwa mujibu wa dondoo hili. (al. 4)
    c) Eleza sifa za msemaji wa kauli hii. (al. 8)
    d) Fafanua umuhimu wa anayeambiwa maneno haya (al. 4)
3. Jadili nafasi ya vijana katika kuleta mabadiliko katika jamii. (al. 20)

**SEHEMU YA C: TAMTHILIA – MSTAHIKI MEYA – TIMOTHY AREGE.**

Jibu swali la nne au la tano.

4. "Si vyombo vya habari, Si wanasiasa, Si wasomi."
   a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (al. 4)
   b) Taja na ufafanue mbinu ya lugha katika dondoo hili. (al. 2)
   c) Fafanua sifa zozote nne za msemaji. (al. 4)
   d) Umaskini ni tatizo kuu katika mji wa cheneo. Tetea huku ukitoa mifano mahususi. (al. 10)
5. Kwa kurejelea wahusika wowote watano onyesha jinsi unafiki unavyodhihirika katika tamthilia ya Msatihiki Meya. (al. 20)

**SEHEMU YA D: HADITHI FUPI**
**Damu Nyeusi na Hadithi Nyinginezo**
**K. Walibora na S.A Mohammed**
**Jibu swali la 6 au la 7**

6. Elimu imeshindwa kutimiza lengo la kuwapa vijana uwezo wa kukabiliana na maisha ya kisiasa. Thibitisha kauli hii kwa kurejelea hadithi zifuatazo.
   a) Mke Wangu.
   b) Samaki Wa Nchi Za Joto.
   c) Damu Nyeusi.

7. "Ulijuaje alikuwa anaangalia kwetu?'
   a) Eleza muktadha wa dondoo hili (al. 4)
   b) Hadithi hii inaonyesha matatizo ya kijamii. Fafanua (al. 8)
   c) Eleza yaliyotokea baada ya mazungumzo haya. (al. 8)
8.
   a) Eleza sifa za mtendaji wa ulumbi. (al. 8)
   b) Fafanua umuhimu wa maigizo katika jamii. (alama 12)

for free revision past papers visit: www.freekcsepastpapers.com

**WESTLANDS GRAPHICS**
102/1
**KISWAHILI**
Karatasi 1
(Insha)
Julai 2017
**Muda: Saa $1^3/_4$**

1. **Lazima**

Hivi karibuni suala la ukosefu wa chakula limekuwa tatizo linalokera jamii. Mwandikie barua mhariri wa gazeti la Mwangaza ukieleza chanzo cha kero hiyo na suluhu mwafaka.

**2.** Teknolojia mpya ina madhara mengi kuliko faida kwa vijana. Jadili.

**3.** Andika kisa cha kudhibitisha ukweli wa methali;
Kazi mbi si mchezo mwema.

**4.** Tunga kisa kinachomalizia kwa maneno haya:
... hakika ilikuwa siku njema kwangu kukutana naye hata nikamshukuru Mola kunipa fursa hiyo.

for free revision past papers visit: www.freekcsepastpapers.com

**WESTLANDS GRAPHICS**
**KISWAHILI**
**102/2**
**Karatasi 2**
**Julai 2017**
**Muda: Saa 2½**

1. **UFAHAMU**

**Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.**

Takwimu ambazo zimetolewa na Shirika la Kazi la Kimataifa (ILO) zinaonyesha kuwa ulanguzi wa watoto umetangaa hususan katika mataifa yanayoendelea. Ipo tumbi ya sababu za kuelezea kwa nini biashara hii imeshamiri.

Athari mojawapo ya utandawazi ni kuunda mtandao mpana ulimwenguni. Mtandao huo unaweza kutumiwa kwa njia chanya au njia hasi. Njia chanya ni zile zinazoukiliwa kuwafaidi wanajamii kwa kuendeleza ubinadamu na kuboresha hali ya maisha kiuchumi, kisiasa na kitamaduni. Maarifa yanayosambazwa huweza kuwa <u>chachu ya kuumua ari ya maendeleo,</u> elimu na mafanikio katika mataifa mengi ulimwenguni. Njia hasi ni zile ambazo <u>maarubu</u> yake ni kuwanufaisha wachache huku zikiwahasiri wengi.

Kuwepo kwa mtandao kunawapa wenye nia tule karna usafirishaji na ulanguzi wa watoto fursa ya kuzitosheleza hawaa zao. Wanaoshiriki katika biashara hii huongozwa na <u>pashau y</u>a utajiri. Hawachelei kuwalangua watoto wanaochimbukia mataifa ya kimaskini huko ughaibuni wanakozongomezwa kwenye madanguro, kufanyishwa kazi za sulubu na za kitopasi na kuishi maisha duni.

Asilimia kubwa ya watoto hurubuniwa kwa ahadi ghushi za kujiendeleza kimasomo. Wengine huuzwa kutokana na msaadawa jamaa zao wanaotovukwa na utu na kuwa mawakala katika amali hii ya kusikitisha. Biashara hii huweza kusahilishwa kwa kuwepo kwa mfumo fisadi wa kisheria, msambaratiko wa muundo wa jamaa na ubinafsi wa kijamii.

Ipo haja kubwa ya ushirikiano wa mataifa alkulihali kuikomesha biashara hii haramu. Jamii ya ulimwengu isipofanya hivi, itakuwa imekitia kizazi kizima kitanzi na kuitumbukiza kesho yake kwenye matatizo kathiri.

**a)** Ni kwa jinsi gani utandawazi umechangia katika biashara ya ulanguzi wa watoto. (alama 2)
**b)** Mwandishi wa kifungu anapendekeza hatua zipi kusuluhisha tatizo la ulanguzi wa watoto ? (alama 3)
**c)** Eleza jinsi watoto wanaolanguliwa wanavyoishi huko ughaibuni. (alama 3)
**d)** Kulingana na muktadha, kifungu "chachu ya kuumua ari ya maendeleo" kina maana gani ? (alama 2)
**e)** Jamii isiyosuluhisha tatizo la ulanguzi wa watoto itakuwa na hatima gani ? (alama 3)
**f)** Eleza maana ya : (alama 2)
    i) maarubu
    ii) pashau

## 2. UFUPISHO

**Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.**

Katika ulimwengu huu tunaoishi wenye hekaheka nyingi, mwanadamu anaendeshwa na maisha mfano wa gurudumu la gari. Kwa watu watu wenye kufanya kazi katika mazingira ya ofisi ambapo wanaketi mchana kutwa, mazoezi ni muhimu sana. Baadhi ya watu huona fahari wapigapo tai na kuelekea au kutoka kazini kwa gari. Tabia hii ya mwanadamu inamsahaulisha kuwa mwili wake ulidhamiriwa kufanya mazoezi ya viungo kwa kutembea au kufanya kazi zenye kuhitaji misuli kupashwa rnoto. Watu wengi hawana habari kuwa mazoezi yana faida tele kwao.

Wataalamu wa sayansi wamebainisha kuwa watu wanaoidhiki miili yao kwa mazoezi ya mara kwa mara huishi zaidi kuliko wasiofanya mazoezi. Watu hawa huwa wamo katika hali nzuri ya afya na wenye nguvu kuliko wale ambao hawaishughulishi miili yao kwa mazoezi au kazi zinazohitaji utumiaji nguvu.

Ni dhahiri kwamba mazoezi huchochea kuundwa kwa seli mpya za ubongo. Utafiti wa kisayanisi umebainisha kuwa sehemu za ubongo zenye kusisimuliwa kwa mazoezi ndizo hutekeleza jukumu la kukumbuka na kujifunza. Bila mazoezi sehemu hizi zitashindwa kukumbuka au kujifunza maarifa mapya. Vile vile, imethibitishwa kwamba watu wanaoshiriki shughuli zenye kuwahitaji kutumia nguvu hutia fora katika mambo yanayowahitaji kukumbuka, kufanya maamuzi, pamoja na kusuluhisha matatizo.

Hali kadhalika, mazoezi huimarisha siha ya binadamu. Mathalani, matatizo ya moyo yanaweza kukabiliwa kwa kufanya mazoezi ya viungo. Kufanya mazoezi mara kwa mara huufanya moyo kuwa imara na kuuwezesha kutekeleza jukumu lake ipasavyo. Ifahamike kwamba moyo wenye siha huweza kupiga kiasi kikubwa cha damu bila ya juhudi kubwa. Hili bila shaka litamkinga binadamu dhidi ya kulemewa na kazi.

Isitoshe, kushiriki mazoezi au shughuli zenye kutumia nguvu mara kwa mara huuweka mwili katika hali nzuri ya kupambana na magonjwa. Utafiti wa kisayansi umeonyesha kuwa shughuli kiasi zinazomhitaji mtu kutumia nguvu, pamoja na upunguzaji wa uzito, na uzingatiaji wa lishe bora, huweza kupunguza uwezekano wa kupata ugonjwa wa kisukari kwa baina ya asilimia 50 na 60. Mazoezi hayapunguzi tu shinikizo la damu, bali pia hatari ya kupata kiharusi. Aidha, kufanya mazoezi mara kwa mara husaidia kudhibiti uzani wa mwili. Mtu anapokula kiasi cha chakula kinachozidi mahitaji yake ya

kimwili huweza kujinenepea na kushindwa kutekeleza majukumu ya kimsingi. Mazoezi husaidia kuzichoma kalori zisizohitajika mwilini. Hatua hii, licha ya kusaidia kupunguza uzani, huvisisimua viungo vya mwili. Matokeo ya haya ni utendakazi wa hali ya juu bila kuchoka. Vilevile mwili unaofanya mazoezi haudorori. Umbo la mtu anayefanya mazoezi hupendeza.

Juu ya hayo, kufanya mazoezi mara kwa mara husaidia kujenga misuli yenye nguvu. Misuli inapokuwa na nguvu tunaweza kulifanya jambo kwa muda mrefu bila kuchoka. Mbali na misuli kuimarika, mazoezi na shughuli zinazohitaji utumiaji nguvu husukuma hewa na virutubisho kwenye viungo mahususi vya mwili na kuvisaidia kufanya kazi vyema zaidi.

Hali kadhalika, mazoezi husaidia kujenga mifupa. Kadiri binadamu anavyoshiriki katika shughuli kama vile kuruka, ndivyo anavyoiimarisha mifupa yake. Shughuli ya aina hii huipa mifupa uzito ambao unaiwezesha kukua na kujengeka ikiwa na nguvu. Mazoezi pia hukawiza kudhoofika kwa mifupa.

Kunyooshanyoosha viungo nako hnchangia kuufanya mwili kuwa imara na wenye kunyumbuka. Hali hii ya mwili hupunguza uwezekano wa kupata majeraha. Mwili usionyumbuka humfanya mtu ashindwe kutekeleza hata shughuli nyepesi zinazomhitaji kutumia nguvu. Si ibra kupata kwamba kuitekeleza shughuli ndogo tu humfanya mtu kupata maumivu.

Utulivu wa akili nao huweza kupatikana kwa kufanya mazoezi. Imebainishwa kwamba kufanya mazoezi kwa angalau dakika thelathini kwa muda baina ya siku tatu na tano kwa wiki hupunguza kwa kiasi kikubwa, dalili za unyong'onyevu. Na je, wajua kwamba kufanya mazoezi husaidia kupata usingizi

Mazoezi ni mfano wa bembea inayokutuliza na kukupa usingizi. .

Mke ni nguo, mgomba kupaliliwa. Nao mwili wa binadamu, kama mgomba, unahitaji

kushirikishwa katika mazoezi ili kuuwezesha kuwa na hamu ya kutenda kazi.

**a)** Kwa kurejelea aya tano za kwanza, eleza matatizo ya kiafya yanayoweza kupatikana kwa kutofanya mazoezi. (Maneno 100) (alama 9, 1 mtiririko)

**b)** Fupisha ujumbe wa aya tano za mwisho kwa maneno 80. (alama 6, 1 mtiririko)

for free revision past papers visit www.freekcsepastpapers.com

**3. MATUMIZI YA LUGHA (ALAMA 40)**

**a)** Tunga sentensi moja ukitumia nomino dhahania. (alama 2)

**b)** Unda nomino kutokana na vitenzi :

i) chelewa ........................................................................................................... (alama 1)

ii) andika ............................................................................................................. (alama 1)

**c)** Onyesha hali katika sentensi zifuatazo:

i) Huenda mvua ikanyesha leo. (alama 1)

ii) Miti hukatwa kila siku duniani. (alama 1)

**d)** Andika sentensi katika udogo na ukubwa ukitumia neno kiti. (alama 2)

**e)** Tunga sentensi inayoldhihirisha matumizi ya ngeli ya I-I (alama 1)

**f)** Taja sauti mbili zinazotamkiwa katika kaakaa laini. (alama 2)

**g)** Changanua sentensi hii kwa mchoro wa matawi.
Maria alikutana na mwalimu aliyemfunza Kiswahili. (alama 4)

**h)** Tambua na ueleze aina ya vitenzi katika sentensi ifuatayo :
Kalamu aliyokuwa nayo mwalimu ni ya mwanafunzi. (alama 2)

**i)** Tambua mzizi katika neno "msahaulifu" (alama 1)

**j)** i) Fafanua maana ya "mofimu huru" (alama 1)

ii) Toa mfano mmoja wa mofimu huru (alama 1)

**k)** Eleza maana mbili za sentensi hii:
Rehema alimpigia mwanawe simu. (alama 2)

**l)** Unda kitenzi kutokana na neno: sahihi (alama 1)

**m)** Andika kwa usemi wa taarifa : (alama 3)
"Nitakuarifu nikimwona," Halima alisema.

**n)** Tunga sentensi ukitumia kivumishi cha nomino. (alama 1)

**o)** Tambua kiambishi awali na tamati katika neno :
alaye (alama 2)

**p)** i) Eleza maana ya shadda. (alama 1)

ii) Onyesha panopowekwa shadda katika maneno haya:

i) Mahakamani

ii) Nchi

**q)** Andika kinyume cha :
Msichana mrefu ameingia nyumbani kwa haraka. (alama 2)

**r)** Ainisha shamirisho na chagizo katika sentensi:
Mwanariadha ameshinda tuzo kwa ustadi. (alama 2)

**s)** Tambua virai katika sentensi hii:
Tajiri yule mwenye mali nyingi alishinda zawadi jana asubuhi. (alama 3)

**t)** Onyesha matumizi ya 'ku' katika sentensi hii:
Matata atakuletea zawadi akitoka kule kwao. (alama 2)

**4. ISIMUJAMII**

Tambua aina ya makosa ya lugha katika sentensi zifuatazo kisha uyarekebishe. (alama 10)

a) Mbamba yangu alinipiga mbure

b) Watoto wakumi waliumia katika ajali.

c) Kanyumba hako katabomolewa leo.

d) Sijui tutakula nini leo nimekuwa broke.

e) Mwalimu wetu hapendangi mchezo.

for free revision past papers visit: www.freekcsepastpapers.com

**WESTLANDS GRAPHICS**
**102/3**
**KISWAHILI**
**KARATASI YA TATU**
**FASIHI**
**JULAI/AGOSTI 2017**

**SEHEMU A : USHAIRI**

**1.** **LAZIMA**

**Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.**

**Wanaume ni wanyama**

1. Nakumbuka vyema sana, sisahau siku ile
Nilipoitwa na nina, akanipa ya kivyele
Mwanangu umsichana, nakuasa usikile
Si watu waone vile, wanaume ni wanyama.

2. Kuwa umevunja ungo, ni hali ya maumbile
Bora uwapo na bongo, anasa uzikimbile
Ukijitia maringo, utatungwa mimba mbele
Si watu waone vile, wanaume ni wanyama.

3. Ngawa waje na manoti, "Nakupenda" wakwambile
Wakuvalie makoti, usiwaachie mbele,
Hata wapige magoti, wambile mna kelele
Si watu waone vile, wanaume ni wanyama.

4. Ngono ni tendo la suna, Amina sikimbilile
Wala miguu halina, kwamba lingekukimbile
Muhimu kwako Amina, kwanza uthamini shule
Si watu waone vile, wanaume ni wanyama.

5. Kuzurura mitaani, si tabia njema ile
Unapotoka nyumbani, fululiza hadi shule
Si kwenda vichochoroni, kuwaona kina wale
Si watu waone vile, wanaume ni wanyama.

6. Uwe mwana msikizi, yano uyazingatile
Mengine kuhusu penzi, mwanangu taonywa shule
Kama marneyo mzazi, nimekuonya kimbele
Si watu waone vile, wanaume ni wanyama.

7. Wakaja kina Harnadi, mwana wa Mzee sule
Kwangu wakapiga hodi, hata rnkuu wa shule
Ila nikajitahidi, kukwepa mitego ile
Si watu waone vile, wanaume ni wanyama.

8. Na kuna huyo Karisa, mwanfunzi kule shule
Akawa hunipapasa, nami pia vile vile
Mwishowe ikatupasa, tugawe tunda tule
Si watu waone vile, wanaume ni wanyama.

9. Nani akachovya uto, wa asali tarnu vile
Na kisha aape kuto, kula asali milele
Kuwa ni mjarnzito, wamenifukuza shule
Si watu waone vile, wanaume ni wanyama.

10. Karisa yu vilevile, angali yuwaenda shule
Na mie kitumbo mbele, ninajikuna upele
Yameshatimia yale, niloonywa siku ile
Si watu waone vile, wanaume ni wanyama.

for free revision past papers visit: www.freekcsepastpapers.com

**Maswali**

**a)** Shairi hili lina dhamira gani ? (alama 2)
**b)** Eleza aina ya shairi hili. (alama 2)
**c)** Onyesha jinsi mshairi aliweza kutumia idhini ya kishairi katika utunzi wake. (alama 4)
**d)** Tambua nafsineni katika shairi. Thibitisha. (alama 2)
**e)** Andika ubeti wa sita kwa lugha ya riwaya. (alama 4)
**f)** Taja mambo matatu ya nafsi neni kama ushauri kwa msemewa. (alama 3)
**g)** Kwa kutoa mifano fafanua tamathali tatu alizotumia mshairi. (alama 3)

**SEHEMU B : HADITHI FUPI**
**Ken Walibora na S.A Mohammed : Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine**

**2.** Huku ukirejelea hadithi zozote tano, fafanua jinsi suala la ndoa lilivyoishughulikiwa. (alama20)

**SEHEMU C : RIWAYA**
**Ken Walibora : Kidagaa Kimemwozea**
**Jibu swali la 3 au la 4**

**3.** "Hatuwezi kuwa binadamu endapo hatuwaoni walemavu kama wenzetu. Tutakuwa tumelemaa ulemavu mbaya zaidi kuliko ulemavu."
**a)** Fafanua muktadha wa dondoo hili. (alama4)
**b)** Eleza kwa tafsili ulemavu sita katika riwaya. (alama 12)
**c)** Taja na ueleze maudhui mawili yanayoendelezwa na msemaji katika dondoo hili. (alama 4)

**Au**

**4.** Fafanua nafasi ya elimu katika jamii ya Kidagaa Kimemwozea. (alama 20)

**SEHEMU D : TAMTHILIA**
**Timothy Arege : Mstahiki Meya**
**Jibu swali la 5 au la 6**

**5.** "Sikio la kufa halisikii dawa .......... amebadilika."
**a)** Ni nini muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
**b)** Tamathali gani ya usemi imetumiwa katika dondoo. Thibitisha. (alam 2)
**c)** Yakinisha dondoo hili kwa kumrejelea mhusika mkuu. (alama 14)

**Au**

**6.** Ukoloni mamboleo umekita mizizi katika mataifa machanga ya Afrika. Dhihirisha ukiangazia tamthilia ya Mstahiki Meya. (alama 20)

for free revision past papers visit: www.freekcsepastpapers.com

**SEHEMU E : FASIHI SIMULIZI**
**Jibu swali la 7 au la 8**

**7.** **a)** Eleza maana ya lakabu. (alama 2)
**b)** Sifa za lakabu ni zipi ? (alama 5)
**c)** Kwa nini lakabu ni muhimu katika jamii. (alama 7)
**d)** Jadili manufaa ya utafiti katika Fasihi Simulizi. (alama 6)

**8.** **a)** Eleza kipera cha mawaidha. (alama 2)
**b)** Fafanua sifa tano za mawaidha. (alama 10)
**c)** Mawaidha yana dhima gani katika jamii ? (alama 8

**GITUAMBA LAIKIPIA**

**102/1**
**KISWAHILI**
**INSHA**
**KARATASI YA KWANZA**
**Muhula wa Pili 2017**

1. Umeshtakiwa kwamba unashiriki katika maovu mbalimbali kijijini mwenu. Andika mahojiano kati yako na polisi.
2. Bila sekta ya kilimo, uchumi wa nchi hauwezi kuendelea. Jadili.
3. Andika kisa kinachodhihirisha ukweli wa methali hii:
   Chumia juani kalie kivulini.
4. Umaskini unaendelea kuongezeka nchini Kenya. Eleza chanzo cha umaskini huu kisha upendekeze jinsi tunavyoweza kuukomesha kuendelea hatimaye kufutilia mbali kabisa.

**GITUAMBA LAIKIPIA**
**Karatasi ya 2**
**(Ufahamu, Ufupisho, Matumizi ya Lugha, Isimu Jamii)**
**Julai / Agosti - 2017**
**Kidato Cha 4.**
**UFAHAMU (ALAMA 15)**
**Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali.**

for free revision past papers visit: www.freekcsepastpapers.com

Watu wengine hawawezi kunywa chai au uji bila kutia sukari. Wanatumia sukari kwa hamu na ghamu bila kutambua kuwa hiyo ni sumu wanayojiongezea mwilini.

Ni ukweli usiopingika kuwa wazee wa jadi waliishi muda mrefu wakiwa na siha njema kuliko sisi. Hii ni kwa kuwa waliishi katika kipindi ambacho sukari inayotengenezwa viwandani haikuweko. Iwapo ilikuweko, ilikuwa bidhaa ya wateule waungwana kutengenezea vitu kama keki, mahamri, vitumbua na kadhalika na akina yahe hawangeweza kuigharamia.

Watafiti wa masuala ya afya wamegundua kuwa sukari inayotayarishwa viwandani sasa haina virutubishi vyovyote . Halikadhalika, utaratibu wa viwandani wa kutayarisha sukari ili iwe nyeupe na kuichuja huharibu virutubishi vinavyoweza kuwa muhimu mwilini. Umuhimu wa sukari wakausaza kwa kutia ladha tamu tu. Umuhimu huu hauwezi kulinganishwa na madhara yanayoletwa na sukari hii. Baada ya kusagika mwilini, sukari hii huacha masalio ya asidi mwilini yenye sumu inayoathiri siha.

Matumizi ya sukari kwa wingi husababisha madhara mbalimbali mwilini. Kwanza, huchangia kuoza na kuharibika kwa meno pamoja na matatizo ya meno kuuma. Pili, sukari nyeupe imehusishwa na ongezeko la maradhi ya kisukari, moyo na hipoglisimia au upungufu wa sukari mwilini. Matumizi holela ya sukari huleta kipandauso au ugonjwa wa gahfla wa kuumwa upande mmoja wa kichwa unaoambatana na kichefuchefu, kutapika na matatizo ya kuona. Pia ,sukari huleta maradhi ya ngozi na figo, pamoja na ongezeko la kemikali iitwayo kolestroli, ambayo ni ufuta unaonata na ambao unatokana na kutoyeyuka kwa mafuta yote mwilini. Kemikali hii ya kolestroli inaporundikana moyoni, hufanya mishipa inayotoa damu moyoni na kuisambaza mwilini kuwa myembamba na sugu. Moyo hulazimika kusukuma damu kwa nguvu na huenda moyo ukachoka na kukoma kufanya kazi.

Madhara haya ya sukari ndiyo yanayowafanya watu wengi kukiri kuwa sukari, ingawa ni tamu, ni sumu mwilini. Wataalamu wa lishe wamependekeza ulaji wa vyakula kama nafaka, matunda, mboga na miwa ambavyo vimejaa sukari asilia.

Fauka ya hayo, sukari inayotoka katika asali ni bora zaidi kwa mwili wa mwanadamu.

Asali huwa na sukari asilia,vitamini, madini na amino asidi. Hivi vyote huwa na manufaa mbalimbali mwilini. Mathalani, asali huupa mwili nishati inayohitajika kuendesha shughuli za viungo. Licha ya hayo, asali huuchangamsha mwili. Asali huwa na kemikali ambazo husaida watoto kukua vizuri. Huweza kuzidisha kiwango cha himoglobini, hivyo kupunguza uwezekano wa watoto kuwa na anemia ( upungufu wa damu ) . Halikadhalika, asali husaidia katika usagaji wa chakula iwapo itatumiwa kabla ya mlo. Matumizi ya kijiko kimoja cha asali kila siku husaidia mwili kujikinga dhidi ya magonjwa ya kukohoa. Asali husaidia pia kuondoa harufu mbaya kinywani.

Asali pia inaweza kutumiwa kujipaka. Inapotumiwa kwa njia hii, hutunza ngozi na kuifanya ing'are, huondoa vipele na ugumu wa ngozi ,pamoja na kutibu kule ngozi ilikokatikakatika . Halikadhalika, asali hutibu vidonda. Viwanda vingi vya vipodozi vilevile hutumia asali kama malighafi muhimu katika utengenezaji wa bidhaa hizo.

**MASWALI**

(a) Kutokanana na taarifa hii, kwa nini wazee wa zamani waliishi muda mrefu wakiwa na siha njema kuliko watu wa siku hizi? (alama 1)

(b) Taja matumizi mawili ya sukari nyeupe. (alama 2)

(c) Onyesha madhara matatu ya sukari nyeupe mwilini. (alama 3)

(d) Taja aina ya sukari iliyo na manufaa mwilini mwa mwanadamu au ueleze ni kwa nini. (alama 2)

(e) Eleza manufaa ya asali: (alama 2)
   (i) Ndani ya mwili
   (ii) Nje ya mwili

(f) Eleza maneno yafuatayo kama yalivyotumika katika taarifa: (alama 4)
   (i) Hamu na ghamu:…………………………………………………………
   (ii) Akina yahe:……………………………………………………………
   (iii) Sugu:…………………………………………………………………
   (iv) Vipodozi:……………………………………………………………..

**2. SEHEMU B: UFUPISHO**

Soma taarifa ituatayo kasha ujibu maswali

Kuna mambo kadha ambayo yamejitokeza hivi majuzi yanayonitia wahaka kuhusu kuundwa katiba ya aushi na ya kudumu. Mosi, kuna watu ambao wanachukulia kuwa lazima tuunde katiba itakayolinda maslahi ya wanasiasa walioko sasa. Katika uundaji wa afisi mbalimbali wanafikiria maslahi ya watu wa makabila yao wala si asasi zinazohusika. Fikra hizi ndizo zilizowafanya watu kuandamana mitaani, wakiwahimiza wajumbe kuhakikisha kuwa tuna afisi maalum zilizotengewa watu Fulani. Licha ya heshima tuliyonayo kwa viongozi wetu wa sasa, si sawa kuunda afisi kwa ajili yao. Tuunde afisi kwa sababu zinahitajika kwa maendeleo ya nchi yetu na zinalinda maslahi ya kila mwananchi. Tujitahidi kupunguza imani za kikabila katika kuunda sheria hii kuu. Tuongozwe na fikira za kizalendo, fikira za kujenga taifa moja kupitia lugha ya Kiswahili.

Pili, kuna watu ambao kutokana na shinikizo za mataifa ya nje, wanataka tuwe na katiba itakayolinda haki za wageni kuliko za wananchi. Jambo hili linasikitisha sana. Sheria hii kuu ni mali ya Wakenya na ndio wanapaswa kuiongoza na kufikisha hatima yake. Kama ijulikanavyo na wengi, katiba ni nyenzo ya kuleta maendeleo na kudumisha maelewano baina ya viongozi na wananchi. Ni mkataba baina ya mwananchi mmoja na mwenziwe kuhusu namna watakavyoishi pamoja. Masharti yanayoiongoza serikali ni muhimu yawe kwa manufaa ya mwananchi, hayapaswi kukinzana na haki za mwananchi.

Katiba nyingi za ulimwengu zina kitangulizi kinachoonyesha kwamba katiba ni mali ya taifa na ndiyo sheria kuu nchini. Aidha huonyesha kuwa wananchi wanaafikiana kuwa ndiyo katiba yao na kwamba kuna masharti na maadili ya kimsingi yanayoiongoza. Kwa mfano, ni nchi moja ya kidemokrasia? Ni nchi iliyopunguza na kusambaza madaraka mashinani? Je, inaamini katika heshima, usawa na haki kwa wananchi wote? Kuna imani yoyote kuhusu uraia, wimbo wa taifa, bendera ya taifa na lugha ya taifa?

Kitangulizi cha katiba ni mwongozo wa falsafa ya taifa na kinaashiria maafikiano baina ya wananchi kuhusu falsafa hiyo. Wanasiasa wanaochukua hatamu za uongozi wa serikali wanatarajiwa kufuata imani na maelekezo ya kitangulizi hicho cha katiba.

for free revision past papers visit: www.freekcsepastpapers.com

**MASWALI**

(a) Dondoa mawazo makuu kwa majibu wa aya ya kwanza na ya pili.
(Maneno 80 – 90). (alama 7)
(Mtiririko 1)

(b) Ukirejelea aya za mwisho mbili, eleza umuhimu wa kitangulizi cha katiba.
(Maneno 35 – 40). (alama 6)
(Mtiririko 1)

**MATUMIZI YA LUGHA (alama 40)**

a) Andika kwa usemi halisi
Wanafunzi walishangaa na kutaka kujua kama mwalimu wao angefika siku hiyo. (alama 2)

b) Onyesha matumizi ya kiambishi 'ku' katika sentensi ifuatayo: [alama 2]
Watahiniwa hao hawakusoma maagizo ya mtihani vizuri.

c) Sauti /e/ na /u/ hutamkwa vipi? [alama 2]

d) Kwa kutumia shadda, onyesha maana tofauti za neno walakini. [alama 2]

e) Andika sentensi ifuatayo kwa wingi katika hali ya udogo: [alama 2]
Mwizi aliiba ndoo iliyoachwa njiani na mtoto.

f) Kanusha ukirejelea maagizo kwenye mabano. [alama 2]
   a) Huomba (katika nafsi ya kwanza umoja) ____________________________________________
   b) Huuza (kwa kutumia nafsi ya tatu wingi.) ____________________________________________

g) Tambulisha aina za shamirisho katika sentensi ifuatayo: [alama 2]
Mama aliwapikia watoto chakula kizuri.

h) Bainisha aina za sentensi zifuatazo kwa kuzingatia Kigezo cha dhamira na kigezo cha muundo. Alama 4
a) Endeni nyumbani.
b) Wanafunzi ambao wamefika ni wenye bidii

i) Changanua sentensi ifuatayo kwa michoro ya matawi: alama 4
Mama aalienda sokoni kununua viazi ambavyo vitapikiwa wageni

j) Tunga sentensi kutofautisha maana ya jozi zifuatazo za maneno: alama 2
a) Funda ii) vunda

k) Eleza maana mbili tofauti zinazojitokeza katika sentensi ifuatayo: alama 4
Kapombe anapenda pombe kuliko kakake.

l) Onyesha mizizi katika maneno yafuatayo: alama 2
i) Tulikula ______________
ii) Yaliteketezwa ______________

m) Bainisha kiima na chagizo katika sentensi ifuatayo: alama 2
Mzee Matuko Weye alienda shambani leo asubuhi.

n) Taja aina za virai vinavyopatikana katika sentensi zifuatazo: alama 2
i) Anatembea kwa maringo

o) Eleza matumizi matatu ya kiimbo. Alama 3

p) Ainisha. alama 3
Alimgombeza

q) Taja nomino mbili milikishi. (alama 2)

**Isimujamii** **(alama 10)**

Eleza vianzo vitano vya makosa yanayofanywa na wazungumzaji wa lugha ya Kiswahili.

for free revision past papers visit: www.freekcsepastpapers.com

**GITUAMBA LAIKIPIA**
**102/3**
**KISWAHILI**
**FASIHI**
**KARATASI YA TATU**
**MUDA: SAA 2 ½**

**SEHEMU A: RIWAYA – KIDAGAA KIMEMWOZEA – Ken Walibora (ALAMA 20)**

1. Kwa kurejelea riwaya ya Kidagaa Kimemwozea eleza vile mwadishi amedhihirisha kwamba vijana wanaweza kuchangia pakubwa katika ujenzi wa nchi yao kwa kuleta mabadiliko. (alama 20)

**SEHEMU B: TAMTHILIA**
Timothy Arege: Mstahiki Meya
Jibu swali la 2 au 3

2) "Nanyi vilevile msikate tamaa. Endeleeni kushinikiza kumwona Meya. Mlango hatimaye huenda ukasalimu armi."
   a) Weka dondoo hili haya katika muktadha wake. (alama. 4)
   b) Taja kwa kutoa mifano; tamathali zozote mbili za lugha zilizotumika katika dondoo hili. (alama. 4)
   c) Kwa kurejelea hoja sita, eleza ni kwa nini wanaorejelewa wanakaribia kukata tamaa. (alama 12)

3. Viongozi katika tamthilia ya Mstahiki Meya wanaonyesha kutowajibika kwa hali ya juu. Eleza (alama 20)

**SEHEMU C - HADITHI FUPI – DAMU NYEUSI NA HADITHI NYINGINE -** Ken Walibora na S.A Mohamed.
Jibu swali la 4 au la 5

4. Kwa kurejelea hadithi mbalimbali katika Diwani ya Damu Nyeusi, fafanua matatizo KUMI yanayokumba nchi za bara la Afrika. (alama 20)

5. "..naomba msaada wako…kichwa kinaniwanga na sijui kama shule yenu ina kliniki ambapo naweza kusaidiwa.."
   a) Eleza mkutadha wa dondoo hili. (alama 4)
   b) Eleza sifa nne za mzungumzaji. (alama 8)
   c) "Mzigo wa mwenzio ni kanda la usufi" Fafanua kauli hii ukirejelea hadithi nzima. (alama 12)

for free revision past papers visit: www.freekcsepastpapers.com

**SEHEMU D : USHAIRI**
(alama 20)
Soma shairi hili kisha ujibu maswali yanayofuata.

Nimeyaandika maneno haya
kwa niaba ya,
Mamilioni wasio malazi
Wazungukao barabarani bila mavazi
Wabebao vifurushi vilivyo wazi,
… milki yao ya maisha.

Kwa niaba ya:
Maelfu wanaovuma bila haki
Wiki baada ya wiki
Leo sumu au spaki
Leo kamba au bunduki
Na kwa wale wanasubiri kunyongwa

Kwa niaba ya
Vijana walio mtaani
Wale mayatima na maskini
Wazungukao mapipani
Kila pembe mjini
Kuokota sumu kutia tumboni
Kujua bila kujua
'ili kupata kuishi.

Kwa niaba ya:
Wakongwe wasiojiweza
Walao chakula kilichooza
Wachukuao choo wakijipakaza
Pole pole wakijiangamiza

Katika vyumba vyao
Baridi na giza
Kwa saba hawan watazama
Wala wauguza
Kwa niaba ya:
Waishi na nyingi hofu
Kw sababu ya madawa tifutifu
Yatiwayo vyakulani yakitufanya wafu
Bila ya mtu kuona
Kana kwamba sote to vipofu
Kwa niaba yetu sote:
Tuliofungwa vifunguni, duniani
Tuliosukumwa kingoni, maishani
Tuliopokonywa maoni machoni
Tulioitiwa sumu malishoni
Tuliodidimizwa kinyesini
Ili `maendeleo'
Yaendelee kwenda njiani
Huku yakitema machicha ya roho zetu.

Maswali

a) Hili ni shairi la aina gani? (alama 2)
b) Eleza matatizo yanayokumba wanaorejelewa katika shairi? (alama 6)
c) Eleza maana ya mishata na utambue mfano mmoja katika shairi. (alama 2)
d) Malenga ametumia idhini yake. Jadili kwa mifano miwilli. (alama 4)
e) Kwa kutoa mfano mmoja, eleza mtindo aliotumuia mshairi kuendelea ujumbe wake. (alama 2)
f) Andika ubeti wa kwanza kwa lugha nathari/tutumbi (alama 4)

**7. SEHEMU E: FASIHI SIMULIZI (alama 20)**

a) Eleza matatizo matano yanayoweza kuikabili fasihi simulizi katika jamii. (alama 10)
b) Taja na ueleze wahusika wanne wa fasihi simulizi (alama 4)
c) Tofautisha kati ya ngonjera za ushairi na za maigizo (alama 2)
d) Fafanua vipera vifuatayo vya fasihi simulizi (alama 4)
   (i) ngoma
   (ii) ngomezi

for free revision past papers visit: www.freekcsepastpapers.com

**IMENTI CENTRAL**
**102/1**
**KISWAHILI INSHA**
**KIDATO CHA NNE**
**JULAI/AGOSTI 2017**

1. Kumekuwa na ukosefu wa usalama katika eneo bunge lako . Andika barua kwa mhariri wa gazeti la mwangaza ukipendekeza jinsi ya kuimarisha usalama.

2. Ufisadi umekwamiza juhudi za maendeleo nchini. Jadili.

3. Aendaye kwa mganga hakosi jambo .

4. Andika insha itakayoanza kwa
   Nilipopatazama mabaki ya nyumba yetu macho yaliingia kiwi machozi yakanilengalenga………………….

**IMENTI CENTRAL**
**KISWAHILI**
**KARATASI YA 2**
**LUGHA**
**MUDA SAA: 2 ½**

**1. UFAHAMU**

***Soma kwa makini makala yafuatayo kisha jibu maswali yanayofuatia.***

Kupanda mchongoma, kushuka ndio ngoma, wanafunzi wengi nchini, wakiwemo wanangu bado hawajaripoti shuleni. Wataenda lini? Juhudi za wanafunzi wengi nchini ambazo hufananishwa na za mchwa wajengao vichuguu kutwakuchwa. Huenda zikazama kwenye bahari yenye kina kirefu.

Hii si kwa kupenda kwa wanafunzi hao bali kwa majaliwa ya Mungu anayewapa waja viti na kumbi kila wakai.
Hakuna mja aliyezaliwa na hela mkononi wala umaskini kinywani. Wewe uliyenacho shukuru mungu.
Wapo wanaoamka Wakunywa chai ya mkandaa kwa kiporo baridi cha ugali na wapo wanaoshtaki njaa kwa matobosha sambusa kwa mikate ya mofa kila asubuhi. Wewe ni wa tapo gani? Kupata kwa maskini au mnyonge ni matajiri wanalilia zaidi haki za kutajirika?

Zaidi ya wanafunzi hamsisni wanakabiliana na umaskini ana kwa ana. Wengi wao walihitimu kujiunga na shule za mikoa na wengine za kitaifa lakini ng'o! kuendelea kwao kusoma kumegeuka jinamizi ya kighafla!
Wakuu wa shule kadhaa tulizozitembelea mapema wiki iliyopita, walilimatia kuzungumzia suala hili ambalo ni nyeti kutoka kwa wanafunzi wa jamii fukara nchini.

Wengine walidai kwamba ulipaji karo wa wanafunzi hao pindi waingiapo shuleni huwa kizungumkuti kwao.
Japo mashirika mengine yasiyo ya kiserikali yakiwemo benki na asasi mbai mbali hujitokeza hadharani ba kujitwika mzigo wa gharama zote, mambo huenda tenga tahanani pindi kufuatilia kwa ada kunapoanza.

Hii husababishwa na ithibati nyingine za uongo baina ya jamii watokako wanafunzi hao na uhalisia wa stakabadhi za wanafunzi waathirika zinazowasilishwa baada ya matokeo yao kuwasilishwa kwa wadhamini. Namaanisha stakabadhi bandia.
Hii si kumaanisha kuwa kila mhusika wa kudhaminiwa hawi mkweli, hasha! Njia za kibinafsi na mikato wakati mwingine hukwamiza ndoto za wanafunzi wanaodhamiria kuukwea mlima wa masomo kwa minajili ya kujikimu na kuzifaa familia zao siku za usoni. Wengine huuza mifugo yao kwa minajili ya kujikimu na kuzifaa familia zao siku za usoni. Wengine huuza mifugo yao kwa minajili ya kupata angalau nusu ya karo ya mwaka mzima. Umewahi kuwaona wenzetu kutoka kwa makabila ya kima sai, wapokot, wasamburu na waturkana wakisherehekea kwa nderemo pindi mtoto wao anapohitimu katika chuo kikuu kwa cheti Fulani kama vile, stashahada, shahada, shahada ya uzamili au uzamifu?

Aghalabu hawafichi nguvu ya sala zao. Jiulize mbona jambo hilo si la kawaida sana kutendeka kwa makabila mengine japo wana sherehe zao pia? Tazama jinsi masomo ya wanafunzi watokao sehemu hizo wanavyokumbwa na majanga tele.
Anzia mavazi hadi masomo.. wanafunzi husomea tabu, hula tabu na kumeza tabu lakini siku yao ya mavuno huwaacha wenzao nusu vilio na wengine nusu vicheko. Huimba na kurukaruka kwa furaha ya ndama wanywao maziwa huku machozi ya raha yakiwatoka mbonini.

Kuna wanafunzi wengi wanalilia misaada ya karo na udhamini hasa wale watokao katika jamii maskini. Eti! Wanaisaka ndoto! Mwenye uwezo ajitokeze kufuta machozi yao jamani. Hongera zangu ni kwa mashirika yote yanayojifunga nira kuimarisha na kuitimiza ndoto ya wanafunzi hawa wenye malengo timamu maishani bila kubagua.
Sio tu mashirika pekee bali watu binafsi ambao wanaweza kufadhili yeyote ambao mungu kuwapa uwezo wa kula na kusaza.
Kwa yakini, kutoa ni moyo usambe ni utajiri. Misukosuko yoyote ya kiuchumi nchini huanza na mzalendo mwenyewe.

for free revision past papers visit: www.freekcsepastpapers.com

Umeitendea haki gani nchi yako? Ama wee warudisha maendeleo nyuma? Nafasi uliyoiwania ukitoa ahadi nyingi, umeitumiaje kuwasaidia wanyonge? sidhani hela za CDF zingali zinatumika sawasawa katika kila kaunti nchini. Ukila kwa vijiko na nyuma, wakumbuke walao kwa vidole kwani vijiko hawajaviona kwao tangu kuzaliwa!

**MASWALI.**

a) Ipe anwani habari uliyoisoma. (alama 2)
b) Nini maana ya huenda juhudi za wanafunzi wengi nchini zikazama kwenye bahari yenye kina kirefu. (alama 2)
c) Kuneemeka kwa mkata kwategemea mambo mawili. Yataje (alama 2)
d) Mashirika yanayojitolea kuwafadhili wanafunzi kutoka jamii fukara hukumbwa na changamoto ipi? (alama 2)
e) Kufikia mwisho wa taarifa hii mwandishi anatoa rai gani? (alama 4)
f) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumiwa katika kifungu. (alama 3)
   i) Matobosha -
   ii) Walilimatia -
   iii) Tenge tahanani –

**UFUPISHO**

***Soma makala yafuatayo na ujibu maswali.***

Mojawapo kati ya misingi na nguzo za maendeleo ulimwenguni ni viwanda. Viwanda ni muhimu kwa kuwa ndivyo vinavyoigeuza malghafi yanayopatikana na kuwa bidhaa zinazoweza kutumiwa na watu. Katika nchi zinazaoendelea, ambazo hazina uwezo mkubwa wa mitaji, viwanda vinavyoimarika ni vile vidogo. Hivi ni viwanda ambavyo huhusisha amali za mikono. Kuimarika kwa viwanda hivi vidogo kunatokana na sababu mbalimbali.

Nchi zinazoendelea huwa na masoko finyu hasa kwa kuzingatia uwezo wa ununuzi wa wanaolengwa bidhaa za viwanda. Katika msingi huu, viwanda vikubwa vitawiwa vigumu kufanya biashara katika mazingira ambako masoko yake ni finyu au utashi wa bidhaa zake sio mkubwa. Viwanda vidogo pia vina uwezo wa kuwaajiri wafanyakazi wengi hasa kwa kuwa havina uwezo wa kugharamia mashine. Uajiri huu wa wafanyakazi wengi ni muhimu katika maeneo mengi ambako tatizo la uajiri ni mojawapo wa matatizo sugu. Tofauti na mataifa ya kitasnia, mataifa ya nayoendelea hayana mifumo imara ya kuwakimu watu wasiokuwa na kazi. Utegemezi wa jamaa wanaofanya kazi kwa hivyo unakuwa nyenzo ya pekee ya kuyamudu maisha.

Kuanzisha viwanda vidogo vidogo hauhitji mtaji mkubwa tofauti na viwanda vikubwa. Hali hii inasahilisha uwezekano wa watu wengi kujasurisha shughuli yoyote ile. Sambamba na suala hili ni kuwa ni rahisi kujaribisha bidhaa mpya kwa kiwango kidogo cha kiwanda kidogo. Ikiwa mzalishaji yeyote atazalisha bidhaa mpya kwa mapana, kwa mfano kama ilivyo kwa viwanda vikubwa, pana uwezekano wa kupata hasara kubwa. Huenda utashi wa bidhaa hizo uwe mdogo ukilinganishwa na ugavi wa bidhaa zenyewe.

Majaribio mazuri huwa ni kiwango kidogo. Kuwepo kwa viwanda vidogo huwa ni chocheo kubwa la usambazaji wa viwanda hadi maeneo ya mashambani. Hali hii inahakikishas kuwa nafasi za ajira zimesambazwa nchini hali ambayo inasaidia kuhakikisha kuwa pana mweneo mzuri wa kimapato nchini. Mweneo huu wa mapato unachangia katika kuboresha uwezo wa kiunnuzi wa umma. Huu ni msingi muhimu wa maendeleo.

Upanuzi na uenenaji wa viwanda vidogo vidogo ni msingi mkubwa wa kujitegemea kiuchumi. Aghalabu viwanda vikubwa huegemea kwenye mitaji ya mashariki ya kimataifa na huwa msingi wa kuendelezwa kwa utegemezi wa kiuchumi.
Lich ya faida zake, ueneaji au kutanda kwa viwanda hukabiliwa na matatizo mbalimbali. Tatizo la kwanza linahusiana na mtaji. Lazima pawepo na mbinu za kuweka akiba ili kuwa na mtaji wa kuanzishia biashara. Njia mojawapo ya kufanya hivi ni kwa kutegemea masoko ya mitaji ambayo katika mataifa mengi hayajaendelezwa vyema. Inakuwa vigumu katika hali hii basi kupata pesa kwa uuzaji wa hisia kwenye masoko hayo.

Tatizo jingine linalotokana na ukosefu wa mikopo ya muda mrefu ya kibiashara kwa wenye viwanda vidogo vidogo. Mikopo ya aina hii huwa muhimu hasa pale ambapo anayehusika ana mradi wa kununua vifaa kama mashine. Mikopo ya muda mfupi inayopatikana kwenye mabenki huweza kuwashinda wengi kutokana na viwango vya riba kuwa juu. Haimakiniki kuwa viwanda kama hivi kukopa kutoka nje ya nchi zao. Juhudi za kuendeleza viwanda hivi huweza pia kukwamizwa na tatizo la kawi kama vile umeme. Gharama za umeme huenda ziwe juu sana. Isitoshe, si maeneo yote ambayo yana umeme. Matatizo mengine huhusiana na ukoseu wa maarifa ya kibiashara, ukosefu wa stadi za ujasiriamali au kuwa na ujasiri wa kujiingiza kwenye shughuli fulani na miundo duni.

Ili kuhakikisha kuwa viwanda vimekuzwa na kuendelezwa pana haja yakuchukua hatua kadha. Kwanza, kuwepo na vihamasisho kwa wanaoanzisha viwandda vidogovidogo kama vile punguzo la kodi, kuhimiza kuanzishwa kwa viwanda vidogo vidogo na kusaka kuyapanua masoko kwa ajili ya bidhaa zinazozalishwa na viwanda hivyo. Aidha kuanzishwa na kupanuliwa kwa taasisi za kuendeleza upanuzi huo. Pana haja ya kuwekeza kwenye rasilimali za kibunadamu; kuelimishwa na kupanua uwezo wao wa kuyaeleewa mambo mbalimbali. Miundo msingi haina budi nayo kupanuliwa na kuimarishwa. Upo umuhimu pia wa kuogeza kasima inayotengewa maendeleo na ukuzaji wa viwanda ili kuharakisha maendeleo yake pana umuhimu wa kupambana na ufisadi unaoweza kuwa kikwazo kikubwa. Inahalisi kutambua ikiwa viwanda vitatanda nchini, uchumi wa inchi utawanda.

for free revision past papers visit: www.freekcsepastpapers.com

2. Muhtasari

a) Kwa maneno 65-75, eleza ujumbe muhimu unaopatikana katika aya ya pili hadi ya nne. (alama 8) matayarisho

b) Kwa maneno (50-55) fafanua mambo yanayotinga ukuaji wa viwanda. (alama 5)

**MATUMIZI YA LUGHA**

a) (i) Taja sauti nne za konsonanti ambazo ni za nazali. (alama 2)

(ii) **Andika sentensi ifuatayo katika ukubwa .**

Nyoka huyo alikatwa mkia na mvulna yule. (alama3)

**b) Kanusha**

Nahodha ameendesha merikebu vizuri. (alama 1)

c) Eleza matumizi ya kiambishi “ji” katika tungo hizi. (alama 2)

i) Mtoto amejikata kidole

ii) Yeye ni mchoraji

d) Changanua sentensi hii kwa njia ya mstari. (alama 4)

Wageni waliofika jana wamerejea nyumbani.

e) Akifisha sentensi ifuatayo (alama 3)

Nilimkuta mkuu wa wilaya ya jirani akisoma kitabu kiitwacho utubora mkulima.

f) Tumia eno “haraka” kama. (alama 2)

- Nomino...................................
- Kielezi...................................

g) Andika kinyume cha sentensi hii (alama 2)

Mama alitandaza zulia kubwa sebuleni.

h) Andika katika usemi halisi .

Rais alisema kuwwa wanagepata tiba bure kama bunge lingepitisha mswada. (alama 3)

i) Bainisha matumizi ya ‘po’ katika sentensi hii. (alama 2)

Alipowasili alionyeshwa walip................................................

j) Ainisha

Lililolika. (alama 3)

k) Bainisha shamirisho katika sentensi ifuatayo.

Karwitha alimjengea baba yake nyuba kwa matofali. (alama 3)

l) Andika sentensi hii bila kutumia ‘amba’

Ng’ombe ambaye hupewa chakula kizuri ndiye ambaye hukamuliwa maziwa mengi. (alama 2)

m) Tunga sentensi moja kutofautisha maana mbili za neno ziwa. (alama 2)

n) Andika kwa wingi.

Kuku yuyu huyu ndi ye aliyetaga yai hili. (alama 2)

o) Ziandike sentensi zifuatazo upya ukizingatia maagizo.

Chakula kinachoiva ndicho kinacholiwa. (mazoea) (alama 2)

Timu hii imeshinda. Haikucheza vizuri.(tumia ijapokuwa)

p) Bainisha kishazi huru na kishazi tegemezi katika sentensi ifuatayo.(alama 1)

Gari lililoharibika limerekebishwa.

for free revision past papers visit: www.freekcsepastpapers.com

**ISIMUJAMII**

| | | |
|---|---|---|
| Mimi | : | Haloo............Huyo ni wewe. |
| Wewe | : | Ndiyo.................uko wapi................? |
| Mimi | : | Dukani .................sasa...........ulizipokea zile bidhaa? |
| Wewe | : | La kampuni ya kikwetu bado haija................ |
| Mimi | : | Sina Credit. Nipigie tafadhali. |
| Wewe | : | Sina pia nitatuma sms. |
| Mimi | : | Iwe saa hii eh! |
| Wewe | : | Sawa |
| Mimi | : | Good day. |
| Wewe | : | welcome |

**MASWALI**

a) Tambua sajili ya mazungumzo haya. (alama 2)

b) Taja sifa nne zinazotambulisha sajili ya hapo juu. (alama 4)

c) Toa sababu mbili mbili zinazowafanya wahusika katika mazungumzo haya kutumia mbinu zifuatazo katika mazungumzo yao. (alama 4)

i) Mdokezo

ii) Lugha mseto

**IMENTI CENTRAL**
**102/3**
**KISWAHILI**
**2017**
**KARATASI YA 3**
**FASIHI**

**USHAIRI**

Huyo! Mshike huyo!
Hakuna bunduki wala kifani
Bomu na risasi hata hawazijui
Lakini mno wanashambuliana
Kwa ndimi zilizonolewa kwa makali
Vipande vya matusi silaha zao.

Yu imara mmoja wao
Akirusha kombora la neno zito!
Limtingishe adui wake
Na kumgusa hisia kwa pigo kuu
Pigo linalochoma moyoni kama kichomi
Kuchipuza joto la hasira na kisasi
Katika mapigano yaso na kikomo

Filimbi ya suluhu inapulizwa kuwaamua!
Nani anayekubali suluhu?
Roho zinakataa katakata
Huku ukaidi ukinyemelea na kutawala kote
Mapandikizi ya watu yakipigana
Vita shadidid visivyo ukomo
Vita vya ndimi!

Magharibi sasa
Jua linapungia mkono machweo
Nalo giza likinyemelea kwa kiburi na kasi
Sisikii tena sauti za misonyo
Mate yawatesi yamekauka
Makanwa yao yamelemewa na uchovu
Sasa wameshikana mikono
Ishara ya suluhu.

for free revision past papers visit: www.freekcsepastpapers.com

**MASWALI**

a) Hili ni shairi la aina gani? (alama 1)
b) Eleza dhamira ya mshairi. (alama 1)
c) Eleza kanuni za utunzi alizotumia mshairi. (alama 4)
d) Taja mbinu zozote tatu za kifasihi alizotumia mshairi. (alama 3)
e) Jadili toni ya mshairi katika beti tatu za awali. (alama 2)
f) Tambua matumizi ya mistari mishata na utoe mifano miwili. (alama 3)
g) Andika mishororo ya kwanza mitatu katika ubeti wa nne kwa lugha nathari. (alama 3)
h) Toa maana ya msamiati huu. (alama 2)
  a) Kombora
  b) Misonyo.

**SEHEMU YA B: TAMTHILIA MSTAHIKI MEYA**

"Dhiki mbali zimekuwapo lakini heri nusu shari kuliko shari kamili".

a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
b) Taja tamathali ya usemi iliyotumika katika dondoo hili. (alama 2)
c) Eleza sifa zozote tato za mzungumzaji. (alama 3)
d) Fafanua aina zozote nne za migogoro inayojitokeza katika tamthilia ya Mstahiki Meya. (alama 8)

**au**

3. kwa kutoa mifano kumi eleza vizingiti walivyokumbana navyo wanacheneo wakati wakupigania mageuzi. (alama 20)

**SEHEMU YA C: RIWAYA KIDAGAA KIMEMWOZEA**.

4. Haki nakwambia..............................afadhali mkoloni mzungu kuliko mkoloni mweusi.
   a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
   b) Eleza sifa za msemaji (alama 6)
   c) Thibitisha ukweli wa kauli hii. (alama 10)

au

5. Eleza namna mbinu zifuatazo zilivyotumwa na mwandishi wa Riwaya Kidagaa kimemwozea kufanikisha maudhui.
   a) Sadfa
   b) Taharuki
   c) Barua
   d) Jazanda
   e) Kisegere nyuma

**SEHEMU YA D: HADITHI FUPI**

6. Hapa huingii bila kuninyooshea mkono.
   a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
   b) Taja na ueleze mbinu ya lugha iliyotumika. (alama 2)
   c) Eleza sifa zozote nne za msemewa. (alama 8)
   d) Fafanua mtazamo wa msemewa kuhusu maisha. (alama6)

**SEHEMU YA E: FASIHI SIMULIZI.**

7
   a) Eleza maana ya miviga. (alama2)
   b) Bainisha dhima ya miviga katika jamii. (alama 8)
   c) Eleza maana ya maghani (alama 2)
   d) Eleza sifa za maghani. (alama 4)
   e) Eleza aina zifuatazo za maghani. (alama 4)
      i) vivugo
      ii) Tondozi

for free revision past papers visit: www.freekcsepastpapers.com

**MURUKA KANDARA**
**102/1**
**KISWAHILI**
**KARATASI YA 1**
**INSHA**
**JULAI 2017**

1. Wewe ni katibu wa kamati ya maendeleo wilayani mwenu. Andika barua kwa Gavana wa Kaunti yenu mkimpendekezea miradi ya maendeleo ambayo mngetaka aishughulikie katika wilaya yenu.

2. Tetea kauli kuwa Dunia ni kijiji tandawazi.

3. Afadhali kujikwaa kidole kuliko ulimi.

4. Andika insha itakayomalizikia hivi:-
………………… Jioni hiyo chajio kilinishinda, nikawazia hotuba ya Waziri wa Usalama kuhusu visa vya kudorora kwa usalama na mauaji yaliyokithiri.

**MURUKA KANDARA**
**102/2**
**KISWAHILI**
**Karatasi ya 2**
**(LUGHA)**
**Julai/ 2017**

**1. <u>UFAHAMU (ALAMA 15)</u> Kangundo**
***Soma taarifa ifuatayo. Kisha ujibu maswali yanayofuata.***

for free revision past papers visit: www.freekcsepastpapers.com

Kwa kipindi cha miezi kadha iliyopita tumeshuhudia vyombo vya dola vikitia makali yake kwenye upekuzi na hata kupiga doria usiku na mchana katika jitihada za kulinda nchi.

Mpango huu ni kweli umeonekana kufanya kazi hivi kwamba hata magaidi wenyewe wameshindwa kupenya katika miji na sasa kuhiari kijinga kushambulia magari ya abiria kitendo ambacho ni cha kuonyesha uwoga. Kwa hatua hiyo, navipa <u>vyombo vya dola</u> kongole. Jambo ambalo lafaa kujulikana ni kwamba mikakati ya kulinda nchi haifai kuwa ni ya wakati mmoja tu, mbali inafaa kuwa ni zoezi la kila siku.

Magaidi nao huwa macho huku yakijua bayana kwamba wakati wa kulala kwa walinzi unapokuwepo, basi wanapata nafasi ya kututupia 'viazi' ukipenda grunedi.

Kama ilivyo kawaida katika mataifa mengi barani Afrika, ni bayana kwamba bado kungali na mianya mingi ambayo magaidi wa kimataifa huendelea kutumia. Dosari bado zipo. Kwa mfano mipaka mingi ya nchi hizi huwa kama lango kuu la ugaidi wa kimataifa, kwani kuenea kwa saratani ya ufisadi halimo tu maofisini mbali pia kwenye mipaka yetu.

Kama kupata kitambulisho, pasipoti na stakabadhi zingine za kusafiri nchini Kenya ashakum si matusi ziligeuzwa 'maandazi' ya kariakoo basi niambie ni nani hawezi kuingia na kutoka nchini bila usumbufu wowote ule bora tu anayehitaji ana hela mkononi? Kwa kuikubali hongo kuwa ufunguo wa kila kitu, Wakenya wenzangu hapo naona ni kama tumejiweka kwenye kikaango kilicho juu ya moto mkali. Hapa hakuna aliye na bahati, tajiri kwa masikini wamo kwenye mtego huu hatari.

Kwa mtindo ambao tunafuata wa kutoa ajira katika idara mbalimbali za ulinzi, inabidi serikali iwe na uangalifu sana hasa kwenye suala nzima la kuhakikisha stakabadhi wanazohitaji si ghushi.

Pasina kufanya hivyo hapo tena tunaweza kuwapata maadui wanaopenya na kujifanya walinzi wetu kumbe ni majasusi wa magaidi. Kila Mkenya anafaa kujihisi kulindwa. Miji, vijiji na hata vitongoji vinafaa kuwa na usalama wa kutosha, kwani kila Mkenya ni mlipa ushuru na hatufai kuona labda tabaka la juu likipendelewa huku mitaa ya mabanda ikiachiwa mbwa koko kama walinzi wao.

Suala lingine muhimu ni kuangaziwa upya usalama kwenye magari ya usafiri.
Juzi tulishuhudia mabasi mawili yakilipuliwa kwenye barabara ya Thika huku tukijua fika kwamba, mpango walinda nchi ungalipo.

La kusitikitisha ni kuona kwamba, madereva na utingo wao walikamatwa na kufunguliwa mashtaka kwa kutozuia shambulizo hilo. Je, hii ni sheria gani? Dereva ataendesha gari au atachukua jukumu la walinda usalama?

Waswahili walinena kwamba mkubwa ni jaa na kwa hivyo Rais wa taifa ndiye anayefaa kubeba mzigo mzima wa usalama wetu bila kubananga wasaa. Wengine ambao wanafaa kuwajibika ni wakuu wote wa idara mbalimbali za usalama. Usalama wako na wangu ni muhimu, elewa bayana kwamba bila usalama watalii hawawezi kuja kututembelea. Bila ya usalama maendeleo ya taifa kamwe hayawezi kupatikana, ndiposa kila jitihada sharti zifanywe ili wote waweze kuendelea kuyafurahia matunda ya uhuru wetu.

Ada ya mja kunena muungwana ni vitendo, hatufai tu kuimba wimbo wa Linda nchi, ilhali mabasi barabarani hayana usalama. Hebu na tuuone ulinzi endelevu na hapo tutawakomoa magaidi kwa yakini.

***Maswali***

1. Ipe taarifa hii anwani mwafaka. ( alama 1 )
2. Kwa nini magaidi wanashambulia magari ya abiria? ( alama 2 )
3. Eleza njia tatu ambazo zinatumiwa na magaidi kutekeleza unyama wao. ( alama 3 )
4. Ni njia gani ambazo magadii hutumia kuingia nchi wanazoazimia kutekeleza uhalifu? (alama2)
5. Kwa nini suala la usalama kwenye magari ya usairi ni muhimu? (alama 1 )
6. Ni njia zipi zinazoweza kutumiwa kupunguza mashambulizi ya kigaidi kulingana na mwandishi? ( alama 2 )
7. Eleza athari za utovu wa usalama. (alama 2 )
8. Eleza neno au mafungu ya maneno kama yalivyotumiwa katika kifungu. (alama 2 )
   (a) Vyombo vya dola
   (b) Jaa

**UFUPISHO (ALAMA 15)**

Sma kifungu kifauatacho kisha ujibu maswali.

Mifuko ni muhimu sana katika maisha ya binadamu ya kila siku. Baadhi ya mifuko huundwa kwa namna ambayo inadumu na inaweza kutumiwa mara kadha wa kadha. Hii huweza kuhifadhiwa na kutumiwa kwa kipindi kirefu. Asilimia kubwa ya mifuko ya aina hii hutengenezwa kutokana na nguo au ngozi. Hata hivyo, ipo mifuko mingine ambayo si ya uashi, haidumu. Hii ni mifuko myepesi, rahisi kubebeka na inayopatikana kwa wingi sana. Hii ni mifuko ya plastiki.

Mifuko ya plastiki hupatikana katika maeneo mengi sana. Mifuko hii sio ghali inapolinganishwa na ile ya nguo au ya ngozi. Hii ni ya gharama ya chni na hupendwa kutokana na wepesi wake. Hata hivyo, mifuko hii inaweza kuwa chanzo cha matatizo mengi. Matatizo haya hutokana na linalopasa kufanywa kuhusu mifuko hii baada ya kutumiwa kwake. Mifuko ya nguo ambayo inatupwa kwenye jalala huishia kuoza na kuwa sehemu ya uchafu wa jalala hilo. Kwa upande wake, mifuko huo. Hata inapofukiwa arthini haiwezi kuoza hata kama kufukiwa huko ni kwa miaka mingi. Aidha hata pale inapochomwa, haiwezi kuteketea hadi kuwa jivu kama ilivyomifuko ya karatasi.

Upo umuhimu mkubwa wa kuwepo kwa sera madhaubuti za kupambana na tatizo la mifuko hii. lazima zitungwe sheria ambazo zinakabiliana na uchafuzi wa mazingira kwa njia hii. kwa njia hii hatari zianzowakabili watu na wanyama zitapunguzwa kwa kiasi kikubwa. Kwa hakika njia mojawapo ambayo ingeweza kutumiwa ni kuharamisha matumizi ya mifuko hii katika upakiaji. Sheria zinaweza kupitishwa ambazo zinahimiza matumizi ya mifuko mbadala kama ile ya karatasi kubebea vitu vidogo Fauka ya hayo, pana haja ya kuwazia kuwepo kwa njia nzuri kuteketezea mifuko hiyo. Inawezekana kuhimiza watumiaji kurejesha mifuko hiyo mahali Fulani kwa ajili ya uteketezaji huo. Hata hivyo, hali hii huenda ikawa ngumu kwa kuwa mahitaji nidhamu ya hali ya juu sana kwa upand ewa watumiaji.

for free revision past papers visit: www.freekcsepastpapers.com

(a) Fupisha ujumbe wa aya tatu za mwanzo kwa maneno 105 – 110. (alama 10, 1 utiririko)
(b) Eleza mawazo makuu yanayojitokeza kaitka aya ya mwisho (maneno 50 – 55) (alama 5, 1 utiririko)

**MATUMIZI YA LUGHA (ALAMA 40)**

(a) Tunga sentensi kubainisha muundo ufuatao. (alama 2)
KN(W+V)+KT(T+E)
(b) Sauti /ch/ ina sifa zipi? (alama 2)
(c) Andika kwa ukubwa wingi. (alama 2)
Mwizi aliiba nguo na kiti
(d) (i) Tofautisha shamirisho kipozi na shamirisho kitondo. (alama 1)
(ii) Onyesha shamirisho kipozi na kitondo katika sentensi moja. (alama 2)
(e) Andika upya sentensi zifuatazo kwa kuzingatia kauli zilizomo mabanoni. (alama 2)
(i) Watoto wenyewe wamekunywa maziwa yao yote. (tendwa)
(ii) Pombe haramu inawafisha Wakenya wengi. (Badilisha kitenzi kiwe nomino) maranda
(f) Tunga sentensi ukitumia kielezi cha jinsi cha nomino ifuatayo.
Uganda. ( alama 1 )
(g) Tambua aina za vitenzi katika sentensi zifuatazo: (alama 3 )
(i) Mjomba alikuwa uwanjani.
(ii) Mjukuu wake ataweza kulima.
(h)) Taja aina ya kirai kilichopigwa mstari katika sentensi ifuatayo.
Walimu wa Kiswahili watawasili leo. (alama.1)

(i) Kanusha
Wanafunzi watundu waliadhibiwa na kuaibishwa. (alama 2)

(j) Nyambua vitenzi vituatavyo katika kauli ulizopewa. (alama 2)
(a) Oa ..............................................(tendesha)
(b) Kokoa......................................... (tendata)

(k) Tunga sentensi mojamoja kubainisha: (alama 2)
(i) Kiwakilishi cha pekee chenye maana ya umilikaji.
(ii) Kiwakilishi cha nafsi kiambata.

(l) Andika kinyume; (alama 2)
Shangazi angeingia tungemsifu.

(m) Tunga sentensi mojamoja kudhihirisha matumizi ya (alama 2)
(a) “ka” ya mfululizo
(b) “a” isiyodhihirika

(n) Changanua sentensi ifuatayo kwa kutumia visanduku:
Rosamaria alipata kitabu chake kipya kilichopotea jana. (alama 4)

(o) Tambua na uainishe viwakilishi katika sentensi ifuatayo: Aliniitisha zawadi uliyokuwa umenituma nimpelekee Hadija. (alama 2)

(p) (i) Kishazi ni nini? (Alama 1)
(ii) Tunga sentensi iliyo na kishazi (alama 1)

(q) Tumia ‘o’ rejeshi tamati kuunganisha sentensi zifuatazo
(i) Jino linauma
(ii) Jino limeng’olewa (alama2)

(r) Tambua vivumishi na uonyesha ni vya aina gani .
Wanafunzi wawa hawa waliochelewa watafanya kazi ya sulubu kama adhabu. (alama3)

4. **<u>ISIMU JAMII (ALAMA 10)</u>**

*Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali*

USAJILI WA WATAHINI

Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia imewaagiza walimu wakuu wa shule za msingi na sekondari wabandike hadharani orodha ya watahiniwa wote waliosajiliwa ili kuwawezesha wazazi na walimu kuthibitisha maelezo yote ya usajili.

Kwenye taarifa aliyoitoa kwa vyombo vya habari, Waziri Dkt Matiang’i alitoa wito kwa wazazi na wanafunzi watakaofanya mitihani ya kitaifa mwaka huu wa 2017 wahakikishe kuwa watahiniwa wamesajiliwa vilivyo. Aliwataka wathibitishe usajili wao katika tarakilishi na kutia saini nakala hizo kama inavyohitajika.

(a) Tambua sajili ya makala haya. (alama 2)
(b) Eleza sifa nane za kimsingi za sajili hii. (alama 8)

for free revision past papers visit: www.freekcsepastpapers.com

**MURUKA KANDARA**
**102/3**
**KISWAHILI**
**Karatasi ya 3**
**FASIHI**
**JULAI 2017**

**SEHEMU YA A**: **Kidaaga Kimemwozea: Ken Walibora**

1. LAZIMA
“……. Kidagaa kimetuozea kwa kutamaushwa na usaliti wa viongozi wa baada ya uhuru.”
(a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
(b) Taja na ufafanue sifa **nne** za viongozi wanaorejelewa. (alama 8)
(c) Kwa kurejelea riwaya hii, eleza ni kwa njia gani viongozi wamedhihirishwa kama wasaliti. (alama 8)

**SEHEMU YA B: Damu Nyeusi na Hadithi Nzingine**

2. “Nashangaa vile kwetu tunavyoabudu watu hao wasiojali.”
(a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
(b) Fafanua hulka za msemewa. (alama 4
(c) Jadili ukweli wa kauli hii. (alama 10)

3. Diwani ya Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine imesheheni uozo wa kijamii unaolemea nchi zinazoendelea. Jadili. (alama 20)

**SEHEMU YA C: TAMTHILIA**
**MSTAHIKI MEYA: TIMOTHY AREGE**

4. Huku ukiirejelea tamthilia ya Mstahiki Meya thibitisha kauli kuwa tamthilia hii ni taswira kamili ya matatizo yanayokumba mataifa mengi barani Afrika. (alama 20)
Au
5. “Sina pingamizi maana hii ni grand idea”
(a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
(b) ‘Grand idea’ Inayozungumziwa ni gani? (alama 2)
(c) Ni Maudhui gani yanajitokeza katika ‘grand idea’. (alama 2)
(d) Taja mbinu ya lugha inayojitokeza katika muktadha wa dondoo hili (alama 2)
(e) Fafanua sifa zozote **tatu** za msemaji. (alama 6)
(f) “Uongozi mbaya umesababisha dhiki kwa wanacheneo”. Fafanua dhiki **nne** (alama 4)

**SEHEMU YA D: USHAIRI**

**6. Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.**

Sahiba umenisema, kwa mchana na laili,
Munaondoa lazima, muenendo wa kiasili,
Kujenga ulipohamaa, mtu huaje aili,
Kupewa usikubali, wajataka usipewe.

Wajataka usipewe, kupewa usikubali,
Haiwi mtu mwanawe, na pia usimjali,
Ulikataa mwenyewe, kwa ghadhabu na ukali,
Kupewa usikubali, wajataka usipewe.

Wajataka usipewe, kupewa usikubali,
Ndipo wewe ushukiwe, ukajifanya mkali,
Na sitaki uambiwe, mtu asije kwa hili,
Kupewa usikubali, wajataka usipewe.

Wajataka usipewe, kupewa usikubali,
Kwani ulihama, kuhgura hapo mahali,
Enenda sinisumbuwe, siniudhi yangu hali,
Kupewa usikubali, wajataka usipewe.

Wajataka usipewe, kupewa usukubali,
Na hili ujuwe, kwangu hili ni jamali,
Siachi ninga kwa mwewe, wala siwezi badili,
Kupewa usikubali, wajataka usipewe.

for free revision past papers visit: www.freekcsepastpapers.com

Wajataka usipewe, kupewa usikubali,
Na hapa ndiyo mwishowe, tamati shairi hili,
Kaa usinizuzuwe, nasubiri filihali
Kupewa usikubali, wajataka usipewe.

Na; Said Karama

***Maswali***

(a) Andika kichwa mwafaka cha shairi hili. (alama 2 )
(b) Mwandishi anadhamiria nini katika shairi hili. (alama 4 )
(c ) Hili ni shairi la aina gani? Eleza. (alama 4 )
(d) Ni methali gani inayoafiki maelezo katika ubeti wa kwanza. ( alama 2 )
(e) Ni nini maana ya kifungu "kupewa usikubali, wajataka usipewe." (alama 2 )
(f) Andika ubeti wa mwisho katika lugha ya nathari. (alama 4 )
(g) Bianisha maana ya msamiati ufuatao kama ulivyotumiwa katika shairi. (alama 2 )
(i) Sahiba
(ii) Liali

**SEHEMU YA E: FASIHI SIMULIZI**

7. a) Tofautisha na ulinganihse mighani na maghani (alama 4)
b) Huku ukitolea mifano ya kipera husika, fafanua dhima nne za maghani. (alama 8)
c) Ukifuata utaratibu unaokubalika, onyesha hatua sita za uwasilishaji wa vitendawili. (alama 6)

for free revision past papers visit: www.freekcsepastpapers.com

**MURANGA SOUTH A**
**102/1**
**KISWAHILI**
**KARATASI 1 (INSHA)**
**JULAI 2017**

**INSHA**

1. Wewe kama mtaalamu wa afya umetambua kuzuka kwa ugonjwa wa kipindupindu wilayani mwenu. Andika barua pepe kwa waziri wa afya huku ukipendekeza hatua za kukabilianana tatizo hili.
2. Pendekeza hatua zinazofaa kuchukuliwa na serikali ili kutatua utovu wa nidhamu miongoni mwa wanafunzi wa shule za upili.
3. Ukiona vyaelea vimeundwa.
4. Andika insha inayoanza kwa maneno haya: sasa ilikuwa patashika, kila mtu akiabiri gari la miguu niponye……..

**MURANGA SOUTH A**
**102/2**
**KISWAHILI**
**KARATASI 2 (MATUMIZI YA LUGHA)**
**KIDATO CHA NNE**
**JULAI 2017**

**UFAHAMU**

Kwa muda mrefu sasa, kumekuwepo na juhudi za kimakusudi na kuchukuliwa kwa hatua za dharura barani Afrika kuzitetea lugha za kiasili.

Dharura hii imechangiwa na athari za ukoloni katika bara hili ambazo zilipalilia upendeleo wa lugha za watawala wa kikoloni waliobagua mila na tamaduni za mwafrika. Katika enzi ya ukoloni, lugha za kigeni zilishamiri katika mianda rasmi kama vile elimu na mawasiliano.

Lugha za kiasili hazikupewa umuhimu- na ikiwa zilipewa umuhimu huo, ulikuwa ni kwa manufaa ya wakoloni. Kuna wataalamu waliotambua mapema kwamba'titi la mama litamu hata likiwa la mbwa'.

Miongoni mwa wataalamu hao ni pamoja na Shabaan bin Robert, Ngugi wa Thiong'o, Grace Ogot, Wole Soyinka miongoni mwa wengine.jitihada za hawa hazikuwahi kupata mafanikio ya kupigia mfano kwa sababu ya upinzani mkali uliotokana na sera baguzi za serikali za mataifa ya Afrika kuhusu uratibu wa masuala ya lugha- hasa lugha zilizofaa kutumika katika kufundishia.

Isitoshe, Waafrika wengi bado wana mielekeo hasi kuhusu lugha zao- kiasi kwamba zinadunishwa na kupuuzwa. Tulipoingia katika karne ya 21, kulitokea mwamko mpya wa kuzitetea lugha za kiafrika.

Makongamano kadha wa kadha yalianza kuandaliwa kumulik ana kuangazia upya nafasi ya lugha za kiafrika katika ramani na masuala ya kiulimwengu.

Mfano wa makongamano hayo ni lile lililoandaliwa Amsara, mji mkuu wa Eritrea mnamo januari 17,200. Mada kuu katika kikao hicho ililenga kupigania lugha za kiafrika dhidi ya pingamizi zote.

Nchini Kenya, chama cha Kiswahili cha taifa(CHAKITA) kimekuwa kikiandaa makongamano kuhusu lugha za fasihi tangu 1998.

Makongamano haya ambayo huwaleta pamoja wataalamu wa lugha na fasihi kutoka Afrika ya mashariki na kati na vyuo vya kigeni yamekuwa ulingo mwafaka wa kuangazia mikondo ya kiafrika karne hii. Je, lugha za kiafrika zitahimili mabadiliko ya kasi yanayojiri katika nyanja za sayansi na teknolojia? Katika utangulizi wa riwaya ya **Shetani msalabani,** NgugiwaThiong'o anauliza:" Tusipozistawisha lugha zetu za kiafrika sisi wenyewe, ni mgeni gani atakayejitokeza kuja kuzistawisha?

Jambo la kusikitisha na kuhuzunisha ni kuwa, watoto wetu wanaoelimishwa kwa taabu ili wawe na elimu ya kustawisha uchumi wa nchi, historia, siasa,sayansi, wao huja wakaandika juu ya taaluma hizo kwa lugha za kigeni.

Walikuwa wakifundishwa kwa manufaa ya kigeni?" Ngugi anaendelea kusema kuwa, kusahau lugha zetu na kuzirukia zile za kigeni ni sawa sawa na kumkebehi Mungu.

Anapendekeza kwamba mkenya (mwafrika) yeyote popote alipo yambidi ajimudu katika lugha mbili; lugha ya kabila lake na Kiswahili. Kwa kuwa lugha husheheni utamaduni wa kundi Fulani la watu, Ngugi anadai kwamba watu wasio na lugha zao ni watumwa- na kwamba hawawezi kamwe kufahamu mafunzo yanayohusu utamduni wao. Sina budi kupongeza watu binafsi na asasi zinazopigania lugha za kiafrika.

for free revision past papers visit: www.freekcsepastpapers.com

**UFAHAMU(alama 15)**

Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali

1. Ipe taarifa uliyosoma anwani mwafaka (al. 2)
2. Ni kwa nini kumekuwepo na juhudi za kimakusudi kuzitetea lugha za kiasili? (al.2)
3. Eleza sababu zilizofanya lugha za kiasili kutoshamiri katika enzi ya ukoloni (al.2)
4. Mwandishi anamaana gani anaposema 'titi la mama li tamu hata likiwa la mbwa? (al.1)
5. Kwa nini juhudi za wataalam wa kiafrika hazikupata mafanikio kuhusiana na lugha za kiasili? (al.2)
6. Ni mwamko mpya wa aina gani uliotokea tulipoingia karne ya ishirini na moja na ulihusu nini? (al.2)
7. Watu wasio na lugha zao ni watumwa. Fafanua (al.2)
8. Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yaliyotumiwa katika makala
   i) Dharura
   ii) Ulingo (al.2)

**UFUPISHO**

**Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali**

Mtihani huzua changamoto kwa yeyote anayepania kuufanya. nakisia ni kwa sababu ya ushindani unaohushishwa nao, hasa nchini mwetu. Aghalabu humfanya anayehusika kuingiwa na wasiwasi ambao hudumaza uwezekano wake wa kufuzu anavyoazimia. Huanza kukata tama kwa kuhisi hawezi kuumudu mrundiko wa kazi anayopaswa kuidurusu kabla ya mtihani huo kuwadia. Wengine hizidiwa na dhana ya uchechefu. Hii ni dhana ambapo mtu huziona nafasi za kushindaniwa kuwa chache mno hivi kwamba hata akijitahidi hawezi kuwa miongoni mwa washindi. Kwa msingi huu hukata tama na kufanya maandalizi yake bila madhumuni maalum. Hivi ndivyo wengi wenye fursa aali za kuupasi mtihani wanavyopoteza nafasi zao.

Hata ya awali zaidi ya maandalizi kabambe kwa mtihani ni kuutambua uwezo wako. Ukisha,jiaminishe kwamba nawe una nafasi maalum ya kuibadilisha jamii yako na kuifanya ifae zaidi. Vigezo vilivyowekwa na jamii ambavyo vimegeuka kuwa vikwazo visikuhadae ukaanza kujionea imani. Linalokupasa kufanya ni kujionea imani. Linalokupasa kufanya ni kujitolea kikamilifu; yaani usisaze hatua itakayokuwezesha kuupita mtihani kasha ukaijutia baadaye.

Nina hakika kwamba kila mwanafunzi, mtahiniwa huwa na lengo la kujishughulisha na elimu yake. Hata hivyo, ni wachache wanaoyahusisha malengo yao na hatua zao za kila siku. Wengi hukosa au kushindwa kuibuka na mikakati ya kuigeuza ndoto zao na malengo yao kuwa matokeo halisi. Unapojiandaa kuwa mtihani wako, ni muhimu kuibuka na mikakati ya kuitimiza ndoto yako.

Katika mkakati wako, jambo moja ni la msingi; kuutambua uwezo na udhaifu wako. Ikiwa utaweza kuukiri udhaifu wako sawa na uwezo wako, una uwezekano mkubwa wa kufanya vizuri. Nakili masomo unayoyamudu nay ale usiyoyamudu. Katika masomo unayoyamudu, orodhesha faslu usizizoielewa  kikamilfu ili kujua kina cha msaada utakaouhitaji ili kuzimudu. Una mwao kuhusu faslu fulani hata katika masomo yanayokulemea, ziorodheshe vilevile.

FASLU

Ukisha kuorodhesha faslu zitakazokuzuia na alama bora zaidi katika masomo unayoyamudu, tafuta msaada wa wenzio kuhusiana na vipengele hivyo. Ikiwa vipo vipengele ambavyo wenzio vilevile hawavielewi, tafuta msaada wa mwalimu/walimu wa somo hilo. Hatua hii itakuhakikishia alama bora zaidi katika somo hilo ili kuimarisha alama yako ya jumla. Aidha, itakuwezesha kuimarisha uwezekano wako wa kusomea taaluma uitakayo kwa kujipa nafasi bora ya kupata alama faafu katika masomo manne ya kimsingi ya taalamu hiyo.

Kuzamia faslu unazozielewa kiasi katika masomo usiyoyamudu kutakupa ujasiri wa kuupita mtihani kwa jumla. Hivi ni kwa sababu kila unapokuwa na atiati kuhusiana na udhaifu wako, hata unayoyamudu hutoweka. Ndiposa ni muhimu zaidi mwanafunzi kukuza ujasiri wake wa kukabili mtihani licha ya maandalizi mengine. Jihakikishie kuibuka na alama isiyokuaibisha katika somo unalolihofia.

Ugawe muda wako kihalisia. Tenga muda mfupi wa kijimarisha zaidi katika masomo unayoyamudu. Orodhesha mada ndogo mahsusi za kuangazia na kwa kipindi bainifu ulichokitenga. Ukishazisoma, jitathmini ili ujifahamishe kuhusu ukubwa wa hatua uliyoipiga.

Tengea vipengele vinavyokutatiza muda zaidi na mwafaka ili kuimarisha uwezo wako kwavyo. Tafuta msaada zaidi katika vipengele hivi. Kuzudi kuvisoma mwenyewe bila msaada wa mwalumu  kutakupotezea muda. Mwalimu wako anajua mbinu itakayokufaa zaidi ili kuyaweka masuala haya kwenye kumbukumbu yako.suala ambalo lingekuhitaji saa mbili kuielewa laweza kuelewa kwa dakika kumi msaada wa mwalimu ukiwapo. Usipoteze muda wako!

Hatimaye, amini kwamba una nafasi muhimu ya kuubadilisha ulimwengu. Si lazima uwe rais, katibu wa kudumu, mhandishi, mwanasheria, mwalimu ilikutoa mchango wako. Taaluma zipo nyingi wala hakuna iliyo dhalili ukiilinganisha na nyingine. Nina hakika kwamba zipo nyingine zitakazobuniwa kadri mazongira na mahitaji ya binadamu yanavyobadilika na kuibua changamoto mpya. Huenda inayotazamiwa kubuniwa itakuhusisha, nawe upo mbioni kukata tama. Usitazame mwingine yeyote na kujihisi dhalili mbele yake. Muulize Muumba wako azma yake ya kukuumba na punde ujuapo, jizatiti kuitimiza.

for free revision past papers visit: www.freekcsepastpapers.com

**UFUPISHO(alama 15)**
**Maswali**

a) Ukitumia maneno kati ya 60-70, fupisha aya tatu za kwanza.
b) Eleza mikakati itakayomwezesha mtahiniwa kufaulu katika mtihani kulingan na taarifa uliyosoma. Maneno(65-70)

**MATUMIZI YA LUGHA (alama 40)**

a) Eleza maana ya kiimbo (al.2)
b) Jaza nafasi zilizoachwa wazi (al. 2)

| Sauti | ala | aina |
|---|---|---|
| ------- | ----------- | kitambaza |
| Gh | ----------- | ------------- |

c) Tumia kivumishi cha kusisitiza katika ngeli ya YA –YA kuandika sentensi (al.2)
d) Andika upya vitenzi vifuatavyo katika kauli zilizo kwenye mabano. (al.2)
   i) Nywa (tendesha)
   ii) La (tendeana)
e) Andika sentensi hii katika ukubwa (al.2)
   Huyu nyoka amekatwa mkia na mvulana Yule.
f) Tambua aina za nomino katika sentensi hii .
   Familia hii hujipaka marashi kila asubuhi (al.2)
g) Tumia'O' rejeshi katika sentensi ifuatayo:
   Mwanafunzi ambaye hufanikiwa ni Yule ambaye husoma kwa bidii (al. 2)
h) Tambulisha aina za shamirisho katika sentensi ifuatayo:
   Mwanafunzi alimsomea mwalimu kitabu (al. 2)
i) Changanua sentensi hii kwa kutumia jedwali (al. 4)
   Wananchi hawa ni wazalendo
j) Taja sifa mbili za sentensi ambatano. (al. 2)
k) Kanusha sentensi ifuatayo (al.2)
   Utingo amefungua mlango wa basi
l) Tumia'amekuwa' katika sentensi kama (al. 4)
   i) Kitenzi kisaidizi
   ii) Kitenzi kishirikishi
m) Andika sentensi hii katika msemo wa taarifa (al.2)
   "Ni jambo la busara kuwasaidia wazazi" mwalimu alituambia
n) Weka shadda panapofaa katika neno walakini (al.1)
o) Eleza matumizi ya na katika sentensi hii (al.2)
   Juma na Rehema wanaadhibiwa kwa sababu waliandikiana barua
p) Bainishi aina za virai katika sentensi hii. (al.3)
   Msichana wake mwerevu ameingia darasani upesi
q) Takinisha sentensi hii (al.2)
   Asipokuja kesho asubuhi sitamlipa deni yake.
r) Unda nomino mbili kutokana na neno'okoa' (al. 2)
s) Geuza katika hali ya kinyume; (al. 3)
   Babu aliinuka na akasimama nje ya nyumba.

for free revision past papers visit: www.freekcsepastpapers.com

**ISIMU JAMII (ALAMA 10)**

a) Eleza maana ya dhaana zufuatazo. (al. 4)
   i) Lahaja
   ii) Lafudhi
b) Tofautisha baina ya lugha ya taifa na lugha rasmi (al.2)
c) Fafanua sifa zozote kuu za sajili ya kisiasa (al. 4)

**MURANGA SOUTH A**
**102/3**
**KISWAHILI**
**KARATASI 3 (FASIHI)**
**KIDATO CHA NNE**
**JULAI 2017**

**SEHEMU A:KIDAGAA KIMEMWOZEA – KEN WALIBORA**

1. Lazima
Kwa kutoa mifano, fafanua maudhui ya utu kama yanavyojitokeza katika riwaya ya kidagaa kimemwozea. (al. 20)

**SEHEMU B:MSTAHIKI MEYA – T AREGE**

Jibu swali la 2 au 3

2. "Mwaka wa kuomba kura utakapofika sitataka mizuka yao kuniandama."
a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (al.4)
b) Eleza maudhui yanayojitokeza katika dondoo hili (al.2)
c) Ufisadi uliokithiri ndio uliokuwa msingi wa matatizo ya cheneo. Thibitisha kwa mifano mwafaka (al. 14)

3. "Majuto ni mujukuu huja baadaye." Thibitisha ukweli wa methali hii ukitoa mifano kutoka kwenye tamthilia ya mstahiki Meya. (al. 20)

**SEHEMU C: USHAIRI**

**SHAIRI**

Hayawihujayakawa, walinena wanenaji
Nyuma walotakwa kuwa, wakawa ndo wajuaji
Nao mbele walokuwa, wakazikosa soseji
Hufika ya wanenaji, hayawi huja yakawa.

Mwendo usimwone waw, damu yake sileleji
Kwa watu akikosewa, kwamba hajipi ujaji
Kimya kikuu angawa, kishindo ukitaraji
Hufika ya wanenaji, hayawi huja yakawa.

Hawanacho walokuwa, huja kuwa wasemaji
Wakawa wanatakiwa, kule wasikotaraji
Hata walioonewa, kama taka za gereji
Hufika ya wanenaji, hayawi huja yakawa.

Hayawi huja yakawa, ulijuwe mjuwaji
Matope waloumbiwa,huziishi za saruji
Na saraji walokuwa, tope likang'ang'aniwa
Hufika ya wanenaji,hayawi huja yakawa.

Mwovu huyo angakuwa, kampe japo kilaji
Sijipe kumumbaguwa,hwenda atawale mji
Kiwa hukumtambuwa, jataka ulimjaji
Hufika ya wanenaji, hayawi huja yakawa

4. (a) Andika kichwa mwafaka cha shairi hili (al. 2)
(b) Taja mbinu mbili za lugha alizotumia mtunzi wa shairi hili (al.4)
(c) Eleza dhamira ya mshairi (al.2)
(d) Eleza umbo la shairi hili (al.4)
(e) Taja methali inayotawala katika shairi (al. 2)
(f) Eleza maana ya msamiati ufuatao kama ulivyotumika kwenye shairi
 i) ujaji
 ii) walotakwa
(g) Onyesha matumizi mawili ya uhuru wa mshairi (al.2)

for free revision past papers visit: www.freekcsepastpapers.com

**SEHEMU D: DAMU NYEUSI NA HADITHI NYINGINE**

5. Uozo katika jamii ni maudhui yaliyoshughulikiwa pakubwa katika diwani ya Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine. Kwa kurejelea hadithi zozote tano fafanua kauli hii (al. 20)

**SEHEMU E: FASIHI SIMULIZI (AL. 20)**

6. a) Eleza istilahi zifuatazo: (al. 12)
   i) Ayani
   ii) Misimu
   iii) Nyiso
   iv) Mbolezi
   v) Mbazi
   vi) Lakabu

   b) Fafanua mbinu nne za kukusanya fasihi simulizi (al. 8)

for free revision past papers visit: www.freekcsepastpapers.com

**MURANGA SOUTH A**
**102/1**
**KISWAHILI**
**KARATASI 1 (INSHA)**
**KIDATO CHA NNE**

**HATI YA KUHITIMU ELIMU YA SEKONDARI**
**MTIHANI WA MWISHO WA MUHULA WA PILI**

**MWONGOZO WA KUSAHIHISHA**
**<u>INSHA</u>**

1. Hii ni barua pepe/mdahilishi
   Mdahilishi uwe na sehemu zifuzatazo:
   - Anayetumiwa
   - Mada/kichwa cha ujumbe
   - Tarehe
   - Kutoka kwa(anwani ya anayetuma barua pepe)
   - Siku, mwezi,tarehe, mwaka na saa ya kutumwa ujumbe
   - Mwanzo
   - Maudhui au ujumbe:
     i) Mtu asiunywe maji yasiyochemshwa
     ii) Kupika chakula hadi kiive vizuri
     iii) Kutenda haja nje bali kutumia vyoo
     iv) Mtu anawe mikono yake kwa sabuni baada ya kutoka msalani
     v) Mtu asile matunda au mboga za majani bila kuziosha kwanza.
     vi) Anayeonyesha dalili ya ugonjwa apelekwe katika kituo cha afya mara moja.
     vii) Uchuuzi wa vyakula upigwe marufuku.
   - Kuaga
   - Jina la anayetuma barua pepe.
2. Mtihani akadirie hoja. Maudhui yasipungue hoja tano
3. Mtahiniwa aandike kisa kinachooana na methali
4. Lazima mtahiniwa aanze kwa maneno aliyopewa kuanzia .
   - Atoe kisa kinachooana na mdokezo huo.
   - Asiyeanza kwa maneno haya amejitungia swali
   - Akiweka kianzio mwishoni amejifungia swali.

for free revision past papers visit: www.freekcsepastpapers.com

**MURANGA SOUTH B**
**102/1**
**KISWAHILI**
**KARATASI 1 (INSHA)**
**KIDATO CHA NNE**
**JULAI 2017**

1. Lazima.
   Umepata kazi ya utangazaji katika kampuni moja nchini. Umealikwa kwa mahojiano. Andika mahojiano kati yako na mkurugenzi wa kampuni hiyo (al.20)
2. Andika kisa kitakachodhihitisha maana ya methali sikio la kufa halisikii dawa (al.20)
3. Jadili mikakati inayotumiwa na serikali kupambana na tishio la usalama nchini (al.20)
4. Andika kisa kitakachomalizia kwa maneno haya
   ………nilitamani ardhi ipasuke inimeze mzima mzima. (al.20)

**MURANGA SOUTH B**
**102/2**
**KISWAHILI**
**KARATASI 2 (MATUMIZI YA LUGHA)**
**KIDATO CHA NNE**
**JULAI 2017**

**UFAHAMU**

Ufupisho ni maelezo ya mawazo au hoja muhimu kuhusu kifungu cha habari au taarifa uliyosoma au uliyoisikia. Maelezo haya yanapaswa kutolewa kwa maneno ya'mfupishaji' mwenyewe. Hapa, ni muhimu tizingatie kifungu:'maneno ya mfupishaji mwenyewe' kwa kuwa nitalirejelea jambo hili baadaye.

Ufupisho ni mojawapo ya stadi muhimu sana zinazotahiniwa katika shule za upili. Stadi hii haiepukiki maishani hata baada ya masomo ya shule ya upili au hata chuoni.

Mathalan, wakati mmoja utajikuta umeteuliwa kuwa katibu wa kikundi fulani na kutakiwa kukiandikia kikundi hicho kumbukumbu za yatakayojadiliwa katika vikao mbalimbali.

Ili kufanya hivyo, unahitaji kuwa naujuzi wa ufupisho. Mara kwa mara, walimu huhitajiwa kuelezea maendeleo ya wanafunzi wao darasani kwa dakika chache.huenda muda huo; wa dakika tano au kumi usimruhusu mwalimu kutoa maelezo ya kina kuhusu kila mwanafunzi darasani ila ataitumia stadi ya muhtasari kufanya hivyo.

Nyanja nyingine zinazohitaji ujuzi wa muhtasari ni uanahabari,uhatibu,uandishi wa ripoti,mahubiri kanisani miongoni mwa nyingine.
Licha ya umuhimu wa stadi hi, wanafunzi wengi hutatizika sana wanapoambiwa kukifupisha kifungu au aya kwa idadi Fulani ya maneno. Utata huu husababishwa na mambo mbalimbali kukiwamo kutolewa vyema kifungu au habari inayotakiwa kufupishwa. Waama stadi yakusoma ni muhimu sana katika kumsaidia mwanafunzi kufupisha habari aliyopewa.

UELEWA
Huwezi kuifupisha habari ambayo hujaielewa. Ufahamu wa kifungu au habari kabla ya kuanza kuifupisha utamfaa mwanafunzi kwa njia mbalimbali. Kwanza, atakuwa na huru wa kuyachagua maneno yake mwenyewe ambayo atayatumia kuifup[isha habari yenyewe.

Pili, utamwezesha kuchagua hoja, mawazo na utondoni muhimu atakaouhitaji katika kufupisha kifngu au taarifa. Tatu, utamsaidia katika kuzitiririsha hoja kwa namna zinavyojitokeza katika kifungu bila kutatiza uelewa wacho. Ni kupitia ufahamu huo ambapo mwanafunzi atakuwa na uwezo wa kuyatathmini yale ambayo ni muhimu katika kifungu alichopewa na kuyaacha nje yale ambayo si muhimu.

Utata mwingine unatokana na hali ya kutekwa na mielekeo ya kibinafsi wakati wa kuchagua hoja na utondoti muhimu. Hapa, mwanafunzi hujikuta amevutiwa sana nay ale yanayompendeza katika kifungu au taarifa aliyopewa na kuacha nje hoja na mawazo muhimu yanayohitajiwa na mtahiniwa.

Hata hivyo, hii haimaanishi kuwa kila hoja au wazo katika kifungu ni muhimu, hapana. Mwanafunzi anapaswa kuwa na uwezo wa kuzichagua kauli, mawazo na mifano muhimu tu. Jambo hili litawezekana tu iwapo amekielewa kifungu au taarifa barabara. Uelewa huo utahitaji kusoma tena na tena. Maswali yafuatayo yanapaswa kumwongoza mwanafunzi wakati wa kuandika ufupisho:
a) Hoja zilizo na uzito ni zipi?
b) Ni maelezo gani muhimu yaliyotumiwa kuunga mkono hoja hizi?
c) Dhamiri kuu ya mwandishi wa kifungu hicho ni ipi?

for free revision past papers visit: www.freekcsepastpapers.com

d) Ni vipi ambavyo hoja zimetiririshwa katika kifungu?
Jambo muhimu analopaswa kulifahamu mwanafunzi ni kuwa uhuru wa kuyatumia maneno yake mwenyewe kukifupisha kifungu haumaanishi kuuvuruga mtiririko wa hoja katika kifungu. Hoja zinapaswa kutiririshwa jinsi zinavyojitokeza kwenye taarifa. Kutaathiri uelewa wa ufupisho

HATUA
Zipo kanuni na hatua mbalimbali za uandishi wa ufupisho ambazo zitamfaa sana mwanafunzi. Kwanza kabisa, ni muhimu kupitia taarifa aliyotakiwa kuifupisha ili pupate mawazo ya jumla; yaani dhamira ya mwandishi. Pili, isome taarifa hiyo barabara ili kuielewa. Tulivyotangulia kusema, huwezi kufupishahabari ambayo hujaielewa vyema. Kutoielewa habari, aghalabu, huwafanya wanafunzi kujaribu kuifupisha kwa kuyagagamiza moja kwa moja maneno yaliyotumiwa na mwandishi kwa'kuyapogoapogoa' yale ambayo hayamvutii au yale ambayo hayaelewi kabisa.

Matokeo yake huwa ni ufupisho <u>hafifu</u> 'uliocheza na maneno tu' na kuacha nje utondoti muhimu. Tatu, ni muhimu sana mwanfunzi kuielewa maana ya jumla au mwelekeo wa mwandishi wa habari anayotakiwa kuifupisha. Zingatia maana ya msamiati na kauli zilizotumiwa kuhusu jinsi kila hoja ilivyoibuliwa na kuendelezwa.

Mwanafunzi achague mpangilio unaofaa kuwasilishia hoja kabla ya kuandikia rasimu ya kwanza. Hatimaye, azingatie idadi maalumu ya maneno aliyoambiwa kukifupisha kifungu kwayo.

**UFAHAMU (AL. 15)**
Soma kifungu kifuatacho kisha jibu maswali yanayofuatia.
Maswali
1. Ufupisho unahusisha zaidi stadi gani mbili? (al.2)
2. Andika mifano ya matumizi ya ufupisho nje ya mazingira ya shule (al. 3)
3. Taja baadhi ya changamoto za wanafunzi katika kuandika ufupisho (al.2)
4. Kuelewa kifungu kuna faida gani kwa mwanafunzi katika ufupisho? (al. 3)
5. Ili kuepusha ufupisho hafifu mwanafunzi afaa afanyeje? (al.3)
6. Eleza maana ya maneno haya kulingana na kifungu (al. 2)
a) Waama
b) Utata

for free revision past papers visit: www.freekcsepastpapers.com

**<u>UFUPISHO</u>**
Mwanafunzi yeyote wa lugha anayemtarajia na kumtegemea mwalimu wake kumpa kila kitu katika stadi za lugha si mwanafunzi mzuri wa lugha. Nafikiri kwamba walimu wamejibebesha mzigo mkubwa zaidi wa kufundisha kila kitu badala ya kuwa waelekezaji, nao wanafunzi wamehiari kuwabebesha walimu mzigo huo ambao kwa kweli unapaswa kuwa wao hao wanafunzi. Matokeo yamekuwa ni kudorora kwa kiwango cha lugha zote zinazofundishwa katika asasi zetu za elimu.

Hatuwezi tukawa na wahitimu mahiri waliobobea katika lugha za Kiswahili na kiingereza kama watakuwa toka mwanzo hadi mwisho wanafunzi wategemezi. Udhaifu wa lugha tuliona umesababishwa kwa akali kubwa na haali ya kukijenga na kukilea kizazi cha wananfunzi wategemezi. Waswahili husema:"kuuliza si ujinga." Lakini nafikiri kwamba wategemezi nao wamekithiri si katika kuuliza tu bali katika kuulizauliza mambo ambayo kwa bidii yao ndogo wanaweza kujipatia majibu wenyewe. Kauli yangu ni kwamba ingawa kuuliza si ujinga, baadhi ya maswali yanaashiria uzembe na utepevu wa wanaouliza. Kwa hivyo, ni kweli kwamba kuuliza si ujinga, ila kuulizauliza ni ujinga wa utegemezi uliopindukia.

Badala ya kujiuliza na kujitafutia jibu wenyewe, lao huwa ni kuulizauliza tu. Nao hukera wanapouliza maswali ambayo wangepata majibu kama wangefanya marejeleo kidogo katika vitabu vya rejea na kamusi, kujua kwa mafano;Yellow ni nini kwa Kiswahili? Apple huitwaje katika lugha ya Kiswahili?

Ung'amuzi

Lugha inamtaka mtu anayeng'amua asichokijua na mwenyewe atafute namana ya hatimaye kukijua bila kupitia njia za mkato. Lugha inataka mtu mwenyewe kufungua kurasa za vitabu na kutafuta, kuchakura na kusakura hazina iliyofichama humo. Lugha haitaki mtu anayezembea tu na kusubiri kudondoshewa nazi na neema za lugha kutoka kwa wakwezi wengine; Inamtaka mtu mwenyewe kukwea mnazi;awe mkwezi. Lugha inamtaka mtu mwenyewe apige mbizi katika kina cha bahari ili aibuke na lulu, si kusubiri kupigiwa mbizi na kuletewa na wengine.

Nakisi tuliyo nayo kilugha inatokana na uzembe na utegemezi. Walimu wanalo jukumu la kuwafanya wanafunzi wao wajitegemee. Wasome vitabu vichache vinavyoteuliwa na walimu, na pia vitabu vingi na vyanzo vingine vya maarifas wanavyoviteua wao wenyewe. Kumbuka asilimia tisini ya umilisi wa lugha inafaa itokane na juhudi za mwanafunzi mwenyewe; walimu watoe asilimia kumi tu.

Na mtu wa kando hawezi kufanya kazi ya mwalimu ya kumwezesha mwanafunzi apate uwezo wa kujitegemea. Mtu wa kando ajaye kama mwezeshaji au msemaji mgeni shuleni au katika kongamano au warsha ya walimu au wanafunzi, ni mshajiishaji au shabiki tu. Kwa hivyo, ninapoalikwa katika kuhutubu, mwalimu asinitarajie nitamfanyia kazi ya kumwezesha mwanfunzi kwa asilimilia 10. Naye mwanfunzi akishawezeshwa, asitarajie mwalimu kumfanyia kazi yake ya kujijenga kilugha kwa asilimilia 90. Hiyo ndiyo siri ya kuondokana na kero ya wategemezi na makupe wa lugha ambao lao kubwa huwa kuulizauliza tu.

Ufupisho (al. 15)

a) Fupisho aya tatu za kwanza kwa maneno 75 (al. 5)
b) Kwa kutumia maneno 85 fupisha aya 3 za mwisho (al. 7)

**MATUMIZI YA LUGHA**

1. Andika sauti mbili za kaakaa gumu (al. 2)
2. Onyesha muundo wa neno hili (al. 1)
3. Eleza maana ya sentensi amabatano (al. 2)
4. Yakinisha sentensi hii (al. 2)
   Wanafunzi wote hawakupita wala hawakutuzwa
5. Andika kinyume cha sentensi ifuatayo (al.2)
   Tia machungwa kapuni na maua uweke mezani
6. Tambua wakati uliyotumiwa katika sentensi hii. (al. 2)
   Nilikuwa nikilalamika sana
7. Eleza matumizi ya kiambishi ki- katika sentensi hizi (al.3)
   (i) Kwao hakuendeki
   (ii) Kijitu kiliondoka haraka.
8. Andika kwa wingi (al. 2)
   Usipoziba ufa utanjenga ukuta.
9. Andika kwa msemo halisi (al.2)
   Mwalimu aliniomba nimletee vitabu ofisini
10. Andika upya bila kutumia amba. (al. 2)
    Wanyama ambao hufugwa mbugani ni hatari.
11. Viambishi ni nini? (al. 2)
12. Ainisha viambishi katika neno hili (al. 2)
    Kinachopikika.
13. Adika katika hali ya wastani (al. 2)
    Buzi hilo limekula guo lote
14. Changanua kwa kutumia mishale (al. 4)
    Mtoto aliyeugua amepelekwa hospitalini.
15. Tunga sentensi kuonyesha matumizi ya mshazari /mkwaju (al.2)
16. Unda kitenzi kutoka kwa nomino rutuba (al. 1)
17. Tambua vishazi katika sentensi hii. (al. 2)
    Kitabu utumiacho kina mafunzo mengi
18. Nyambua kitenzi –ja katika hali ya kutendeana kisha tunga sentensi (al. 2)
19. Andika katika hali ya kuamuru (al. 1)
20. Tambua shamirisho katika sentensi hii (al. 2)
    Mwana ataletewa zawadi na mjombake.

**ISIMU JAMII (ALAMA 10)**

1. Kwa nini kulikuwa na haja ya kusafirisha lugha ya Kiswahili? (al. 5)
2. Taja sifa za sajili ya vijana (al. 5)

for free revision past papers visit: www.freekcsepastpapers.com

**MURANGA SOUTH B**
**102/3**
**KISWAHILI**
**KARATASI 3 (FASIHI)**
**KIDATO CHA NNE**
**JULAI 2017**

**MTIHANI WA MWISHO WA MUHULA WA PILI**

**SEHEMU A – TAMTHILIA – MSHAHIKI MEYA**

Lazima

1. (a) Upinzani dhidi ya Meya unachochewa na vitendo vyake. Fafanua kauli hii kwa mifano mwafaka (al. 12)
   (b) Eleza maana ya majazi (al. 2)
   (c) Onyesha namna mbinu hii inavyodhihirika kwa kurejelea (al.6)
      a) Sosi
      b) Kheri
      c) Cheneo

**SEHEMU B : RIWAYA KIDAGAA KIMEMWOZEA**

2. Damu nzito kuliko maji ati.
   i) Eleza muktadha wa dondoo hili. (al. 4)
   ii) Taja tamadhali ya lugha iliyotumiwa (al. 2)
   iii) Fafanua ukweli wa falsafa hii ukirejelea riwaya nzima (al.14)
3. Eleza kwa utondoni matatizo yoyote kumi ya uongozi yanayojitokeza katika riwaya ya kidagaa kimemwozea (al. 20)

**SEHEMU C: HADITHI FUPI – DAMU NYEUSI NA HADITHI NYINGINE**

4. Kwa kurejelea hadithi mwana wa darubini na ndoa ya samani eleza athani za imaskini (al. 20)
5. (a) Huku ukirejelea hadithi ya Damu Nyeusi . Onyesha namna mwandishi alivyotumia mbuni rejeshi kufanikisha ujumbe wake. (al. 10)
   (b) fafanua wasifu wa mhusika mkuu katika hadithi Damu Nyeusi (al. 10)

**SEHEMU D: FASIHI SIMULIZI:**

6. (i) Eleza maana ya miviga. (al. 2)
   (ii) Taja mifano 5 ya miviga katika jamii za kiafrika, kabla ya kuja kwa wamishenari (al. 5)
   (iii) Eleza majukumu ya miviga (al. 5)
   (iv) Taja na ueleze vitambulishi vya fasihi simulizi. (al.8)

**SEHEMU E: USHAIRI**

HINI GILASI YA MWISHO!

Kazini loanza zama, kusema na Mama Pima
Leo inafika tama, mbele sitoi sukuma
Nimezama nimezama, na kwa wengi sikusema
Hini gilasi yamwisho!

Hini gilasi ya mwisho, nyingine sitotazama
Sitaki mahangaisho, ya vito vya mama pima
Si leo katu si kesho, mitaro kulala jama
Hini gilasi ya mwisho!

Tupo tusolipa karo, wana shule kutotuma
Kwa sababu ya umero, wetu huja baki nyuma
Na kushonwa matakuro, na wenzao wanasoma
Hini gilasi ya mwisho!

Hini ya mwisho gilasi, nimesema nimesema
Afadhali kula nyasi, nisiwe nabaki nyuma
Wenzetu waliziasi, uchumi wameuchuma
Hini gilasi ya mwisho!

for free revision past papers visit: www.freekcsepastpapers.com

Maswali

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Hili ni shairi la aina gani? | (al. 2) |
| 2. | Eleza toni ya mshairi | (al. 2) |
| 3. | Onyesha uhuru wa mshairi | (al. 4) |
| 4. | Taja mbinu mbili za lugha zilizotumiwa katika shairi | (al. 2) |
| 5. | Tambua nafsineni katika shairi hili | (al. 2) |
| 6. | Taja hasar anazozungumzia mshairi zilizoletwa na tabia yake. | (al. 2) |
| 7. | Eleza maamuzi anayotoa mshairi | (al. 3) |
| 8. | Taja bahari mbili za shairi hili | (al. 2) |
| 9. | Kibwagizo kina umuhimu gani katika shairi hili? | (al. 1) |

for free revision past papers visit: www.freekcsepastpapers.com

**MURANGA SOUTH C**
**102/1**
**KISWAHILI**
**KARATASI 1 (INSHA)**
**KIDATO CHA NNE**
**JULAI 2017**

**INSHA**

1. Wewe ni raia katika nchi ya Tomoko katika nchi yako, kuna ongezeko kubwa la utovu wa nidhamu miongoni mwa vijana. Andika barua kwa mhariri wa gazeti la Tomoko leo ukitoa maoni yako kuhusu vianzo vya utovu huu wa maadili.
2. Utawala wa kimaeneo(ugatuzi) umeleta faida nyingi nchini Kenya. Jadili
3. Andika kisa kitakachodhihirisha maana ya methali: baada ya dhiki faraja.
4. Tunga kisa kitakachomalizika kwa maneno yafuatayo:
   ………… alipompata mtoto wake aliyepotea, alishusha pumzi.”Mungu hamsahau mja wake.” Akasema huku akifurahi ghaya

**MURANGA SOUTH C**
**102/2**
**KISWAHILI**
**KARATASI 2 (MATUMIZI YA LUGHA)**
**KIDATO CHA NNE**
**JULAI 2017**

**SEHEMU YA KWANZA (ALAMA 15)**

**UFAHAMU**

MAJILIO ya wakoloni barani Afrika ambao walidumisha utawala wao katika’bara jeusi’ kwa takriban kipindi cha miaka sabini kulisababisha mivutano ya kiisimu mpaka leo (Ngugi,1993,uk 42)

Wakoloni walizipa kipaimbele lugha za kigeni na kuzikandamiza zile za kiasili zisiweze kuelezea uhalisi wa maisha katika viwango vya teknolojia. Kwa hakika, itazichukua lugha hizi muda mrefu kwenda sambamba na maendeleo ya fikra na teknolojia kwa kutoandaliwa vyema kutekeleza wajibu huu.

Lugha ni kipengele muhimu sana cha utamaduni. Hivyo basi serikali zinawajibika kuzilinda, sio tu kwa sababu lugha zimejaa maarifa mengi ya tangu jadi, bali pia kwa sababu lugha ni chombo cha maendeleo ya binadamu.

Maarifa yote na ufanisi wa binadamuu huelezwa kupitia kwa lugha. Mwelekeo ulioonekana kishika sana katika mataifa megi barani afrika, ikiwemo Kenya, ni kuhusudu lugha na tamanduni za kigeni. Lugha za kigeni zimehusishwa na maendeleo na ustaarabu.

Hatua iliyochukuliwa na serikali ya Tanzania ya kufunza masomo yote kwa lugha ya Kiswahili kuanzia darasa la kwanza hadi chuo kikuu ilizua kejeli na kicheko kwa baadhi wa wakenya; hususan katika stesheni za fm. Kisa na maana: jambo hili haliwezekani!

Je, ni lazima tutegemee lugha za kigeni kupiga hatua kimaendeleo? La hasha! Kuna ushahidi wa mataifa kama vile Uchina, Ufini,Sweden, Indonesia,Japan,Malaysia, India,Uyahudi n.k. yalioendeleza lugha zao kimakusudi ili ziweze kukidhi haja kufundishia masomo yote hadi viwango vya juu sana vya elimu.

Katika sherehe za kuadhimisha siku ya kimataifa ya ‘lugha mama’ miongoni mwa mataifa wanachama wa umoja wa mataifa (united Nations International Mother Language Day) mnamo februari, 2000, mkurugenzi wa shirika la umoja wa mataifa kuhusu Elimu,sayansi na utamanduni(UNESCO), jenerali koichiro Matsuura alisema: ‘mojawapo ya vigezo vitumiwayo na wataalmu kukadiria iwapo lugha Fulani inatishiwa kuangamia au kufa ni iwapo watoto wanajifunza lugha hiyo…

Iwapo takribani asilimia 30 ya watoto, hawajifunzi lugha yao’ya mama’, basi lugha hiyo inatishiwa kuangamia… lugha hiyo bila shaka huenda ikafa pamoja na kizazi kinachoizungumza.’

Kwa mujibu wa UNESCO, lugha nyingi ambazo zimetishiwa kufa au kutoweka zinapatikana katika mabara ya merakani na Australia. Shirika hililinaongeza kuwa, nchini Kenya, lugha kama vile suba,El Molo, Lorkoti, Yaaku sogoo,kore,Segeju,Omotik, na KInare’ zimekufa’ au kutoweka huku Bong’om na Terik/Tiriki zimo kwenye hatari ya kutoweka.

Lugha pia huangamia wakati ambapo lugha hizo zinashindwa kuzihudumia jamii zao ipasavyo kama chombo mahsusi cha mtagusano wa kijamii. Baadhi ya lugha huku na kusambaa huku zingine zikididimia na hatimaye’kumezwa’ na lugha zilizoshaimiri au hata kutoweka kabisa. Kwa mfano, jamii ya Seng’wer ‘imemezwa’ na makabila kama vile Wapokot, Wamarakwet, Wakeiyo, Watugen, Wanandi na Waluhya, ilhali Wakipsigis,Watugen na Wamaasai’wammeza’jamii ya Ogiek.

for free revision past papers visit: www.freekcsepastpapers.com

Hata hivyo,mkaoni nyanza ya kusini nchini Kenya, wakakti wa uchaguzi mdogo wa useneta katika gatuzi ya Homabay, tulisikia kupitia kwa profesa….(aliyewania kiti), kwamba jamii ya Abasuba ipo-wala'haijamezwa' na jamii ya waluo.

Msimamo wa wizara ya elimu nchini Kenya kuhusu ufundishaji wa 'lugha ya mama' unaonekana kuyumba. Mara tunaambiwa lugha ya mama itafundishwa katika madarasa ya chini katika shule za mashambani; mara tunaambiwa itafundishwa katika madarsa ya chini katika maeneo Fulani; ilimradi wizara haijitokeza waziwazi na sera wala mwongozo mwafaka.

Njogu (2003) anahoji;'mkondo uliopo nchini Kenya hivi sasa ni ule wa jamii nyingi kuwahimiza watoto wao kuzungumza lugha za kigeni kama vile kiingeraza, kifaransa, na hata kijerumani na kupuuza lugha ya kwanza. Hii inatokanan na imani kuwa lugha za kigeni ndizo zitakazofungua njia za kigeni ndizo zitakazofungua njia za maendeleo hapo baadaye.

Mkondo huu usipozuiliwa, huenda ukasababisha vifo vya lugha za kiasili' Njogu anaendelea: 'uwezo wa kuongea lugha nyingine pamoja na yenye asili ya kikoloni huweza kujenga jisia za kujiamini miongoni mwa watu wasiokuwa na uwezo mwingi wa kiuchumi-nako kujiamini ni hatua ya awali ya kuleta maendeleo ya jamii'MAKIWA! Familia, jamaa na marafiki wa Grace Ogot aliyeandika baadhi ya kazi zake kwa lugha ya mama.

Maswali

1. Ni nini kisababishi cha mivutano ya kiisimu katika bara la afrika (al. 2)
2. Serikali zinafaa kuwajibika katika kuzilinda lugha . eleza (al. 2)
3. Ni hatua gani ambayo ilichukuliwa nan chi ya Tanzania ambayo ilizua kejeli na kicheko kwa baadhi ya wakenya (al. 1)
4. Lugha ya mama inasemekana kuwa katika tishio la kuangamia kwa kutumia vigezo gani? (al. 2)
5. Kwa nini jamii nyingi huwahimiza watoto wao kuzungumza lugha za kigeni kigeni (al. 2)
6. Kuna mabara ambayo yametajwa kuwa na lugha nyingi ambazo zinatishiwa na kufa au kutoweka. Yataje mabara hayo. (al. 2)
7. "Msimamo wa wizara ya elimu kuhusu ufundishaji wa lugha ya mama unaonekana kuyumba " Eleza (al. 2)
8. Eleza maana ya msamiati ufuatayo kwa mujibu wa taarifa au ufahamu
   i) Takriban
   j) Mtagusano

for free revision past papers visit: www.freekcsepastpapers.com

**<u>UFUPISHO</u>**

TUMEKWISHA kueleza katika makala ya hapo awli kuwa lugha ni maalum kwa binadamu tu na kwamba hakuna kiumbe yeyote ambaye si mwanadamu mwenye uwezo wa kujua, kujifunza na kutumia lugha zaidi ya binadamu.

Bila shaka, mawasiliano ya binadamu yanaweza kujumuishwa kama mawasiliano ya wanyama yaliyoendelezwa. Utafiti wa mawasiliano ya wanyama, uitwao'zuosemiotiki'(zoosemiotics) tofauti na 'athroposemiotiki'( utafiti wa mawasiliano ya binadamu), umechangia pakubwa katika ukuzaji wa uwezo wa mnyama wa kutambua. Jambo hili ni dhahiri kwani binadamu wanaweza kuwasiliana na wanyama kwa kutumia njia za kipekee lakini si'lugha'.

Makala haya yanalenga kuthmini na kuzamia sifa au tabia za lugha ya mwanadamu. Kimsingi sifa ai Tania hizi ndizo zinazoitofautisha lugha ya mwanadamu na aina nyinginezo za mawasiliano zitumiwazo na ndege au wanyama.

Unasibu wa lugha ya binadamu unaangaliwa katika ukweli kwamba binadamu hazaliwi na lugha, anakutana nayo kwa unasibu tu. Hakuna uhusiano wa moja kwa moja au wa aili kati ya kitajwa(kitu au umbo linalomaanishwa au maana).

Uhusiano wake ni wa unasibu na unatokana na makubaliano ya watu wajua – lugha yao. Hata makubaliano haya ya kwamba kitu kiitwe au dhana Fulani iitwe na kuelezwa kwa namna Fulani ni ya kinasibu tu. Hapa tunamaanisha kwamba mkutano au kikao ambaco binadamu amewahi kukaa akasema mathalani neno "chuki" limaanishe hali ya kutompenda mtu au neno "upendo" limaanishe hali ya kuonesha huba kwa mtu. Kila jamuiya-lugha ina namna yake ya kuufasili na kuelekezea ulimwengu kwa lugha yake ambayo inatofautiana na jamuiya-lugha nyingine.

Lugha ya mwanandamu inao uwezo wa kuambukiza utamanduni kutoka katika kizazi kimoja kwenda kizazi kingine au kutoka katika jamuiya-lugha moja kwenda katika nyingine. Leleweke kuwa, uwezo huu wa kuambukiza maarifa ya lugha hufanyika kwa njia ya kusoma au kujifunza na si kurithi. Kwa mfano, mtu anaweza kurithi. Kwa mfano, mtu anaweza kurithi maumbile kutoka kwa wazazi wake, mathaalan aina ya nywele, macho, pua, kucha au masikio lakini mtu hawezi kurithi lugha.

Lugha inamfikia kwa kuambukiza katika jamuiya-lugha anayokulia na kulelewa. Yatupasa tukumbuke kuwa, ingawa mwanadamu anazaliwa na ule uwezo(kitengo cha lugha) wa kujifunza lugha"language Acquisition Device"kama anavyoeleza mwanaisimu Naom Chomsky, lakini hazaliwi na lugha. Hii ndiyo sababu mwanandamu anaweza kujifunza lugha yeyeote ile na kwa wakati wowote maadamu yupo katika mazingira na hali ya kawaida na saidizi.

Lugha ya mwanandamu imepangwa katika viwango viwili ambavyo vinashirikiana na kukamilishana. Kiwango cha kwanza I kile kiwango cha utamkaji wa sauti au utoaji wa sauti kwa kutumia ala mbalimbali za matamshi. Sauti hizi zikisimama peke

yake hazina maana yoyote, ni kama milio tu kama kupiga chafya, au kelele zinazotokana na kubururwa kwa meza kwenye sakafu au kelele za injini ya pikipiki.

Sauti hizi zinapounganishwa (kwa kufuata sheria, kanuni na taratibu za lugha husika) tunapata kiwango kingine cha pili cha maana. Sifa ya uwili inadhihirisha sifa ya uwekevu katika lugha ya mwanadamu kwani kwa kutumia sauti hizi chache mzungumza lugha anaweza kutunga na kutamka sentensi nyingi au tungo nyingi na zenye maana tofauti tofauti bila kikomo

Suala jingine la msingi ni kwamba, tunaposema kuwa lugha imegawika katika viwango viwili, kiwango cha sauti na kiwango cha maana haimaanishi kwamba binadamu anatumia viwango hivi kuipekepeke. Hata siku moja mwanadamu hasemi kwamba sasa naanza kutamka sauti za neno Fulani, halafu ndiyo niweke maana yake. La hasha!

Binadamu hutamka kwa mara moja sauti pamoja na maana zikiwa zimebebana ndani kwa ndani(hutamka sauti pamwe na maana). Yaani, wakati anatamka sauti na kuziunganisha ndiyo wakati anaambatanisha na maana ndani yake. Hii ndiyo sifa au uwili katika lugha ya mwanadamu.

Uzalikaji katika lugha ya binadamu unajidhihirisha katika uwezo wa mwanandamu kubuni na kuunganisha maneno na miundo mbalimbali ya tungo bila kikomo. Mjuzi wa lugha anastahili kutunga na kuzielewa tungo mbalimbali ikiwa ni pamoja na zile ambazo hajawahi kuzisikia wala kuzitunga yeye mwenyewe.

Aidha, anapaswa kuelewa tungo zilizotungwa na watu wengine na kufahamu maana ya kisemantiki na ile kipragmatiki zinazodhihirika kadri anaposimbua jumbe zilizomo. Anapaswa kuzielewa tungo sahihi na zile zisizo sahihi. Hivyo uwezo huu unatofautiana na aina nyingine ya mawasiliano inayotumiwa nan a wanyama wengine, kwa mfano,"nyenje ni mnyama mwenye milio au ishara nne za kuchagua ili awasiliane, tumbili ana miito sita tu. Hivyo wanyama wote hawa wana idadi isiyobadilika ya milio na sauti au ishara na hawana uwezo wa kubuni namna nyingine ya kuwasiliana au kubuni milio mingine ya kuwezesha na kudumisha mawasiliano yao.

Maswali

a) kwa maneno kati ya 50- 60 fupisha aya tau za kuanza (al. 8. 1 mtiririko)

b) kwa kutumia maneno 60-70 bainisha ujumbe ambao mwandishi anaibua katika ya tatu za mwisho (al. 7, 1 mtirirko)

**<u>SEHEMU YA TATU: SARUFI NA MATUMIZI YA LUGHA (ALAMA 40)</u>**

1. Bainisha sifa za sauti ifuatayo /o/ (al. 2)
2. Kambishi ni nini? (al. 1)
3. Onyesha matumizi ya kiambishi "ku" katika sentensi ifuatayo
   Nitakupa fedha za mchango ili uende ukaniwakilishe (al. 2)
4. Nyambua vitenzi vifuatavyo katika kauli zilizowekwa katika mabano
   i) pa(kutendeka)
   ii) ha(kutendewa) (al. 2)
5. Tunga sentensi moja katika wakati ujao hali timilifu (al. 1)
6. Onyesha aina za virai katika sentensi ifuatayo.
   Mteja wangu atawasili kesho saa tatu (al. 2)
7. Tumia kivumishi kionyeshi kisisitizi cha mbali kidogo pamoja na nomino katika ngeli ya li-ya kutunga sentensi (al. 2)
8. Tunga sentensi moja yenye kishazi huru na kishazi tegemezi ukitumia'o' rejeshi tamati (al. 2)
9. Changanua sente4nsi ifuatayo kwa jedwali/visanduku
   Mkulima alilima kwa bidii lakini hakupata mazao mengi (al. 4)
10. Onyesha aina za shamirisho katika sentensi uliyopewa
    Babu alisomewa barua na mjukumu wake
11. Tunga sentensi mbili ili kuonyesha matumizi ya kiambishi 'po' cha
    (i) Wakati
    (ii) Mahali
12. Changanua kitenzi kufuatacho (al. 4)
    Alimlisha.
13. Kwa kutunga sentensi eleza matumiz mawili tofauti ya kiakifishi (al. 2)
    Parandesi
14. Eleza maana ya sentensi ya masharti (al. 1)
    Tunga sentensi ya masharti (al. 2)
15. Andika visawe vya maneno yaliyopigiwa mstari
    Daktari alipokuwa akimtibu alishikwa na kisulisuli (al. 2)
16. Bainisha kihisishi na kihusishi katika sentensi
    Naam! Ameingia kabla ya mwalimu kufika (al. 2)
17. Andika sentensi ifuatayo kwa msemo wa taarifa
    "nitaweza kuondoka kwangu kesho asubuhi."mwalimu akasema (al. 3)
18. Bainisha kiima na chagizo katika sentensi
    Mwenyewe alimpenda kwa dhati (al. 2)

for free revision past papers visit: www.freekcsepastpapers.com

**SEHEMU YA NNE: ISIMU JAMII (ALAMA 10)**

1. Taja dhana au nadharia zinazohusiana na chimbuko la lugha ya Kiswahili (al. 3)
2. Eleza maana ya istalahi zifutatazo kama zinavyotumika katika isimujamii
   i) misimu
   ii) lafudhi
   iii) pijini (al. 3)
3. Taja sifa nne za sajili ya maabadini (al. 4)

for free revision past papers visit: www.freekcsepastpapers.com

**MURANGA SOUTH C**

**102/3**
**KISWAHILI**
**KARATASI 3 (FASIHI)**
**KIDATO CHA NNE**
**JULAI 2017**

**SEHEMU YA A: FASIHI SIMULIZI**

1. Lazima.

a) Taja sifa tano zinazotambulisha fasihi simulizi (al. 5)

b) (i) ngano ni nini? (al. 2)

(iii) baadhi ya ngano huwa na fomula maalum za ufunguzi na hitimisho. Fomula ya ufunguzi ina umuhimu gani? (al. 5)

(iii) eleza umuhimu wa nyimbo katika utambaji wa ngano (al. 4)

(c) eleza istalahi zifuatazo katika maghani masimulizi

i) tendi

ii) rara (al. 4)

**SEHEMU YA B: TAMTHILIA**

2. "Tamaa hatujakataa. Hata hivyo inavunja moyo kuona mabo kama haya ya watu kuvurumishwa na askari…

a) Eleza muktadha wa dondoo hili (al. 4)

b) Mbali na kuvurumishwa na askari, ni masaibu yapi mengine wahusika hawa walizungumzia katika kikao hiki (al. 6)

c) Taja tamathali ya lugha iliyotumika katika dondoo hili (al. 2)

d) Eleza wasifu na umuhimu wa msemezwa (al. 8)

3. "……. Ikiwa hii si insubordination ni nini?"

a) Eleza muktadha wa dondoo hili

b) Taja mbinu za kimtindo au tamathali za lugha zinazojitokeza katika dondoo hili (al. 2)

c) Nukuu hili linadhihirisha mgogoro baina ya wahusika wawili. Taja migogoro yoyote mingine mine katika tamthilia (al. 8)

d) Jadili njia ambazo wanacheneo walijaribu kutumia ili kultea mabadiliko baada ya changamoto nyingi kuwakumba. (al. 6)

**SEHEMU YA C: RIWAYA**

4. ….. mbali na kuambukizwa yale maradhi yasiyosikia dawa ambayo baadhi ya dalili zake ni kufichaficha faili za watu…

a) Eleza muktadha wa dondoo hili (al. 4)

b) Taja na ueleze sifa za aliyeambukizwa maradhi yasiyosikia dawa (al.8)

c) (i) ni maudhui gani yanayojitokeza katika dondoo hili (al. 2)

(ii) Thibitisha maudhui katika/i/ huku ukirejelea riwaya nzima (al. 6)

5. Kwa kurejelea riway ya kidagaa kimemwozea thibitisha mbinu zifuatazo (al. 20)

i) barua
ii) sadfa
iii) barua
iv) majazi

for free revision past papers visit: www.freekcsepastpapers.com

**SEHEMU D: USHAIRI**

Jinalo limetukuka, kutkoka jadi mwanzoni
Milele hutadunika, hata kwa pigo vitani
Ulugha uloumbika, muundo wa wasitani
Hakuna wa kukuponda, mwana mwema Kiswahili.

Kila anokuutamka,hukunyambua kifani
Hasemi kuhakahaka, ja mwana wa uchangani
Vitabuni kitumika, hupumbaza nyoyo ndani
Na milele hutavunda, mwana mwema Kiswahili.

Mja akikitamka, mwenyenji ama mgeni
Msikizi huridhika, ungiavyo mdomoni
Humwondokea wahaka, ukapenya sikioni
Hapana wa kukushinda, mwana mwema Kiswahili.

Vitabuni huchpika, ukashawishi maoni
Hutuwili kila rika, wakakutuza nishani
Name ninakuzindika, usambae duniani

Hawapi wa kukukinda, mwana mwema Kiswahili.

Kiswahili tokatoka, uenee duniani
Kila baidi we fika, pembe'ne ulimwenguni
Ukizamishwa ibuka, uabiri kila kani
Hazuki wa kukushinda, mwana mwema Kiswahili.

Kwa vina umeubika, umeshinda kilatini
Na mizani za mwafaka, utamkwapo wimboni
Nishani nitakutwika, utamalaki maoni
Hazuki wa kukushinda ,mwana mwema Kiswahili.

Nakuaga mtukuka, Kiswahili mwenye mboni
Kitabani nakuweka, wasome mamilioni
Utuwe kusalimka, maombi ya mwarandani
Hayuko wa kukufyanda, mwana mwema Kiswahili

Maswali

1. Pendekeza anwani inayofaa shairi hili (al. 2)
2. Ni mbinu gani ya lugha ambayo imetumika katika mshororo wa mwisho wa ubeti wa pili (al. 2)
3. Eleza toni ya shairi hili (al. 2)
4. Uhuru wa kishairi umetumikaje katika shairi hili (al. 3)
5. Shairi hili linaweza kuwekwa katika bahari gani. Taja mbili (al. 2)
6. Eleza muundo wa shairi (al. 4)
7. Msahiri anatoa ujumbe gani katika ubeti wa sita (al. 3)
8. Eleza maana ya:
   i) na milele hutavunda
   ii) Kiswahili mwenye mboni (al. 2)

**<u>SEHEMU YA E: HADITHI FUPI</u>**

"hilo ni jambo la kutia moyo sana. Wewe basi lazimia u msichana mwerevu"

a) Eleza muktadha wa dondoo hili (al. 4)
b) Eleza athari za kimagharibi kwa mujibu wa hadithi hii (al.6)
c) (i) kwa kurejelea hadithi ya'mizizi na matawi. Thibitisha mbinu ya majazi (al. 5)
d) Mwanamke amesawiriwa vipi katika hadithi ya maeko (al. 5)

for free revision past papers visit: www.freekcsepastpapers.com

**COMPLIANT PREPARATORY EXAMINATION**
**102/1**
**2017**
**KISWAHILI**
**Karatasi ya 1**

1) **LAZIMA**
Mwandikie rafiki wako aliye ughaibuni barua pepe huku ukimweleza unvyojiandaa kufanya mtihani wa kitaifa mwishoni mwa mwaka huu.
2) Wizara ya Elimu imeweka mikakati kabambe ili kukabiliana na suala la udanganyifu katika mitihani ya kitaifa. Thibitisha ukweli wa kauli hii.
3) Kumcha Mungu si kilemba cheupe.
4) Andika insha inayomalizika kwa maneno yafuatayo:
…ndipo niligundua umuhimu wa kutia bidii masomoni.

**COMPLIANT PREPARATORY EXAMINATION**
**102/2**
**2017**
**KISWAHILI**
**Karatasi ya 2**
**LUGHA**

**1. UFAHAMU**

**Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali yanayofuata**

Lugha inaweza kuelezwa kwa jumla kuwa ni mfumo wa mawasiliano.Haiyamkiniki kwa mtu yeyote kueleza chanzo au kiini cha lugha na sote tunakubaliana kuwa matumizi yake yameanza tangu kuumbwa kwa binadamu kwani ni vigumu kukisia kuwepo ya watu bila lugha ya mawasiliano yeyote ile.

Katika taifa lolote, huwapo na lugha moja au hata zaidi ya moja ambayo huwa ndicho chombo cha mawasiliano ya taifa katika nyanja za elimu, maandishi, siasa na biashara. Kwa mfano, mataifa kama vile Kanada hutumia lugha mbili kwa usawa kama lugha za taifa na za kikazi. Maana ya lugha ya taifa ni lugha moja ambayo huteuliwa kutumika katika shughuli zote za kitaifa hasa katika nchi yenye lugha nyingi za kabila. Lugha ni muhimu sana kwa maisha na maendeleo ya taifa lolote lile. Lugha ni kiungo cha kueneza umoja na uelewano miongoni mwa jamii nyingi tofauti na huwa kama kitambulisho kwao kuwa wao ni ndugu wa jamii moja kubwa yaani taifa lao.

Kenya ni mfano mzuri wa taifa lenye lugha nyingi zinazozidi 40 za vikundi vidogo vidogo vya kikabila. Hapo kabla ya miaka mia moja hivi iliyopita kila kimojawapo cha vikundi hivi kilijitambulisha kama kabila huru. Baada ya kuja kwa serikali ya kikoloni hasa baada ya Kenya kujinyakulia uhuru, haja ya kuwaunganisha raia wote chini ya taifa moja lenye uongozi na shabaha moja lilikuwa ndilo jambo lililozingatiwa sana. Kwa hivyo, utamaduni wa taifa la Kenya ni mchanganyiko wa tamaduni za watu wengi wenye mila, desturi, imani na itikadi tofauti. Utamaduni humaanisha jumla ya imani na tabia za watu wa jamii fulani. Amali hizi hufungamanisha fikira, ustaarabu, mila, taasiri na sanaa za aina zote za jamii inayohusika. Ili kujieneza na kujiimarisha, taifa huhitaji chombo hicho kuwasiliana na kuwaunganisha watu wake wenye asili mbalimbali. Chombo hicho huwa ni lugha ambayo huwa siyo tu kwamba ni sehemu ya utamaduni wa jamii bali ni njia muhimu sana ya kuwatawanyia na kustawishia ule utamaduni.

Katika taifa leo lugha nyingi kama Kenya kwa mfano, lugha ya taifa inayozungumzwa na kueleweka na baadhi kubwa ya raia ambayo imekiuka mipaka na tofauti za kikabila ni njia muhimu sana ya kueneza maongozi ya taifa na kuleta ufahamikiano bora kote nchini. Kama zilivyo taasisi kama wimbo wa tafia, bendera ya taifa au bunge la taifa, lugha ya taifa ndicho kilelezo cha taifa lolote lile lililo huru. Lugha kama hiyo huvunja na kukomesha hisia za kibinafsi na kikabila na badala yake kuunda moyo wa uaminifu wa kitaifa.

Zaidi ya kuwa chombo cha mawasiliano, lugha ni kielelezo cha fikira na hisia za binadamu. Lugha ya watu fulani haituelezi tu ujuzi au maarifa yao bali pia mtazamo wao wa kimaisha, falsafa na mawazo yao. Kwa ufupi, lugha hutufahamisha namna akili za watu wazungumzao ile lugha zinavyofikiri na kufanya maazimo. Lugha ni sehemu ya utamaduni wa taifa tulimozaliwa na lazima lugha hiyo ifunzwe katika muktadha wa maisha ya utamaduni wa maisha ya jamii ihusikayo. Utamaduni wa jamii havitenganiki na lugha yake.

a) Ipe taarifa hii kichwa mwafaka. (alama1)
b) Eleza maana ya utamaduni. (alama2)
c) Eleza majukumu manne makuu ya lugha. ( alama4)
d) Kuja kwa serikali ya kikoloni kulileta mabadiliko gani nchini Kenya? (alama2)
e) Eleza majukumu ya lugha ya taifa nchini Kenya. (alama2)
f) Eleza msamiati ufuatano kama ulivyotumika katika taarifa. (alama4)
   i. haiyamkiniki

for free revision past papers visit www.freekcsepastpapers.com

ii. imekiuka mipaka
iii. ustaarabu
iv. kujiimarisha

2. **MUHTASARI**

**Soma makala yafuatayo kisha ujibu masuali yanayofuata**

Fasihi simulizi ndiyo fasihi ya awali na ambayo ni ya jadi. Binadamu alianza kuwasiliana kwa mdomo tangu siku alipozaliwa. Ingawa fasihi hii imeishi tangu zama hizo hadi leo,kuna watu wanaodhani kuwa huenda ikapotea. Wasiwasi wao unatokana na mabadiliko katika mazingiza yetu na piamaendeleo ya teknolojia ulimwenguni.

Chombo pekee cha mawasiliano katika fasihi simulizi kilikuwa ni mdomo lakini siku hizi inaandikwa. Maandishi yamegeuza ubo la fasihi hii. Uwanja huu umepungua kwani mengi ya mambo yaliyokuwa yakikaririwa na kupitishwa kutoka mtu mmoja hadi mwinginekwa mdomo hayapo. Mambo hayo yamerithiwa na kusomwa. Mabo yaliyokuwa yakihifadhiwa kwa kichwa sasa yamehifadhiwa kwa kalamu na karatasi.

Siku hizi kuna vinasa sauti. Ngano , methali, vitendawili na mambo yanayohusu fasihi simulizi yamerekodiwa na kuhifadhiwa.Watoto ambao walizoea kuketi karibu na moto huku wakisimuliwa ngano na bibi au babu, sasa wanategea redio. Ule uhalisia wa kukaa na kumwona mtambaji wa hadithi au mtegaji wa vitendawili umeanza kupotea. Mawasiliano mwafaka ya fasihi simulizi ni yale ya ana kwa anaambapo wasikilizaji ni washiriki kamili.

Maendeleo ya teknolojia yameiwezesha fasihi hii kuhifadhiwa kanda za pataninga (video) na sinema. Watazamaji wanaona matendo yakiigizwa kwenye runinga. Hali hii inamnyima mtazamaji uhuru wa kuuliza, kudadisi na kushiriki kikamilifu katika uigizaji na utendaji. Hivyo, kinyume cha inavyotarajiwa, mawasiliano hayawi ya moja kwa moja kutoka kwa msimulizi hadi kwa hadhira. Wasiwasi mkubwa wa watu ni kwamba fasihi simulizi ikapotea, hasa inapopoteza uhalisia wake.

Mbali na fasihi hii kutishwa na uvumbuzi wa teknolojia ya sasa, hadhira yenyewe imeathiriwa. Hadhira kubwa ya msimulizi ya kupokeza ujumbe wake ni watoto. Siku hizi watoto hawana muda wa kusikiliza hadithi au fasihi simulizi kutoka kwa wazee wao. Iwapo mwalimu hatatenga muda wa funzo la hili darasani, basi watoto watakosa muda wa kuwasiliana na wazee wao jioni hasa wakiwa wana kazi nyingi ya kuwafanya ya shuleni.

Wazazi wengine nao hawana muda wa kukutana na watoto wao, hasa mjini. Wao hutoka alfajiri kwa shughuli zao za kikazi na wengine kurudi jioni wakiwa wamechoka. Hivyo, wanakosa nafasi ya kuwasimulia au kuwasiliana na watoto wao. Huenda hali hii ikawa tofauti kule vijijini ambako pilkapilka za siku nyingi mno. Swali ni hili: Iwapo maendelezi ya fasihi simulizi ni mapokezi, je, itaendelezwaje wakati msimulizi hana muda wa kusimulia mpokezi? Au mpokezi hana wakati wa kusimulia?

for free revision past papers visit: www.freekcsepastpapers.com

**MASWALI**

a) Fupisha aya za kwanza tatu (maneno 90-100) (alama 9,1 ya mtiririko)
b) Eleza changamoto zinazoikumba fasihi simulizi kama zinavyojitokeza katika aya ya 4,5 na 6. (maneno 55-60) (alama 6,1 ya mtiririko)

3. **MATUMIZI YA LUGHA**

a) Eleza maana ya nomino. (alama1)
b) Tunga sentensi moja yenye nomino ambata na nomino dhahania (alama2)
c) Tunga sentensi ukitumia neno "tu" kama: (alama3)
  i) Kielezi
  ii) Kitenzi
  iii) kiwakilishi
d) Tambua vitenzi vilivyopigiwa mistari katika sentensi zifuatazo: (alama2)
  i) Mtoto yule <u>anasoma.</u>
  ii) Wewe <u>ulikuwa hujawahi kusoma</u> riwaya hiyo.
e) Unda vitenzi kutokana na nomino zifuatazo kisha uvitungie sentensi. (alama2)
  i) Sarufi
  ii) ukarimu
f) i) Eleza maana ya kishazi (alama1)
ii Taja njia tatu za kutambua kishazi tegemezi (alama3)
g) i) Ni nini maana ya ngeli? (alama1)
  ii) Huku ukitoa mfano mmojammoja wa nomino, onyesha miundo yoyote mitatu ya nomino katika ngeliya A-WA. (alama3)
h) i. Eleza dhana ya silabi. (alama1)
  ii. Onyesha miundo ya silabi katika maneno yafuatayo. (alama2)
    nchi
    ndwele
i) Tumia neno "lia" katika sentensi kama: (alama2)

i. Kishazi huru
ii. Kishazi tegemezi

i) Taja sifa tatu za konsomanti ifuatayo. /sh/ (alama3)

j) Weka mkazo katika mahali panafaa katika maneno yafuatayo (alama2)
muhtasari

karakana

k) Tana mifano minne ya sauti ambazo zinapotamkwa hewa nyingi hutokea katika chemba ya pua. (alama2)

l) Changanua sentensi ifuatayo kwa kutumia njia ya jedwali. (alama4)
Maria na Susa wanakula embe lililooza.

m) i. Ni nini maana ya shamirisho? (alama1)
ii. Tunga sentensi yenye shamirisho kitondo, kipozi na chagizo. (alama3)

n) Tunga sentensi moja inayobainisha maana ya vitate vifuatavyo
i. mdaa
ii. mtaa

**4. ISIMUJAMII**

a) Eleza sifa tano za sajili ya magazetini. (alama5)

b) Eleza mambo matano yaliyokosababisha Kiswahili kuteuliwa kama lugha ya taifa nchini Kenya. (alama5)

for free revision past papers visit: www.freekcsepastpapers.com

**COMPLIANT PREPARATORY EXAMINATION**
**102/3**
**KISWAHILI**
**KARATASI YA 3**
**FASIHI**

**SEHEMU YA A: USHAIRI (LAZIMA)**
**Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali yanayofuata**

Kama dau baharini, duniya inavyoyumba,
Limeshamiri tufani, kila mmoja lakumba,
Viumbe tu hali gani!

Duniya yatikishika, utahisi kana kwamba,
Vilima vyaporomoka, na kuvuruga nyumba,
Viumbe tu hali gani!

Tufani hilo la kusi, languruma na kutamba,
Linapuliza kwa kasi, hapana kisichoyumba,
Viumbe tu hali gani!

Mujiwe ni mkubwa sana, mfanowe kama nyumba,
Yazuka na kugongana, wala hatuna la kwamba,
Viumbe tu hali gani!

Mibuyu hata mivule, kama usufi na pamba,
Inarushwa vilevile, seuze hiyi migomba?
Viumbe tu hali gani!

Ni kipi kilotulia, tuwazeni na kudumba,
Mandovu kiangalia, yagongana na masimba,
Fisi wako hali gani!

Hata papa baharini, tufani limewakumba,
Walioko mikondoni, kila mmoja asamba,
Dagaa wa hali gani!

Mashehe wa mdaduwa, kwa ubani na uvumba,
Tufani hilo kwa kuwa, kusoze kwake kutamba,
Itokee afueni!

for free revision past papers visit: www.freekcsepastpapers.com

**Maswali**

a) Eleza bahari ya shairi hili huku ukiegemea kwenye vigezo vifuatavyo: (alama4)
   i. Kiishio
   ii. Mishororo

b) Fafanua tamathali moja ya usemi iliyotumiwa katika shairi hili. (alama2)

c) Eleza mbinu tatu za uhuru wa mshairi kama zinavyojitokeza katika shairi. (alama6)

d) Ekeza muundo wa shailri hili. (alama5)

e) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumiwa katika shairi hili (alama3)
   i. asamba
   ii. Kutamba
   iii. kwamba

**SEHEMU YA B: *MSTAHIKI MEYA***

2) "Siku zote tumeshudia wasiotosheka wakipuliza tarumbeta zao za uzushi na sisi tukizizima kwa kukohoa tu."
   a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama4)
   b) Fafanua mbinu ya lugha inayojitokeza katika dondoo hili. (alama2)
   c) Eleza maudhui yaliyoangaziwa katika dondoo hili. (alama2)
   d) Wanaorejelea walipulizaje tarumbeta zao za uzushi katika mji wa Cheneo? Fafanua njia zozote tatu. (alama6)
   e) Eleza sifa zozote tatu za msemaji katika dondoo hili. (alama6)

**AU**

3) Fafanua suala la usaliti kama linavyojitokeza katika tamthilia ya *Mstahiki Meya*. (alama20)

**SEHEMU YA C: *KIDAGAA KIMEMWOZEA***

4) " Naona unakula njama na mwanao kunila ningali hai."

a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama4)

b) "Mwana" anayejelewa alifanya nini kilichompelekea msemaji kudai kuwa wanapanga kumla angali hai? (alama2)

c) Eleza tamathali mbili za usemi zinazojitokeza katika dondoo hili. (alama4)

d) Huku ukimrejelea msemewa katika dondoo hili, fafanua tatizo la mwanamke katika jamii. (alama10)

**AU**

5) Suala la kutowajibika ni tatizo sugu linaloikumba jamii. Thibitisha ukweli wa kauli hii ukirejelea *Kidagaa Kimemwozea*. (alama20)

**SEHEMU YA D: DAMU NYEUSI NA HADITHI NYINGINE**

**MASIKINI, BABU YANGU!**

6) "Kila mara aliposema na mama na baba alitaja maneno kama uhuru, ukabila, ufisadi, hongo…"

a) Elea muktadha wa dondoo hili. (alama4)

b) Eleza sifa zozote tatu za mrejelewa katika dondoo hili. (alama6)

c) Eleza hatma ya mrejelewa katika dondoo hili. (alama2)

d) Ukabila una madhara chungu nzima. Eleza yoyote manne huku ukirejelea hadithi husika. (alama8)

**AU**

7) Huku ukirejelea hadithi za: *Kanda la Usufi*, *Tazamana na Mauti*, *Mwana na Darubini* na *Samaki wa Nchi za Joto*, fafanua changamoto zinazowakumba vijana katika jamii. (alama20)

**SEHEMU YA C: FASIHI SIMULIZI**

8)

a) Eleza mambo matatu yanayoifanya fasihi kuitwa sanaa. (alama6)

b) Ni kwa njia gani fasihi simulizi huwa kuwa hai kuliko fasihi andishi? (alama6)

c) Eleza sifa zozote nne zinazozibainisha ngano. (alama4)

d) Taja majina ya fanani wa vipera vifuatavyo vya fasihi simulizi. (alama4)

i) Ngano
ii) Mawaidha
iii) Maghani
iv) ulumbi

for free revision past papers visit: www.freekcsepastpapers.com

**NYERI CENTRAL**
**102/1**
**KISWAHILI**
**INSHA**
**KARATASI YA KWANZA**

1. Umeteuliwa kumtambulisha kiongozi anayeweza kupatiwa tuzo ya kuwa kiongozi bora nchini mwako. Andika wasifu wa kiongozi huyo.
2. Pendekeza njia zinazoweza kutumiwa ili kuimarisha elimu ya mototo wa kike chini.
3. Baada ya dhiki faraja.
4. Andika insha inayomalizikia kwa maneno haya: …Kimya kilitanda chumbani. Mgonjwa aligaragara kitandani kisha akaniita kwa sauti hafifu. Nilimsogelea kwa hofu na masikitiko, halafu akapepesa macho yake na kunyooka.

**NYERI CENTRAL**
**102/2**
**KISWAHILI**
**(LUGHA)**
**KARATASI YA PILI**
**MUDA: SAA 2 ½**

**UFAHAMU (Alama 15)**

Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.

Zaraa ndio uti wa mgongo wa taifa la Kenya. Viwanda vingi ncnini hutegemea kilimo kama malighafi yake na kuwalisha wafanyakazi. Licha ya umuhimu wa sekta hii, mkulima ambaye ndiye nguzo za zaraa anaendelea kukabiliwa na matatizo mbalimbali yanavokwamiza juhudi zake.

Mojawapo ya matatizo yanayomkabili mkulima ni ukosefu wa ushauri wa zaraa. Wataalamu wanaotarajiwa kumshauri |i mkulima kuhusu njia bora za kuzalisha na kuongeza pato lake ni haba ikilinganishwa na idadi ya wakulima wanaohitaji ' ushauri. Wachache walioko nao wanakwamizwa na mambo tofauti. Mathalani, utawapata hawaendi nyanjani ili kukutana na I wakulima kwa kuwa hawana usafiri. Iwapo usafiri upo, huenda petroli ikawa ni kizungumkuti. Halikadhalika, usisahau kuwa baadhi ya wataalamu hawa ni walazadamu au mafisadi. Kuna wale wanaofika ofisini na kushinda siku nzima wakisonia gazeti huku wakijaza miraba, wakicheza bao au karata. Kuna wale nao ambao hufika ofisini wakaangika koti au sweta kitini ili waonekane kuwa bado wapo na kisha kutokomea kwenda kushughulikia mambo yao ya kibinafsi yasiyohusu ndewe wala sikio kazi waliyoajiriwa kuifanya.

Ukosefu wa sera mwafaka kuhusu ardhi nalo ni tatizo jingine linalotatiza kilimo nchini. Serikali haijaweka sera mahususi kuhusu matumizi ya ardhi. Wananchi wengi huongozwa na taratibu za utamaduni wa nasaba zao. Taratibu hizi hupendekeza ugawaji wa ardhi kwa minajili ya urithi kulingana na warithi waliopo. Si ajabu kuwa kote nchini, ardhi inayofaa kwa kilimo imekatwakatwa vipande vidogo vidogo ambavyo haviwezi kuwa na faida kwa zaraa.

Kushindwa kwa mkulima kuongeza virutubishi ardhini ni changamoto nyingine inayokabili kilimo nchini. Ulimaji wa kile kipande cha ardhi mwaka nenda mwaka rudi, bila kukipa nafasi ya kukipumzisha, huufanya mchanga kupoteza virutubishi muhimu vinavyohitajiwa na mimea. Hili nalo huchangia kupunguza uzalishaji wa mazao. Ili kutatua tatizo hili, wakulima wengi hukimbilia mbolea za kisasa ambazo badala ya kumsaidia, humwongezea madhila. Mbolea hizi zinatambulikana kuchangia uchafuzi wa mchanga na ardhi.

Mabadiliko ya hali ya anga nayo huongeza msururu wa madhila ya mkulima. Mabadiliko haya yamemfanya mkulima kushindwa kupanga wakati anaotakiwa kutayarisha shamba, kupanda, kupalilia, kunyunyizia dawa na kadhalika. Mvua imekuwa adimu. Badala yake panakuwa na vipindi virefu vya kiangazi ambavyo huathiri bidii za mkulima. Maji nayo yanaendelea kupungua na wakulima wengi hawawezi kukimu mahitaji ya unyunyizaji maji mashambani.

(a) Andika anwani inayofaa kifungu hiki. (alama 1)
(b) Huku ukirejelea kifungu, fafanua umuhimu wa kilimo hapa nchini. (alama 2)
(c) Eleza changamoto tatu zinazowakabili wataalamu wa kilimo (alama 3)
(d) Mbali na matatizo yanayowakumba wataalamu onyesha matatizo mengine matatu yanayokumba sekta ya zaraa. (alama 6)
(e) Eleza maana za msamiati ufuatao kulingana na taarifa. (alama 3)
(i) Yanayokwamiza
(ii) Sera
(iii) adimu

for free revision past papers visit: www.freekcsepastpapers.com

**Ufupisho (Alama 15)**

**Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.**

Aibu kubwa ya taifa kushindwa kukabiliana na tatizo sugu la ajali za barabarani bado inaendelea kuwafedhehesha wahusika katika sekta ya uchukuzi na mawasiliano licha ya matumizi ya vidhibiti mwendo na kanda za usalama.

Ajali za barabarani zinaangamiza idadi kubwa ya watu kila mwaka wakiwemo viongozi na watu mashuhuri. Miongoni mwa sababu ambazo zinaleta maafa barabarani pamoja na uendeshaji kasi kupita inavyotakikana, yaani kukiuka masharti yaliyowekwa na wizara ya Uchukuzi na Mawasiliano. Madereva wengi hung'oa vidhibiti mwendo vilivyowekwa, hawarekebishi mikanda ya usalama, wala hawayapeleki magari yao kukaguliwa mara kwa mara kama inavyopaswa. Yale yanayopelekwa kwa ukaguzi, mengi hushindwa kutekeleza kanuni zilizoweka kwa hivyo hutegemea hongo kuwa barabarani. Fauka ya hayo, madereva wa malori na matrela mara nyingi huendesha magari hayo wakiwa walevi. Dawa za kulevya kam[a] miraa na bangi hutumiwa sana na hawa na matokeo yake huwa ajali mbaya.

Hata hivyo, lawama haiwezi kuelekezewa madereva pekee. Ukiangazia barabara nchini Kenya utapata kuwa barabara hazik" katika hali nzuri. Zile za lami zimekuwa na mashimo makubwa ambapo mvua ikinyesha hufanya vidimbwi mithili *f* michimbo ya madini yaliyojaa maji baada ya kuachwa wazi. Na zile barabara zisizokuwa na lami zimeharibika kiasi kwamba ni vigumu kuzitofautisha na njia za ng'ombe kvvenye maeneo kame. Kinachohitajika ni kuzirudisha katika kiwango ambacho zinaweza kufaa tena.

Wananchi pia inafaa waelimishwe ili wasikubali kupanda magari ambayo tayari yamejaa. Hili litawasaidia wananchi j wenyewe kudumisha usalama wao barabarani. Pia inawafaa watambue ya kwamba wana jukumu la kuwaarifu walinda usalama endapo dereva anaendesha kwa kasi kuliko ile ya kilomita themanini kwa saa liiyokubaliwa. Inafahamika kuwa maafia wa usalama ndio wafisadi zaidi, hivyo basi huchangia katika kuongeza idadi ya vifo barabarani. Katika vita vya ufisadi na ajali za barabarani ni mwanachi mwenyewe ambaye atawezesha kukomesha hali hii. Kwa mfano, afisa wa usalama akipatikana akichukua hongo, yeye pamoja na yule aliyetoa hongo walcamatwe na kupelekwa kwenye vituo vya kukabiliana na ufisadi na kuchukuliwa hatua kali, matatizo haya yataisha. Lakini kabla kufikia hapo, ni muhimu kumhamasisha mwananchi kuhusu haki zake na namna ya kukabiliana na suala hili la ufisadi. Hali hii inatuonyesha kwamba mipango maalum inapaswa kufanywa na serikali ili kuwaelimisha wananchi kama hatua ya kwanza kukabiliana na ufisadi, hatimaye izilainishe sekta zote wala si ya uchukuzi na mawasiliano pekee.

for free revision past papers visit: www.freekcsepastpapers.com

(a) Kwa kurejelea aya ya pili na ya tatu, eleza mambo yanayochangia ajali za barabarani. (Maneno 45-50) (alama 6, 1 ya mtiririko)

(b) Fupisha ujumbe wa aya ya mwisho. (maneno 50-55) (Alama 6, 2 za mtiririko)

**MATUMIZI YA LUGHA (Alama 40)**

a.) Tofautisha kati ya irabu /e/ na /o/. (Alama 2 )

b.) Onyesha viambishi katika sentensi hii : (Alama 3)
Alivyoikimbia

c.) Tambua aina ya vivumishi katika sentensi hizi : (Alama 3)
- i) Msichana mrembo alituzwa zawadi.
- ii) Daktari kijana amehamishwa.
- iii) Mwalimu wetu hatushauri vizuri.

d.) Kanusha sentensi hii : (Alama 2)
Akinishinda masomoni nitamlipa.

e.) Tumia kiambishi : 'ku' katika sentensi mbili tofauti. (Alama 2).

f.) Yakinisha.
Mgonjwa huyo hakula wala kunywa. (Alama 2)

g.) Andika kwa wingi ukubwa. (Alama 2)
Mtu huyo aliangushwa na ng'ombe wake.

h.) Changanua kwa matawi sentensi hii. (Alama 4)
Aliyetujengea nyumba ameenda Marekani.

i.) Onyesha shamirisho. (Alama 3)
Mama alimjengea nyanya nyumba kwa mbao.

j.) Weka nomino hizi katika ngeli zake. (Alama 1)
- i) Mbalungi
- ii) Mturuki.

k.) Akifisha. (Alama 3)
Juma Maria ulimwona Farida Maria la hukuwepo.

l.) Tumia kiashiria kisisitizi cha karibu katika sentensi hii. (Alama 2)
Kijiko kile kilitumiwa jana.

m.) Unda nomino kutokana na : (Alama 2)
- i) Tepetevu
- ii) Oza

n.) Nyambua vitenzi hivi katika kauli ya fanyishi. (Alama 3)

i) –fa
ii) –la
iii) –ja

o.) Eleza matumizi mawili ya mshazari. (Alama 1)

p.) Tunga sentensi iliyo na kishazi huru na kishazi tegemezi. (Alama 2)

q.) Andika kinyume cha : (Alama 1)
Mtoto msichana alimeza dawa.

r.) Andika katika msemo wa taarifa : (Alama 2)
''Tutakuja kwenu leo.'' Mama alisema.

**ISIMU JAMII (Alama 10)**

a) Eleza nadharia tatu kuhusu chimbuko la lugha ya Kiswahili. (Alama 6)

b) Taja matatizo yanayokumba ukuaji wa lugha ya Kiswahili nchini Kenya. (Alama 4)

for free revision past papers visit: www.freekcsepastpapers.com

**NYERI CENTRAL**
**102/3**
**KISWAHILI**
**KARATASI YA TATU**
**KIDATO CHA NNE**
**(FASIHI)**
**SEHEMU A : TAMTHILIA : MSTAHIKI MEYA**

**1. Swali la Lazima**

''Inatosha kumkunja kila aliye chini yake kama ua la wakati wa alasiri.''

a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (Alama 4)
b) Onyesha tamathali ya usemi iliyotumiwa. (Alama 2)
c) Kwa kurejelea tamthilia nzima, eleza mbinu za kiutawala zilizotumiwa kutawalia Cheneo. (Alama 10).
d) Eleza sifa nne za mzungumzaji. (Alama 4).

**SEHEMU B : RIWAYA: KIDAGAA KIMEMWOZEA**

**2.** ''Tembo itakuua ndugu yangu, punguza ulevi bwana. Siku hizi naona aibu kukuita ndugu yangu.''

a) Fafanua muktadha wa dondoo hili. (Alama 4)
b) Wahusika hawa wawili ni kama shilingi kwa ya pili. Jadili. (Alama 16)

**3.** Kwa kurejelea riwaya ya Kidagaa Kimemwozea, onyesha jinsi sheria zilivyokiukwa katika nchi ya Tomoko. (Alama 20)

**SEHEMU C : HADITHI FUPI: DAMU NYEUSI NA HADITHI NYINGINE**

**4.** Fafanua mabadiliko ambayo mwandishi angetaka yafanywe ili ubaguzi ukomeshwe kabisa katika hadithi ya Damu Nyeusi. (Alama 20).

**5.** ''Mwalimu nina swali ambalo ningetaka unijibu. Je, ni kwa nini sisi huwaleta watoto shuleni?

a) Yaweke maneno haya katika muktadha wake. (Alama 4)
b) Eleza hulka za wazungumzaji. (Alama 8)
c) Fafanua maudhui yanayohusiana na dondoo hili. (Alama 8)

for free revision past papers visit: www.freekcsepastpapers.com

**SEHEMU D : USHAIRI**

**6. SHAIRI 1**

Jicho, tavumiliaje, kwa haya uyaonayo? Jicho, utasubirije, maonevu yapitayo? Kiwacho, lijalo na lije, nimechoka vumiliya Naandika!

Moyo, unao timbuko, maudhui tusikiayo Nayo, visa mauko, wanyonge yawakutayo Kwayo, sina zuiliko, natoa niyahisiyo Naandika!

Hawa, wanatulimiya, Dhiki wavumiliayo Hawa, mamiya, na mali wazalishayo Hawa, ndo mamiya, na maafa waikutayo Naandika!

Hawa, sioni wengine, kwao liko angamiyo Hawa, huwapa unene, kwao liko angamiyo Hawa, bado ni wavune, kwa shida waikutayo Naandika!

Bado, wawapo mabwana, wenye pupa na kamiyo Bado, tofauti sana, kwa pato na mengineyo Bado, tuling'owe shina, kwa shida waikutayo Naandika!

Maswali

(a) Pendekeza anwani kwa shairi hili. (alama 2)
(b) Eleza umbo la shairi hili. (alama 4)
(c) Fafanua ujumbe wa ubeti wa kwanza kwa lugha tutumbi. (alama 4)
(d) Tambua nafsi-nenewa na sababu ya kunenewa? (alama 2)
(e) Kwa kutoa mifano eleza jinsi idhini ya utunzi ilivyotumika katikashairi hili. (alama 2)
(f) Ainisha bahari mbili zinazoafiki utungo huu na sababu za uamuziwako. (alama 4)
(g) Eleza maana ya msamiati ufuatao kama ulivyotumika katika shairi. (alama 2)
    (i) Timbuko
    (ii) Ndo mamiya

7. **SHAIRI 2:**

**Maendeleo ya Umma**

1. Maendeleo ya umma
Sio vitu maghalani
Kama tele vimesaki
Lakini havishikiki
Ama havikamatiki
Ni kama jinga la moto
Bei juu

2. Maendeleo ya umma
Sio vitu gulioni
Kuviona madukani
Kuvishika mikononi
Na huku wavitamani
Kama tama ya fisi
Kuvipata ng'o

3. Maendeleo ya umma
Sio vitu shubakani
Dhiki ni kwa mafakiri
Nafuu kwa matajiri
Ni wao tu washitiri
Huo ni ustiimari
Lo! Warudia

4. Maendeleo ya umma
Ni vitu kumilikiwa
Na wanyonge kupatiwa
Kwa bei kuzingatiwa
Bila ya kudhulumiwa
Na hata kuhadaiwa
Hiyo ni haki

5. Maendeleo ya umma
Dola kudhibiti vitu
Vijapo nchini mwetu
Na kuwauzia watu
Toka nguo na sapatu
Pasibakishiwe na kitu
Huo usawa

6. Maendeleo ya umma
Watu kuwa na kauli
Katika zao shughuli
Vikaoni kujadili
Na mwisho kuyakubali
Maamuzi halali
Udikteta la

7. Maendeleo ya umma
Watu kuwa waungwana
Vijakazi na watwana
Nchini kuwa hakuna
Wote kuheshimiana
Wazee hata vijana

for free revision past papers visit: www.freekcsepastpapers.com

**Maswali**

(a) Shairi hili ni la aina gani? Toa sababu zako. (alama 2)
(b) Eleza dhamira ya mwandishi kuandika shairi hili. (alama 3)
(c) Toa mifano mitatu ya urudiaji katika shairi hili. Je urudiaji huu una kazi/majukumu gani? (alama 6)
(d) Onyesha matumizi mawili ya tamathali za usemi katika shairi hili. (alama 4)
(e) Eleza toni ya mashairi. Toa sababu. (alama 1)
(f) Nafsi neni ni nani? (alama 1)
(g) Toa mfano mmoja wa taswira katika shairi hili. Je, taswira hiyo inajengwa na nini? (alama 3)

**8. SEHEMU E : FASIHI SIMULIZI**

a) Eleza maana ya miviga. (Alama 2)
b) Fafanua umuhimu wa miviga kwa wanajamii. (Alama 4)
c) Eleza maana ya ulumbi. (Alama 2)
d) Fafanua umuhimu wa ulumbi katika jamii. (Alama 3)
e) Eleza sifa za mlumbi mahiri. (Alama 4)
f) Eleza maana ya ngomezi. (Alama 2)
g) Toa mifano mitatu ya ngomezi za kisasa. (Alama 3)

for free revision past papers visit: www.freekcsepastpapers.com

**KASSU**
**102/1**
**KISWAHILI**
**2017**
**KARATASI Y A 1**
**INSHA**

1. Wewe ukiwa mwenyekiti wa chama cha msalaba mwekundu shuleni mwako, umemtembelea afisa mshirikishi wa usambazaji msaada wa chakula katika gatuzi lako. Andika mahojiano baina yenu kuhusu changamoto zinazokumba usambazaji huo.
2. Pendekeza hatua zinazofaa kuchukuliwa ili kuimarisha utalii kama kitega uchumi nchini.
3. Andika kisa kinachoafiki ukweli wa methali hii: Achanikaye kwenye mpini hafi njaa.
4. Andika insha itakayoanza kwa:
   "Nilipotazama gazeti la "Tangaza leo," anwani ilinikodolea macho: Shule nyingi zakoza matokeo ya mtihani wa kitaifa KCSE.

**KASSU**
**102/2**
**KISWAHILI**
**2017**
**Karatasi ya 2**
**Muda: Saa 2½**

**UFAHAMU**

*Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali.*

Mchezo wa kandanda umenifunza jambo moja: mashabiki ndio wachezaji bora sana. Wao hawakosei kufunga bao au "kuhata" penalti wanavyosema magwiji wa mchezo huu wenyewe. Mchezaji akiukosea mpira, mashabiki hunung'unika na kupiga yowe. Katika hilo yowe, huwa kumebebwa makombora mengi. Yapo ya matusi, yapo ya "mwondoeni nje ya uwanja" yapo ya "kocha lazima aende," na yapo ya "asipewe nambari tena" wajua tena kandanda!

Tunaweza kutumia kandanda kujifunza mengi mengine maishani. Kwa mfano, juu ya sheria na haki za watu. Hebu fikiria, mashabiki kufanya yowe hata timu ikashinda kombe! Au hata kufanya yowe hata mchezaji akabadilishwa na wengine bora wakaletwa uwanjani? Isitoshe, shabiki ambaye ni mfalme wa uwanja, yowe lake linaweza hata kumfanya kocha wa kilabu maarufu duniani kama Manchester United au Arsenal au Real Madrid kuondoka! Mbona hatufanyi hivyo dhidi ya sheria zinazovuruga maisha ya ndugu zetu?

Mbona hatupigi yowe dhidi ya ubakaji? Wapi yowe mwanamke anapopigwa na mumewe hadi kufa? Wapi yowe mtoto wa kike anaponyimwa urithi kwa sababu ya sheria potovu za kitamaduni? Wapi yowe dhidi ya wizi wa kimabavu?

Watoto wetu leo hawawezi kutembea peke yao haswa magharibi yanapoingia. Je, hatuwajui watu wanapowahatarisha wana wetu? Tunafanya kitu gani? Mbona hatupigi yowe polisi au utawala ukasikia ili hatua ichukuliwe?

Si kitambo tuliposikia kuhusu biashara ya ngozi ya binadamu kuuzwa ghali sana, hasa katika nchi jirani ili waganga watengenezee dawa za kuwapumbazia waja. Huu ni uchawi na kilele cha ushetani. Katika nchi jirani juzijuzi, walishikwa watu wawili ambao walikuwa wamechinja mtoto wa kiume na kumchuma ngozi kwa ushirikiano na mpumbao mkubwa. Yaani tumeuza za wanyama zikatushinda, sasa tunauza za watu?

Tatizo kubwa ni kwamba watu wanaofanya biashara haramu tunawajua. Je, tunachukua hatua gani? Haijalishi wanavaa nguo gani, za fisi au za mwanakondoo! Tunahitaji kuwaweka wazi ili biashara zao zijulikane. Wawe weusi au manjano, weupe au kijani, sharti weupe uwepo kuondoa hofu na taharuki kwa ajili ya kila mwanajamii.

Hatua ya kwanza itakuwa ya kugeuza sera na mtazamo wa vikosi vyetu vya usalama kuhusu upokeaji wa habari kutoka kwa umma. Endapo hawatasita kufichua wanaowapa habari , watajikuta katika hatari ya kuonwa na raia kama wapinga amani na lazima wachukue lawama kwa uongezekaji wa uhalifu nchini. Kwa wazalendo hata hivyo, yowe ni silaha yetu.

for free revision past papers visit: www.freekcsepastpapers.com

**Maswali**

a) Yape makala haya kichwa mwafaka. (alama 1)
b) Mchezo wa kandanda una mchango gani? (alama 2)
c) Ni matatizo gani ambayo mwandishi anailaumu jamii kwayo? (alama 4)
d) Lawama kubwa inaegemea kina nani? Taja mawili. (alama 2)
e) Ni nini maana ya mistari ifuatayo? (alama 2)
   i) Haijalishi wanavaa nguo gani, za fisi au mwanakondoo!
   ii) "…sharti uwepo ili kuondoa hofu na taharuki…"
f) Ni hatua gani muhimu zinazofaa kuchukuliwa dhidi ya waovu waliotajwa? (alama 2)
g) Taja mbinu zozote mbili za lugha zilizotumiwa na mwandishi. (alama 2)

**UFUPISHO** (Alama 15)

*Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali yanayofuata*.

Kuna haja ya serikali ya Kenya kuwa na sera mwafaka ya ukuzaji wa Kiswahili, ili kiweze kukabiliana na maendeleo ya teknolojia. Jambo hili limepuuzwa siku nyingi. Ni vyema ifahamike kwamba umilisi wa lugha unawezesha mawasiliano yenye ufanisi kwa sababu mwasiliniaji anaweza kujieleza kwa ufasaha. Kwa jinsi anaweza kuhusiana na hadhira vizuri na kufanikisha mawasiliano yaliyo na tija katika maendeleo.

Ingawa kwa sasa Kiswahili kinatumika katika nyanja mbalimbali za maendeleo sehemu za mashambani, ufanisi mkubwa zaidi utapatikana ikiwa Kiswahili kitapewa uzito zaidi kupitia michezo ya kuigiza, hadithi na sarakasi zilizo na dhamira ya maendeleo. Mtindo huu unapendelewa sana na shirika la umoja wa mataifa linaloshughulika na maswala ya idadi ya watu katika kuhamasisha umma kupanga uzazi na kupunguza idadi ya watu. Iwapo mtindo huu utatumiwa na watalamu wanaowahamasisha wananchi kuhusiana na maswala ya maendeleo huku lugha ya Kiswahili ikitumiwa bila shaka lugha hii itakuwa na nafasi kubwa ya kufanikisha maendeleo.

Kuna haja ya kutumia Kiswahili katika vyombo vyote vya habari kama redio, majarida na hata kanda za video kusambaza habari zinazohusiana na maendeleo. Kwa sasa idhaa za redio ndizo hutumia Kiswahili kwa wingi ilhali runinga zinatumia lugha hii kwa kiasi tu. Lugha ya Kiswahili haijatumika kuandika majarida ya kilimo, afya au uchumi ilhali Kiingereza ndicho kilichotawala katika uwanja huu. Matokeo ya mwelekeo huu ni kwamba idadi kubwa ya watu wasio na elimu katika sekta zote za maendeo hawaelewi mambo mengi ambayo yangewafaa kujiendeleza kwa vile Kiingereza hakieleweki kwao.

Vilevile kuna haja ya kutafsiri matokeo ya tafiti mbalimbali zinazofanyika nchini Kenya na kwingineko kwa lugha ya Kiswahili ili maarifa ya tafiti hizo ziwafikie walio wengi na wanaoelewa Kiswahili. Hili likifanyika tafsiri hizi zinapaswa kuwekwa katika sehemu maalum za maktaba za kitaifa na vituo vya kijamii vinavyowahamasisha wananchi kuhusu maswala ya maendeleo. Kwa jinsi hii, maarifa mapya yatawafikia Wakenya wengi. Maarifa tunayoyazungumzia hapa ni pamoja na yale yanayopakuliwa kutoka kwenye tovuti. Katika mustakabali huu, mradi wa kampuni ya Mikrosoft wa kufikisha teknolojia ya mawasiliano hasa kwa tovuti sehemu za mashambani hauna budi kuigwa na kuungwa mkono na serikali ya Kenya. Iwapo utafanikiwa, utawezesha watu ambao wana elimu kupakua maarifa hasa maafisa wanaohamasisha maendeleo, na kuyaeneza kwa watu wengine kwa kutumia Kiswahili.

Hata hivyo, hakuna utafiti ambao umefanywa kuchunguza uenezaji wa Kiswahili na matumizi yake hasa katika maeneo ya mashambani. Wataalamu wa lugha ya Kiswahili wana jukumu la kufanya hivi ili kupendekeza hatua za kufanikisha lugha hii.

**Maswali**

(a) Fupisha aya tatu za mwanzo kwa maneno 90 – 100 (alama 8, 1 ya mtiririko)

(b) Eleza mambo muhimu yanayojitokeza katika aya ya nne. (Maneno 40 – 50) (alama 5, 1 ya mtiririko)

**MATUMIZI YA LUGHA**

(a) Tumia neno Kamene kama yambiwa katika sentensi. (alama 2)

(b) Taja misingi ya upangaji wa irabi za Kiswahili. (alama 3)

(c) Huku ukitoa mfano mmoja, eleza maana ya mofimu ya kimsamiati. (alama 2)

(d) Vitambue vijenzi vya kimsingi vya lugha ya Kiswahili. (alama 2)

(e) (i) Eleza maana ya kishazi. (alama 1)

(ii) Tunga sentensi moja yenye kishazi tegemezi kinachovumisha. (alama 2)

(f) Badilisha kitenzi kisaidizi kilicho kwenye sentensi ifuatayo kiwe kishirikishi. (alama 2)

Mvule alikuwa akilala bweni ni.

(g) Taja majukumu ya vipengele vilivyopigwa kijistari. (alama 4)

Nanyi nendeni haraka au muadhibiwe kinyama kwa utundu wenu.

(h) Andika sentensi ifuatayo katika ukubwa. (alama 2)

Uteo alionunuliwa umezeeka sana.

(i) Tunga sentensi moja mwafaka kudhihirisha matumizi ya kiunganishi madhali. (alama 2)

(j) Onyesha minyambuliko ya maneno yafuatayo katika kauli zilizotolewa mabanoni. (alama 2)

(i) ja (tendewa) …………………………………………………………………………………

(ii) cha (tendeka) …………………………………………………………………………………

(k) Katika sentensi moja, onyesha matumizi mawili ya kibainishi. (alama 2)

(l) Yakinishi (alama 2)

Usipolipa usiingie ndani

(m) Neno 'gofu' linapatikana katika ngeli gani? (alama 1)

(n) Geuza sentensi ifuatayo iwe katika usemi halisi. (alama 2)

Kassim alimwomba Hirshi aende mahali alipokuwa ili amtume.

(o) Changanua sentensi ifuatayo kwa kutumia kielelezo matawi. (alama 4)

Japo Mutiso anasinzia darasani hajamaliza kazi yake.

(p) Iandike upya sentensi ifuatayo kwa kutumia visawe vya maneno yaliyo katika italiki. (alama 3)

*Mdarisi* aliwashauri wanafunzi kuwa *bidii* huzaa *ufanisi*

(q) Unda kitenzi kutokana na kivumishi jasiri. (alama1)

(r) Andika maana ya nahau: kunjua jamvi (alama 1)

**ISIMUJAMII** (Alama 10)

Eleza sifa tano za kimsingi zinazotambulisha sajili ya siasa. (alama 10)

for free revision past papers visit: www.freekcsepastpapers.com

**KASSU**
**102/3**
**KISWAHILI**
**2017**
**Karatasi ya 3**
**FASIHI**
**Muda: Saa 2 ¾**

**SEHEMU A: USHAIRI**
**LAZIMA (alama 20)**

**1.** Soma shairi hili kisha ujibu maswali yafuatayo. (alama 20)

Nikumbuke mwanangu,
Kila asubuhi unapoamka,
Kwenda kazini,
Unapochukua sabuni ya kunukia,
Na dodoki jororo

Na kopo la koligeti,
Kwenda kukoga hamamuni,
Penye maji ya bomba,
Yaliyochunjwa na kutakaswa,
Mororo…

Kumbuka nyakati zile,
Za staftahi ya sima na mtama,
Ndizi na nagwa,
Kwa mchicha na kisamvu,
Na ulipokwenda choo,
Ulilia kwa uchungu,

Nikumbuke,
Unapotoka nyumbani asubuhi maridadi,
Katika suti ya moto,
Miwani ya pembe,
Viatu vya Paris,
Saa ya dhahabu,
Unapong'oka kwenda kazini,
Katika Volvo,
Katika njia iliyosakafiwa.

Kumbuka,
Nyakati zile,
Mimi ni mamako,
Tulivyojidamka,
Mara tu kwale wa kwanza,
Alipoanza kukoroma,
Jogoo wa kwanza hajawika,
Mimi nikachukua mundu na panga,
Mamako jembe na shoka,
Tukaelekea porini,
Kufyeka na kuchimbua,
Na hubaki wajiandaa kwenda shule..
Nikumbuke,
Saa za jioni,
Unapovalia kitanashati

Maswali

a) Thibitisha kuwa utungo huu ni shairi (alama 4)
b) Fafanua toni ya utungo huu (alama 2)
c) Huku ukitoa mifano, linganua kati ya mistari toshelezi na mistari mishata (alama 4)
d) Eleza maudhui yoyote matatu yanayojitokeza (alama 6)
e) Eleza sifa zozote mbili za nafsi nenewa (alama 4)

for free revision past papers visit: www.freekcsepastpapers.com

**SEHEMU B: RIWAYA**

**Kidagaa kimemwozea (alama 20)**

**2**.…Walimpiga kituku kama nyoka.Nikumbukapo naona fundo chungu moyoni…

(a) Eleza muktadha wa dondoo (alama 4)

(b) Taja mbinu mbili za lugha katika dondoo hili (alama 2)

(c) Kwa kurejelea dondoo hili fafanua maudhui yanayojitokeza (alama 2)

(d) Fafanua maudhui uliyotaja hapo juu (c) kwa kutoa mifano kwa riwaya nzima (alama 12)

Au

**3**. Fafanua mbinu hizi kama zinavyojitokeza katika riwaya. (alama 20)

(a) Barua

(b) Kinaya

(c) Sadfa

(d) Mbinu rejeshi

(e) Majazi

**SEHEMU C : TAMTHILIA**

**TAMTHILIA YA MSTAHIKI MEYA**

**(Timothy Arege)**

**4**. "Najua ni kazi ila usisahau pia kwamba wafanyikazi wamegoma."

(i) Fafanua muktadha wa dondoo hili. (alama 4)

(ii) Wahusika wawili wanaohusishwa na dondoo hili wamebaidika kama ardhi na `mbingu. Thibitisha. (alama 16)

Au

**5**. (b) "Unaona sasa?Mlinidanganya."Kauli hii ni idhibati tosha kuwa,Mstahiki Meya alidanganyika na kuongozwa na falsafa zisizo na mashiko katika uongozi wake.Tetea ukweli huu. (alama 20)

for free revision past papers visit: www.freekcsepastpapers.com

**SEHEMU D: HADITHI FUPI**

**Damu Nyeusi na hadithi nyingine (alama 20)**

**6**. "Mara walianza ama kuniashiria kidole au kutuashiria..Macho wameyakodoa kwa tuhuma.Walisemezana kwa Mizengwe."

(a) Weka dondoo hili katika muktadha wake. (alama 4)

(b) Eleza kwa tafsili yaliyotokea baada ya dondoo hili. (alama 4)

(c) Kwa kurejelea hadithi hii,eleza masuala makuu yanayoibuka katika kisa hiki. (alama 12)

Au

7.

(a) Jadili ufaafu wa anwani " **Shaka ya Mambo**". (alama 10)

(b) Fafanua jazanda ya **Kikaza** kwa mujibu wa hadithi husika. (alama 10)

**SEHEMU E: FASIHI SIMULIZI**

**FASIHI SIMULIZI (alama 20)**

**8**. (a) Linganisha fasihi simulizi na fasihi andishi. (alama 5)

(b) Taja asili ya lakabu. (alama 5)

(c) Fafanua sifa tano za maghani. (alama 5)

(d) Mtafiti huenda akapatwa na changamoto nyanjani, fafanua. (alama 5)

**KANGEMA/MATHIOYA**
**102/1**
**KISWAHILI**
**LARATASI YA 1**
**INSHA**

1. **LAZIMA**
   Wewe ni katibu wa Kamati iliyoteuliwa kujadili changamoto zinazowakabili vijana.
   Andika kumbukumbu za mkutano wenu.
2. Tatizo la njaa nchini ni msiba wa kujitakia. Jadili.
3. Tunga kisa kinachodhihirisha maana ya methali ifuatayo: Tamaa mbele mauti nyuma.
4. Andika insha inayoanza kwa:
   "Umeletwa hapa na wasamaria wema." Sauti ya kike ikanieleza. Nikavuta kumbukizi . . . . .

**KANGEMA/MATHIOYA**
**102/2**
**KISWAHILI**
**(LUGHA)**
**KARATASI YA PILI**

A. UFAHAMU (alama 15)

Soma ufahamu unaofuata kisha ujibu maswali yanayofuatia

Asilimia kubwa ya mataifa mengi yamefikia ngazi ya juu katika maendeleo ya afya ya umma katika miaka thelathini iliyopita. Kuna sababu nyingi ambazo zimesababisha hali hii. Moja kati ya sababu hizi ni kuwako kwa ufahamu wa kina kuhusiana na magonjwa na vyanzo vyake. Pili, kuwako kwa njia wazi na utambuzi wa makundi yanayoadhirika na magonjwa fulani. Tatu, utekelezaji na usambazaji wa maarifa pamoja na uhamasishaji wa makundi yanayohusika kubadili tabia zao au kuchukua hatua bora za kiafya. Msemo wa kuwa ni heri kuzuia kuliko kutibu umekuwa nguzo ya matendo hayo.

Hata hivyo hali kama hii haionekani kuhusiana na suala la usalama wa umma. Katika miji mingi ulimwenguni, hususan ile mikubwa viwango vya uhalifu vimepanda. Ghasia zinazohusiana na vijiana, ukosefu wa usalama kwa watoto na wanawake, wizi wa magari, uvunjaji wa nyumba, utumiaji wa nguvu, wizi wa mabavu na ukosefu wa usalama yamekuwa matatizo sugu. Je, ni kwa nini hali ikawa mbaya kiasi hiki?

Kwa kiasi Fulani hali kama hii inatokana na mambo mengi. Mojawapo ni upungufu wa njia asilia za kuukabili uhalifu kama polisi, mahakama na magereza. Pili ni kutochunguza na kutojaribu kusuluhisha matatizo ya kimsingi yanayochangia kuwako kwa uhalifu. Usalama wa umma ni moja kati ya vigezo vya kimsingi vya maisha bora pamoja na maendeleo ya kijamii na kiuchumi. Usalama huu unapaswa kuzingatiwa kama msingi muhimu na kila mwanajamii ana jukumu kubwa la kuhakikisha kuwa umepatikana. Suala la uhalifu sio suala la polisi na mfumo wa utendaji haki tu. Ili kufanikiwa katika uzuiaji wa uhalifu, lazima washika dau wote wahusike katika suala hili. Je, ni mambo gani tunayopaswa kufanya ili tuzuie kuwako kwa uhalifu? Kwanza, pana haja kubwa ya kuchunguza na kuielewa barabara misingi ya uhalifu na ghasia za mijini. Baada ya kuchunguza, pana haja ya kuchukua hatua zitakazosaidia kupunguza idadi ya waathiriwa na jamii ya wahalifu mijini. Hatua hizi ni kama kuwako kwa muundo mzuri na salama wa miji. Kusaidia watoto na jamaa zisizokuwa na uwezo, kuhakikisha baadhi ya huduma kama polisi na utekelezaji wa haki zimetengenezwa kwenye jamii; kuwawezesha wahalifu kuyarudia maisha ya kawaida na kuwasaidia waathiriwa wa uhalifu. Pili, njia za kuzuia uhalifu lazima zihusishe sehemu zote za jamii kama vile polisi, mfumo wa utendaji haki, huduma za kiafya na kijamii, huduma za malazi, sekta ya kibinafsi na mashirika ya umma.

Uzuiaji wa uhalifu unachangia kuleta umoja, ushiriki wa raia na utawala ufaao unaochangia kwa kiasi kikubwa katika ukuzaji na uendelezaji wa asasi za kidemokrasia, uwajibikaji wa vyombo vya huduma za umma kama polisi na mfumo wa utendaji haki. Kama ilivyo kuhusiana na ugonjwa ni heri kuzuia kuliko kutibu. Vivyo hivyo, uzuaji wa uhalifu ni bora kuliko kuukabili na kuutibu uhalifu wenyewe.

**Maswali**

a) Kwa nini mataifa mengi yamepiga hatua kubwa kiafya. (alama 2)
b) Eleza sababu zinazofanya uhalifu kuwako katika maeneo ya mijini? (alama 2 )
c) Je, ni hatua zipi huchukuliwa kuupiga vita uhalifu? (alama 6)
d) Eleza faida za kuuzuia uhalifu. (alama 2)

for free revision past papers visit: www.freekcsepastpapers.com

e) Eleza maana ya vifungu hivi kwa mujibu wa kifungu ulichosoma. (alama 3)

i) Uhamasishaji wa makundi. ..........................................................................................................

ii) Matatizo sugu ..........................................................................................................

iii) Washika dau ..........................................................................................................

2. **MUHTASARI (alama 15)**

<u>Soma makala yafuatayo kisa ujibu maswali</u>.

Utamaduni unaweza kugawika katika makundi mawili makuu. Utamaduni simulizi na utamaduni andishi. Utamaduni simulizi kama lilivyo jina lenyewe, linalochochea fikra kuwazia fasihi simulizi, ni utamaduni ambao unahusishwa na jamii ambazo zinatilia maanani maandishi mno. Katika jamii za aina hiyo, usimulizi au upokezanwaji kwa njia ya mdomo kutoka kwa mwanajamii mmoja hadi kwa miwingine huchukua nafasi kubwa sana. Katika jamii hiyo; wanajamii wanachukuliwa kama kanzi ya kuhifadhi amali, thamani, fasihi, falsafa na historia ya jamii inayohusika.

Utamaduni simulizi unategemea neno la mwanajamii ambalo ni hai bali sio maandishi ambayo yanabakia katika hali moja. Neno hilo linaweza kuwasilishwa kwa hali mbalimbali. Mbali kutegemea hadhira ya jamii inayohusika kwa mfano, katika utambaji wa ngano za fasihi simulizi, fanani ana uwezo wa kutumia ubingwa wake wa ufaraguzi, kubadilisha sifa fulani za ngano ili ziafikiane na hadhira yake. Kwa njia hii anaweza kuwasiliana na hadhira yoyote ile. Jamii zetu bado zingali zinatawaliwa kwa kiasi kikubwa na utamaduni wa aina hii. Tuangalie mfano wa methali kadha za kiswahili. Zipo methali mbili maarufu, 'ashibaye hamjui mwenye njaa', na 'mwenda pate kuayi kiuyacho ni kiririo'. Methali hizi huweza kusemwa kama, 'mwenye shibehamjui mwenye njaa; na 'aendaye pate harudi kirudicho ni kilio' au mwenda pate harudi kinachorudi ni kilio. Kuwepo kwa sifa hii hutokana na utamaduni simulizi uliopo katika jamii. Utamaduni simulizi umejengwa kwenye jadi ya kuielewa jamii na matakwa yake. Hii ni jadi ya kuelewa jinsi ambavyo sauti inakuwa na machango mkubwa katika kuujenga na kuimarisha ushirikiano wa wanajamii.

Utamaduni andishi kwa upande wake ni zao la kuvumbuliwa kwa mfumo wa maandishi; mfumo huu hauna historia ndefu katika jamii za walimwengu. Utamaduni simulizi ndio uliokuwapo tangu zamani. Utamadani andishi unategemea maandishi ambayo yanawasilishwa kwa njia tofauti. Wapo wanafalsafa ambao wanasema kuwa mfumo wa kuandika unawasilisha tu maandishi ambayo yalikuwa akilini kabla ya kuandikwa huko. Wapo wanajamii wanaoshikilia kuwa utamaduni andishi unakosa uhai kwa sababu unategemea maandishi. Ule uhusiano uliopo baina ya fanani na hadhira yake haupo. Kwa kiasi ni kama yapo mazungumzo yanayotokea baina ya fanani na hadhira yake. Mazungumzo haya yanajenga mahusiano ya kihisia ambayo yanapotea katika utamaduni andishi. Huu ni utamaduni unaosisitiza ubinafsi na upweke wa kuchukua kitabu na kujisomea. Ni utamaduni unaoua mshikamano wa jamii. Ni utamaduni unaoua uwezo mkubwa wa neno lililotamkwa. Hata hivyo, tamaduni zote mbili zinapaswa kuendelea kuwako katika jamii.

for free revision past papers visit: www.freekcsepastpapers.com

**Maswali**

a) Eleza sifa za utamaduni simulizi. (maneo 60 - 65) (alama 7)

b) Eleza sifa za utamaduni andishi. (maneno 50) (alama 7)

**C. SARUFI NA MATUMIZI YA LUGHA. (alama 40)**

a) i) Eleza maana ya mofimu. (alama 1)
ii) Ainisha mofimu katika neno lifuatalo Amkeni. (alama 2)

b) Eleza kazi ya vitenzi katika sentensi ifuatayo. (alama 3)
Utakuja kuwa mtu maarufu ukifuata maagizo.

c) Tunga sentensi iliyo na nomino ya kitenzi -jina na nomino ya jamii. (alama 2)

d) Bainisha matumizi ya 'po' katika sentensi ifuatayo. (alama 2)
Alipowasili alionyeshwa walipo.

e) Ainisha chagizo katika sentensi ifuatayo .
Jumba kubwa ajabu lilijengwa kwa kasi mwezi uliopita. (alama 3)

f) Andika sentensi ifuatayo katika wakati ujao hali ya kuendelea.
Wanafunzi hawakuadhibiwa. (alama 2)

g) Andika katika hali ya udogo wingi .
Mvulana yule alipewa kipande cha mkate. (alama 2)

h) Eleza maana mbili za sentensi ifuatayo. (alama 2)
Ameniletea changu.

i) Changanua sentensi ifuatayo kwa kutumia jedwali. (alama 4)
Yeye alifaulu hata kama hana adabu

j) Bainisha virai katika sentensi ifuatayo. (alama 3)
Haya machafu yataoshewa mtoni kesho asubuhi.

k) Tunga sentensi mbili konyesha maana tofauti ya maneno haya. (alama 2)
nchi
inchi

l) Huku ukitoa mifano tofautisha sauti ghuna na sauti sighuna. (alama 2)

m) Tambua aina ya shamirisho katika sentensi ifuatayo. (alama 2)
Baba alimjengea nyanya nyumba kwa nyasi.

n) Akifisha sentensi ifuatayo. (alama 2)
nitaenda mombasa kesho baba alisema

o) Ainisha vishazi katika sentensi ifuatayo. (alama 2)
viatu hivi vinang'aa ijapokuwa havipendezi

p) Tunga sentensi ukituma kiwakilishi cha pekee kuleta dhana ya umilikaji. (alama 2)

q) Tambua kiunganishi katika sentensi ifuatyo na utaje dhana inayowakilishwa. (alama 2)
Alimuua simba seuze paka.

**4. ISIMU JAMII.**

a) Fafanua sifa nne za sajili ya mazungumzo ya ana kwa ana. (alama 4)

b) Taja na ueleze pingamizi zozote sita zinazokwamiza juhudi za kukuza Kiswahili. (alama 6)

for free revision past papers visit: www.freekcsepastpapers.com

**KANGEMA/MATHIOYA**
**102/3**
**KISWAHILI**
**2017**
**KARATASI YA TATU**
**(FASIHI)**

**1. SEHEMU YA 'A'**
**TAMTHILIA:**
**Mstahiki Meya :** Timothy M. Arege

1. " Hii harufu mbaya ya taka iliyoupamba mji wetu ni kiwakilishi tu cha uozo ulio ndani".
   a) Fafanua muktadha wa maneno haya. (alama 4)
   b) Taja na ueleze tamathali za usemi zilizotumika katika dondoo. (alama 2)
   c) Kwa kutoa hoja kumi onyesha uozo ulio ndani ya mji huu. (alama 10)
   d) Eleza umuhimu wa msemaji tamthiliani. (alama 4)

**SEHEMU YA B RIWAYA:**
**Kidagaa Kimemwozea ;** Ken Walibora
Jibu swali la 2 au la 3

2. "Yaani ardhi ndicho kichocheo kikubwa cha unyama kwa binadamu, ukosefu wa utu."
   a) Thibitisha ukweli wa kauli hii kwa kutoa hoja zozote saba. (alama 14)
   b) Thibitisha kuwa anayewaza maneno haya alikuwa mwenye utu. (alama 6)

AU

3. Ndoa ni asasi ambayo kwayo mwanamke amedhulumiwa pakubwa katika jamii. Jadili kwa mujibu wa riwaya hii. (alama 20)

**SEHEMU YA C**
**HADITHI FUPI**
**Damu Nyeusi na Hadithi nyingine** : Ken Walibora na Said A. Mohamed
*Jibu swali la 4 au la 5*

4. "Hapa huingii bila kuninyoshea mkono."
   a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
   b) Eleza sifa mbili za msemaji katika dondoo hili. (almaa 4)
   c) Jadili maudhui sita yanayojitokeza katika hadithi hii. (alama 12)

**AU**

5. Waafirka hupitia matatizo mbalimbali wakiwa ughaibuni. Jadili ukirejelea hadithi ya Damu Nyeusi na Tazamana na mauti. (alama 20)

**SEHEMU YA D: USHAIRI**
***Jibu swali la 6 au la 7***

**6. Soma shairi lifautalo kisha ujibu maswali.**

**SIPENDI KUCHEKA.**

Pana jambo ninatukiya, kwangu hilo ni muhali,
Kitenda naona haya, kujishusha yangu hali
Sipendi unipe hidaya, sipendi kutenda hili.
Sipendi mimi kucheka

Sipendi mimi kucheka, kuchekea mawi
Sipendi na ya dhihaka, kwangu nyemi hiwi
Sipendi kwa hakika, mwovu kistawika
Halafuye nikacheka!

Masikini akiteswa
Yatima akinyanyaswa
Mnyonge naye akinyonywa
Sipendi hata ikiwa
Unazo nguvu najuwa
Ni hili sitatekezwa

Mbona lakini nicheke, kwayo furaha?
Na wewe ukajiweke, uli na siha?
Na yatima ali pweke, wa anahaha?
Amenyimwa haki yake, hanayo raha!
Na moyo wangu ucheke, kwa ha, ha, ha!
Kucheka kwa kucheka mimi katu sitacheka.

for free revision past papers visit: www.freekcsepastpapers.com

a) Taja sababu, zinazomfanya mshairi asitake kucheka. (alama 3)
b) Shairi hili ni la aina gani? Thibitisha . (alama 4)
c) Eleza toni ya shairi hili. (alama 2)
d) Fafanua uhuru wa mshairi katika shairi hili. (alama 3)
e) Andika ubeti wa pili kwa lugha nathari (tutumbi) (alama 4)
f) Tambua nafsi neni katika shairi. (alama 2)
g) Eleza maana ya msamiati ufuatao kama ulivyotumika katika shairi . (alama 2)
   i) Mawi.
   ii) Nyemi

AU

**7. Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali yatakayofuata.**

Kimya changu kimezidi, navunja yangu subira,
Marejeya ya miradi, kuhitimisha dhamira,
Kukejeli sina budi, niwafunze utu bora,
Nani aali zaidi, Wakenya au vinara?"

Serikali bila hadi, ndo kiini cha madhara,
Yanopiga kama radi, isokuwa na ishara,
Yamini kuwa gaidi, wakitupora mishahara,
Nani aali zaidi, Wakenya au vinara?

Wamejifanya hasidi, wasopatana kifikira,
Wana yao maksuudi, kujisombea ujira,
Wakilenga kufaidi, tumbo zao za kichura,
Nani aali zaidi, Wakenya au vinara?

Nchi yetu kufisidi, ni jambo linonikera,
Tangia siku za jadi, ufukara ndo king'ora,
Kutujazeni ahadi, nyie mkitia fora,
Nani aali zaidi, Wakenya au vinara?

Maskini watozwa kodi, wapwani na walo bara,
Kwa uvumba na uudi, mwawalipa kwa hasara,
Hamudhamini miradi, mejihisi masongora,
Nani aali zaidi, Wakenya au vinara?

Mesema kazi ni chudi, basi sirikali gura,
Nafsi zenu mzirudi, mkubali kuchakura
Makondeni mkirudi, muondoe ufukara,
Nani aali zaidi, Wakenya au vinara?

Ujanjenu umezidi, demokrasia bakora,
Debeni takaporudi, michirizi kwenye sura,
Kuwachuja a! muradi, kwa za mkizi hasira
Nani aali zaidi, Wakenya au vinara?

for free revision past papers visit: www.freekcsepastpapers.com

6

a) Toa anwani mwafaka kwa shairi hili. (alama 1)
b) Fafanua tamathali tatu za usemi zilizotumiwa katika shairi hili ukizitolea mifano mwafaka. (alama 6)
c) Ainisha shairi hili ukizingatia. (alama 2)
   i) Vina
   ii) Vipande
d) Andika ubeti wa nne kwa lugha nathari. (alama 4)
e) Taja maudhui matatu yanayojitokeza katika shairi hili. (alama 3)
f) Tambua toni ya shairi hili (alama 1)
g) Fafanua mbinu zilizotumiwa kutosheleza mahitaji ya kiarudhi. (alama 3)

**SEHEMU YA E: FASIHI SIMULIZI**

8. i) a) Eleza maana ya vitendawili. (alama 1)
      b) Eleza sifa tano za vitendawili. (alama 5)
      c) Jadili majukumu saba ya vitendawili katika jamii. (alama 7)
   ii) a) Eleza maana ya ulumbi. (alama 2)
      b) Eleza sifa ozote tano za mlumbi bora. (alama 5)

**SHULE YA UPILI YA SUNSHINE**
**102/1**
**KISWAHILI**
**INSHA**
**KARATASI 1**
**2017**
**MUDA: 1 ¾**

**1.** Umepata habari kwamba binamu wako anayeishi uholanzi ameanza kutumia mihadarati. Mwandikie barua pepe ukimweleza kuhusu athari hasi za tabia hiyo.

**SHULE YA UPILI YA SUNSHINE**
**KARATASI 102/2**
**KIDATO CHA NNE**
**IDARA YA KISWAHILI**
**SARUFI NA MATUMIZI YA LUGHA**
**2017**
**SAA: 2 ½**

**UFAHAMU ( AL 15 )**
**Soma taarifa ifuatayo kisha uyajibu maswali yaliyoulizwa.**

Miaka na dahari iliyopita katika nchi ya Uyunani aliishi mtaalamu anayefahamika kama Aristotle. Mtaalamu huyu anachukuliwa na watu wengi lama kitovu cha utaalamu nyingi. Msingi wa msimamo huu ni kuwa kauli, matamko na maandishi yake mengi yameishia kuwa kama msingi ambako majengo mbalimbali ya kitaalamu yamejengwa. Aristotle alisema kuwa binadamu au mja kimaumbile kuvutwa na hisia za kuishi katika jamii. Hisia hii ya kuishi katika jamii ndiyo msingi mkuu wa kushirikiana kwa njia anuwai, mathalani, maisha ya jamaa, vijijini, shuleni, serikali ha hata tawala mbalimbali.

Maisha yoyote ya jamii humjuzu binadamu ashirikiane na wenzake pamoja na kuvishirikisha vyake ili kuimarisha na kuyakomaza maisha au jamii yenyew. Yaani kuimarika na kokomaa kwa maisha ya jamii hutegemea kwa kiasi kikubwa mchango, japo ukufi, wa kila mwanajamii hiyo. Mchango huo hutokana na nia ya kutaka kuyaona maendeleo makubwa yamefikiwa siyo kwa nia ya kujinufaisha kama mtu binafsi bali kwa faida ya umma. Katika ushirikiano huo, ni lazima pasiwe na ubaguzi wala kutengana kwa misingi yoyote ile; ya rangi, maumbile, dini au hata hali ya maisha. Inahalisi kuikumbuka maana ya msemo kuwa rangi na ngozi ni utambuzi si ubaguzi.

Waja hushirikiana katika hatua mbalimbali. Binadamu anazaliwa katika jamaa na pale pale hujiunganisha na majirani. Ujirani huu wa binadamu wenzake pamoja na mazingira yao huiunda tabia yake. Kadiri anavyokua ndivyo anavyoanza kujihisi mmoja wa watu wanaomzunguka, jamii ile, kabila lile au hata taifa lile. Ile kukabiliana na mazingira yake, binadamu huhitaji msaada na hata ulinzi wa watu wengine. Huu hasa ndio msingi wa methali ya kuwa mtu ni watu. Tangu akiwa mwana mkembe, mja huhitaji msaada wa watu wengine kupewa chakula, kusimama na kutembea, kufundishwa jinsi ya kujielezea, kupata matunzo wakati wa magonjwa, kuelekezwa jinsi ya kupambana na mazingira yake, kusoma na kuilewa jamii yake na hata kufuata Imani Fulani. Binadamu hutamani kufanya mambo ya kila nui ambayo hawezi kuyatimiza peke yake. Kwa mfano, mia hutegemea haki zake zilindwe na wengine, mathalani, serikali.

Popote binadamu alipo, ana haki ya kushirikiana na wenzake katika jamii yake. Haki ya kuishi maisha ya kijamii ni mojawapo katika haki za kimsingi katika maisha ya binadamu. Haki hii inaenda sambamba na uhuru wa binadamu wa kuchagua kikundi au tapo la wanajamii analotaka kujihusisha nalo. Haki hii ni ya lazima na inapaswa kulindwa isipokuwa pale tu inapokwenda kinyume na sharia za jamii Fulani. Kwa mfano , ikiwa kujihusisha na kikundi Fulani kunaelekea kuwa tishio kwa usalama wa jamii, basi haki hii huwa imetumiwa vibaya. Pili, binadamu anayeishi katika jamii anaweza kujipatia ali kutokana na kazi au juhudi zake. Hii ni haki yake. Hata hivyo, huruhusiwi kuiba ili aweze kuipata mali hiyo.

Ushirikiano kati ya binadamu au ushirikiano katika jamii ni msingi imara wa kuwepo kwa maendeleo katika jamii Fulani. Kila tutumiapo neo 'maendeleo', humaanisha kujielekeza lengo maalum tulilochagua na ambalo litayakuza maisha yetu. Maendeleo huhusisha kupiga hatua mbele. Mtu anayesonga mbele hana budi kuwa na kitu au lengo analoliendea huko mbele ikiwa hana lengo, basi takuwa anawayawaya kama kuku aliyedenguliwa kichwa na anapaswa kujitathmini. Maendeleo yanahusisha kutoka hatua Fulani duni hatua nyingine afueni.

Katika zama kongwe za kisayansi yamefikia ngazi za juu sana katika awamu hii kumesahilisha mambo mengi sana. Kuna mambo mengi chanya ambayo yametokana na maendeleo ya kisayansi kama vile: kurahisisha mawasiliano, kuharakisha na kuboresha uzalishaji mali, kufanya usafiri bora na mwepesi miongoni mwa wengine. Hata hivho, kuna maendeleo hasi kwa kuwepo kwa silaha za haki zinazoweza kuuangamiza ulimwengu mzima. Nchi ambazo zina satua kubwa huweza kutumia uwezo wao wa kiuchumi na kimaendeleo kuzidhalilisha jamii nyingine. Hata hivyo, ni vizuri maishani binadamu, mkubwa kwa mdogo, mwenye uwezo kwa asiyekuwa nao atambue kuwa mja anahitahi jamii.

for free revision past papers visit: www.freekcsepastpapers.com

**Maswali**

a) Je, ina maana gani kusema 'Aristotle anachukuliwa kama kitovu cha taaluma nyingine? (alama2)
b) Taja haki mbili kuu za binadamu (alama2)
c) Je, kwa mujibu wa kifungu hiki, maana ya maendeleo ni nini? (alama 3)
d) Kulingana na taarifa na taarifa hii, ni kwa nini huhitaji jamii. (alama 3)
e) Kifungu hiki kinatoa ushauri gani kubwa binadamu? (alama 2 )
f) Eleza maana ya maneno na kifungu kifuatacho kama kilivyotumiwa katika taarifa hii. (alama 3 )
   i) Satua
   ii) Anawayawaya

**2. UFUPISHO** **( ALAMA 15)**

**Soma kifungu kisha uyajibu maswali yanayofuata.**

Nidhamu ni kitu cha maana sana maishani mwa binadamu. Kila mwanafunzi anapaswa kuwa na nidhamu ya hali ya juu sana. Akiwa na nidhamu, atakuwa mtu mwadilifu anaweza kustahiwa na kusadikika katika mambo, shughuli na hali tofauti.

Kwanza, motto mwenye nidhamu huwa kama anga au nuru nyumbani, shuleni na pia katika jamii. Watu wote wanampenda na kumheshimu. Wazee kwa vijulanga wale wanamtegemea kama msimamizi wa mambo nyeti ya maisha yao. Kwa hivyo, ni dhahiri shahiri kwamba mwadilifu hunufaika sana, kinyume cha mkaidi ambaye wahenga walimwambia kwamba atakosa kufaidi hadi siku ya Idi.

Pili huwadia nyakati ambapo huwa kuna jambo la busara, mathalani jukumu ana dhima Fulani ambayo huhitaji tu mwakilishi mmoja darasani, shuleni au katika jamii. Bila shaka watu watamteua yule mwadilifu kuchukua nafasi kama hiyo. Ndio maana viranja wanaoteuliwa shuleni, huwa ni wanagenzi ambapo tayari wamekwishatiwa katika mizani na kupigwa msasa madhubuti.

Vile vile, mwadilifu daima atajiepusha na shutuma na manjanga yote yanayoweza kuchipuka.

Kuna msemo maarufu kwa busara yake iliyobusarisha mwadilifu kwamba, "aliye kando haangukiwi na mti. Pia waliambiwa kwamba, " Pilipili usiyoila yakuwashiani?"

Ni bayana kutokana na misemo hiyo miwili kwamba mwenye nidhamu hawezi kuhusishwa na majanga hatari yanayoweza kuwakumba watu.

Walakini ni vyema kujiuliza, je, nidhamu huanzia wapi, na kwa nini kuna baadhi ya ' watoro ambao ni watovu wa nidhamu? Utovu wa nidhamu huanzia awali sana maishani mwa mja. Mtoto anapozaliwa, anategemea miongozi na mielekeo ya watu wazima ambao mazingirane mwake. Ndipo wa kale wale waliokaramka walisema kwamba mtoto akibebwa, hutazama kisogo cha nina.

Hivi ni kusema kwamba, nidhamu au utovu wa nidhamu huanzia nyumbai hadi shuleni, kisha hupanuka hadi kutikia kiwango ambapo mja anatangamana na watu katika maisha yake ikiwa sehemu moja ya ukuaji wa nidhamu maishani mwa mja itasambaratika, basi hawezi akawa mkamilifu kinidhamu maishani mwake.

Kwa vile ni bayani kwamba mabaya yote wayatendao duniani hulipwa na Mola papa hapa duniani, watovu wa nidhamu wote huishia kuangamia, ama kujuta mno kwa amali zao potovu. Ni heri mja kujihidi mwenyewe, kwani huhalifu haulipi chochote.

for free revision past papers visit: www.freekcsepastpapers.com

**Maswali**

a) Kwa kurejelea aya tano za kwanza, eleza madhara yanayoweza kumpata mtu kwa kutokuwa na nidhamu. ( maneno kati ya 50 – 60 ) (al 6, 1 ya mtiririko)
b) Bila kubadilisha maana, fupisha aya nne za mwisho. (Tumia maneno 55-60) ( al 7, mtiririko 1)

**3. MATUMIZI YA LUGHA ( ALAMA 40 )**

1. Kwa kuzingatia hali y a mtetemeko wa nyuzi za sauti, taja aina mbili kuu za sauti. (alama 2 )
2. Fafanua muudno wa silabi ya neno <u>Ngwena.</u> (alama 2 )
3. Tunga sentensi moja kwa kutumia neno hili ' walakini' (alama. 2 )
4. Taja vipashio vikuu vya lugha kuanzia kikubwa hadi kidogo. (alama. 2)
5. Tunga sentensi moja kudhihirisha maana mbili tofauti ya maneno haya: (alama 2)
   Shaba
   Shamba
6. Taja kwa kutolea mifano matumizi mawili ya kinyota. (alama 2)
7. Ikarabati sentensi hii: (alama 2 )
   Mgeni ambaye aliyekuja atarudi jana
8. Taja miundo mine ya ngeli ya A-WA. (alama.2)
9. Tunga sentensi kwa kutumia kihisishi cha dharau. (alama. 2)
10. Ainisha mofimu katika neno: (alama. 2)
    yanyweka.
11. Taja sifa mbili za vitenzi vya asili ya kigeni. (Alama. 2)

12. Onyesha kiima na kiarifa katika sentensi. (alama. 2)
13. Eleza miundo yoyote tatu ya kirai Nomino. (alama. 3)
14. Taja sifa zozote mbili za kishazi tegemezi. (alama. 2)
15. Tunga sentensi yenye muundo huu: (alama. 2)
    Kitondo, kiarifa, kipozi, ala.
16. Tofautisha kati ya chagizo na kijalizo. (alama. 2)
17. Changanua sentensi hii kwa njia ya matawi. (alama. 4)
    Alifika jana alipotarajiwa.
18. Tunga sentensi kwa kutumia kiambishi cha masharti yanayowezekena. (alama. 2)
19. Ainisha matumizi ya ji katika sentensi hii: (alama. 1)
    Jitu lililojitokeza limeuawa

**4. ISIMU JAMII (AL. 10)**

1. Eleza maana ya istilahi zifuatazo (alama. 6)
   a) krioli
   b) Jamii -------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------
   c) Linguo Franka ---------------------------------------------------------------------------------------------------------------
2. Fafanua mambo yanayochangia mtu kuwa na wingi lugha. (alama. 24

for free revision past papers visit: www.freekcsepastpapers.com

**SHULE YA UPILI YA SUNSHINE**

**102/3**
**KISWAHILI**
**FASIHI YA KISWAHILI**
**2017**
**MUDA: 2 ½**

1. **SEHEMU YA A: KIDAGAA KIMEMWOZEA** **( ALAMA 20)**
Walemavu katika jamii wametengwa badala ya kupendwa. Fafanua kauli hii kwa kurejelea Riwaya ya Kidagaa Kimemwozea. (alama 20)

2. **SEHEMU YA B: TAMTHILIA ( ALAMA 20)**
1. **"**Ya mwananti kiuvunda nti!"
a) Weka dondoo hili katika muktadha wake.
b) Tambua tamathali za usemi katika dondoo. (alama 2)
c) Fafanua ukweli wa "Ya mwananti kiuvunda nti!" kwa kurejelea tamthilia nzaima. (alama. 14)
2. Fafanua hali ya matibabu katika mi wa Cheneo (alama. 20)

3. **SEHEMU Y A C: HADITHI FUPI - Damu Nyeusi**
**i)** Vijana hukumbana na changamoto nyingi katika maisha Jadili kauli hii kwa kurejelea hadithi hizi. (alama. 20)
a) Damu nyeusi
b) Danda la usafi
c) Samaki wan chi za joto
d) Tazama na mauti
e) Shaka ya mambo

**ii)** "Leo ni siku ya siku , siku ya nyani kufa ambapo mtiti yote huteleza.
a) Eleza muktadha ya dondoo hili . (alama. 4)
b) Eleza sifa mbili za mrejelewa. (alama 2)
c) Fafanua changamoto zinazowakabili waafrika wasomi ughaibuni. (alama 14)

for free revision past papers visit: www.freekcsepastpapers.com

4. **SEHEMU YA C: USHAIRI**
**Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.**

1. Haki ya mtu thawabu Kuidai sitasita
Hata 'nipatishe tabu muhula mimi kukita
Kulitenda la wajibu liwe hai au mata
Nitafanya majaribi na inapobidi matata
Haki yangu 'taidai hata iwe ni kwa vita

2. Haki ha mtu u'ngwana siseme mimi nateta
Sitaukiri ubwna na jeuri unoleta
Na ikiwa ni kuwana sitajali sitajuta
Sikiri kuoneana na kupakana mafuta
Haki yangu 'taidai hata iwe ni kwa vita

3. Haki ifukie chini ipige na kubuta
'tumbukize baharini 'tazamia kufwata
Ukaifiche jangwani nitakwenda kuileta
Itundike milimani nitawana kuileta
Haki yangu 'taidai hata iwe ni kwa vita

4. Haki ijingee ngome izungushe na kata
Na fususi isimame iwe inapitapita
Tainuka nishikame haki yangu kukamata
Sifa kubwa mwanamume kuenda huku wasota
Haki yangu 'taidai hata iwe ni kwa vita

5. Uungwana siuuzi kwa njugu au kashata
Ahadi za upuuzi na rai kuitaita
Kwa kila alo maize hawi mithili ya bata
Tope yake makaazi na chakula cha kunata
Haki yangu 'taidai hata iwe ni kwa vita

**Maswali**

a) Bainisha dhamira ya mshahiri (alama. 2)
b) Eleza umuhimu wa mbinu zozote mbili ambazo mwandishi ametumia kutosheleza mahitaji ya kiarudhi. (alama. 4)
c) Andika ubeti wanne kwa lugha tutumbi. (alama. 5)
d) Fafanua aina tatu za urudiaji zilizotumiwa katika shairi hili. (alama. 3)
e) Ainisha shairi hili kwa kuzingatia vigezo vifuatavyo. (alama. 2)
   i) Idadi ya mishororo
   ii) Mpangilio wa vina
f) Fafanua toni ya shairi hili (alama. 1)
g) Taja nafsineni katika shairi hili (alama. 1)
h) Tambua na ueleze maana ya mshororo ufutao (alama. 2)

for free revision past papers visit: www.freekcsepastpapers.com

**MOKASA**
**102/1**
**KISWAHILI**
**2017**
**LARATASI YA 1**
**INSHA**

1. Swali la lazima
   Nchini Kenya, wananchi wamegawanyika katika misingi mbalimbali. Hali hii inatishia usalama na umoja wa kitaifa. Kama mtaalamu na katibu wa shirika lisilo la liserikali la Kenya Moja, mwandikie rais barua ukipendekeza mikakati ya kuimarisha na kudumisha umoja wa kitaifa.
2. Utandawazi una athari nyingi mbaya kuliko nzuri katika maisha yetu. Jadili.
3. Siku ya nyani kufa, miti yote huteleza.
4. Andika insha itakayomalizika kwa;
   Tokea siku hiyo, maisha yangu yakachukua mkondo mpya**.**

**TO BE TYPED P2**

for free revision past papers visit: www.freekcsepastpapers.com

**MOKASA**
**102/3**
**KISWAHILI**
**2017**
**Karatasi ya 3**
**FASIHI**

**SEHEMU A: TAMTHILIA**
**Timothy Arege:** *Mstahiki Meya*

**1. Lazima**

"Acha nimfuate mara moja hii."

(a) Weka dondoo hili katika muktadha wake. (alama 4)
(b) Fafanua sifa zozote **nne** za msemaji. (alama 4)
(c) Ubarakala unalemaza maendeleo katika Cheneo. Jadili. (alama 12)

**SEHEMU B: RIWAYA**
**K. Walibora :** *Kidagaa Kimemwozea*
*Jibu swali la 2 au la 3*

**2.** Usaliti umeitawala jumuiya ya Kidagaa Kimemwozea. Thibitisha ukweli huu ukirejelea wahusika mbalimbali katika riwaya. (alama 20)

**3.** 'Sijawahi kumwona kibogoyo akiguguna mfupa. Siku moja isiyokuwa na jina siri zako zitafichuka na hila zako zikutokee puani.'

(a) Eleza muktadha. (alama 4)
(b) Taja na ueleze mbinu zozote mbili zinazodhihirika kwenye dondoo. (alama 4)
(c) Huku ukirejelea riwaya hii, fafanua kwa kutoa hoja sita namna anayelengwa na kauli hii, siri zake zilivyofichuka na hila zake kumtokea puani. (alama 12)

for free revision past papers visit: www.freekcsepastpapers.com

**SEHEMU C: USHAIRI**
*Jibu swali la 4 au la 5*

**4.** Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali yafuatayo.

**LONGA**

Longa longea afwaji, watabusarika
Longa uwape noleji, watanusurika
Longa nenea mabubu, sema na viduko

Longa usichachawizwe, tamka maneno
Longa usitatanizwe, mbwa aso meno
Longa usidakihizwe, kishindo cha funo

Longa yote si uasi, si tenge si noma
Longa pasi wasiwasi, ongea kalima
Longa ukuli kwa kasi, likate mtima

Longa zungumza basi, liume ja uma
Longa japo ni kombora, kwa waheshimiwa
Longa liume wakora, kwani wezi miwa

Longa bangu na papara, hawakuitiwa
Longa bunge si kiwara, si medani tawa
Longa ni simba marara, wanaturaruwa.

**Maswali**

(a) Tambua na ueleze nafsi neni katika shairi hili. (alama 1)
(b) Onyesha vile kibali cha utunzi wa mashairi kilivyotumika kukidhi mahitaji ya kiarudhi. (alama 4)
(c) Kwa kutoa maelezo mwafaka, tambua bahari nne zilizotumika na mtunzi kwenye shairi hili. (alama 4)
(d) Eleza aina tatu za urudiaji katika shairi. (alama 3)
(e) Tambua na kueleza toni ya shairi. (alama 2)
(f) Eleza maana ya msamiati ifuatayo kama ilivyotumika katika shairi. (alama 2)
  (i) Afwaji
  (ii) Tenge
(g) Eleza umbo la shairi hili. (alama 4)

**5.** Soma shairi lifuatalo kisha uyajibu maswali.

Jiji Juani
Jiji
Lililojaa fahari na vinyume

Maghorofa
Yatishayo kupasua ngozi ya mawingu
Viumbe na magari
Waliobanana barabarani.

Jiji la
Waliostaarabika
Ya kidunia
Mafukara.

Lililojaa mfano na mwambatano
Wa majalala ya taka na waokotezaji
Wa ombaomba na waliotakata
Wa polisi na dereva
Wa waliopujuka na wanaostahi.
Jiji la :
majengo ya aushi na mioyo ya mawe
jua linalooka viumbe
jua linalotekenya ngozi za watalii – wakimbiao ganzi ya
maji baridi
jua lichomalo wavuja jasho
Huku wakizumbua riziki.

La viwanda
Vijazavyo vibeti vyenye mimba vya wenye viwanda
Vinavyofuka moshi kwenye Madongoporomoka
Vinavyosumu maisha machanga na kuua wasiozaliwa.

Jiji
La wazururao na manamba
Wanaotia kitanzi staha
Wanaotoa kauli na maneno
Yanayouma na kukereketa.

La wazee na vijana
Ambao taadhima yao
Imemezwa na jiji juani.
Jiji litandalo mashariki na magharibi
Kaskazini na kusini
Mbuga zitandazo
Katikati ya tanuri hili.

Litengalo sehemu kwa baadhi
Majumba vilimani
Vyumba visivyodari
Na mabanda yaso dirisha
Kusugua mikono laini ya mwenye nyumba.

for free revision past papers visit: www.freekcsepastpapers.com

**Maswali**

(a) Fafanua maswala **matatu** makuu aliyoyashughulikia mshairi tungoni. (alama 6)
(b) Jadili jinsi mtunzi alivyotumia jazanda kufanikisha ujumbe wake. (alama 6)
(c) Mishata ni nini ? Bainisha matumizi mawili katika shairi. (alama 4)
(d) Shairi hili ni la kukatisha tamaa. Dhihirisha. (alama 4)

**SEHEMU D: FASIHI SIMULIZI**

**6.** **(a)** Fafanua sifa za matambiko katika jamii. (alama 4)
(b) Eleza tofauti kati ya maigizo ya kawaida na maonyesho ya sanaa. (alama 10)
(c) Taja shughuli zozote mbili zinazoonyesha matumizi ya ulumbi katika jamii ya kisasa. (alama 2)

(d) Tofautisha dhana zifuatazo :

(i) Miviga na maapizo (alama 2)

(ii) Ngoma na ngomezi (alama 2)

**SEHEMU E: HADITHI FUPI**

**K. Walibora** na **S. A. Mohamed:** *Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine*

**7.** Upungufu wa maadili ni suala linaloangaziwa katika Diwani ya *Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine*. Jadili kauli hii kwa kuzingatia haditi zozote tano. (alama 20)

for free revision past papers visit: www.freekcsepastpapers.com

**MTIHANI WA MWIGO - SUKEMO 2017.**
**102/1**
**KISWAHILI**
**Karatasi ya 1**
**INSHA**
**Julai 2017**
Muda: Saa 1 ¾

1. **Lazima.**
   Andika taarifa kuhusu namna wizi wa mifugo unavyoathiri jamii nyingi nchini Kenya.
2. Mafuta yaliyovumbuliwa nchini Kenya yataleta faida nyingi kuliko hasara. Jadili.
3. Andika kisa kinachoafikiana na methali ifuatayo; "Elimu ni taa,gizani huzagaa."
4. Andika insha itakayoanza kwa maneno haya, " Kimya! Ukumbi mzima ulitulia tuli kwa matarajio makubwa. Wote walikuwa..."

**TATHMINI YA PAMOJA YA SUKEMO Kenya Certificate of Secondary Education**
102/2
**Karatasi ya 2**
**LUGHA**
Muda: Saa 2 ½

1. **UFAHAMU**: (Alama 15)
   *Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali*
   **Kigumba kwa nguruwe**

Kikamilifu methali hii ni kigumba kwa nguruwe kwa mwanadamu ki chungu. Kufahamu maana yake, ni lazima tuchunguze kijuujuu maana ya maneno yaliyotumiwa. Kigumba ni chembe cha mshale, mkuki au chusa kinachotumiwa kuchoma na kumjeruhi mnyama. Nguruwe ni mnyama anayesakwa na kufumwa na kufurahikiwa na wasasi anapopatwa. Uchungu ni maumivu yanayoletwa na kitendo hicho cha kufuma. Nguruwe hufisidi mimea ya wakulima. Hapo basi husakwa kwa mishale na mikuki na kuuliwa. Watu hupata uhondo wa nyama. Wakati mwingine, katika zile hekaheka za kusaka, huenda mshale au mkuki ukamdunga mtu badala ya yule mnyama. Vivyo hivyo anapaswa afahamu kuwa uchungu anaousikia yeye ndio ule aliousikia nguruwe.

Mzee Kisheta alikuwa mraibu wa bangi, na kwa sababu hiyo, hakuweza kumkimu yeyote; si mkewe, si watoto hata mwenyewe na aila yake yote. Kila hela aliyoipata, alilongeza katika vishindo vya wauzaji bangi. Mkewe, Kitete, alikuwa akienda kutafuta vibarua angalau awasitiri wanawe. Chochote kile alichopata, ilimbidi akifiche, kwani mumewe alivisaka vibetini, mitoni na matandikoni, chini ya mivungu ilmradi nyumba nzima aliichakura. Akikipata hukimbilia kwa wachuuzi wake. Asipokiona, humkabili mkewe kwa matusi na magumi. Mkewe, aliyechelea sana kufufutwa, humtolea nusu ya pesa alizopata ili aipoze ghaidhi ya mumewe. Kisheta huchomoka huyooo! Hapo basi Kitete huepukana na kero.

Siku moja, Kitete alirudi na shilanga lake begani huku akitabasamia mwanawe mdogo Kita, aliyeuona uso wa furaha wa mamaye uliobashiri mafanikio aliuliza, "Mama una furaha leo! Je, umetuletea nini?" Mamake alimjibu kuwa alikuwa na furaha sana siku ile kwa sababu bibi aliyemlimia ngwe siku hiyo alimpa bashishi ya shilingi ishirini kwa kazi yake nzuri. Badala ya shilingi hamsini alipata shilingi sabini. Ilikuwa furaha iliyoje! Alipomaliza kumjibu mwanawe kwa furaha, aliingiza jembe lake ndani na kutoka haraka haraka awahi kwenda madukani kabla ya Kisheta kufika pale na kumnyang'anya pesa zake alizozipata kwa jasho.

Alipotoka nje ya nyumba tu, alikutana na mumewe aliyezuka ghafla, haijulikani kutoka wapi! Papo hapo alimtolea jicho mkewe mkono kaunyosha akitaka kupewa ujira wote alioupata siku hiyo. Mama Kita alikataa katakata akisema hakupata chochote siku ile.

Kisheta alikuja juu, akamshika mkewe akitaka kumvunja kama ukuni mkavu. Mkewe alilia kwa uchungu akijaribu kujikwamua, lakini mikono yake Kisheta ilikuwa imemkaba kama koleo. Hakuweza kumtoka. Mwanawe, Kita, alivyomwona mamaye alivyokuwa akiteseka alisema, "Mama kwa nini ufe na pesa unazo? Si umpe baba hizo shilingi sabini ulizozifunga hapo katika pindo la leso?" Kusikia hivyo, Kisheta alimwachilia mkewe kwa kumkita chini na kumwamrisha ampe pesa zile. Bibi huyo hakuwa na la kufanya ila kuzitoa. Kisha akakaa chini na kujiinamia kwa huzuni. Mzee Kisheta alifurahi na kumyanyua Kita juu na kusema. "Wewe u dume kweli! Unampenda baba yako. Kua mwanangu na uwe kama babako. " Mtoto huyo alisikiza maneno hayo, lakini hakuonekana kuelewa aliyoambiwa.

Siku nyingi zilipita na maisha ya Kisheta yalizidi kuzorota. Jumapili moja baada ya kupotea kutwa nzima, asijulikane alikokuwa. Kisheta alirudi akiandamana na watu wawili hadi pale nyumbani kwake. Walipofika mkabala wa ukumbi, Kisheta alisikika akisema, "Mabwana, mimi asilani sivuti hata sigara, lakini ikiwa

for free revision past papers visit: www.freekcsepastpapers.com

mwasisitiza kuwa mwataka kuingia ndani basi mwakaribishwa." Kita aliposikia babake akisema hivyo alidakia, "Wewe baba huvuta sigara. Hata jana ulinituma sigara sita kubwa dukani kwa Ali." Kisheta alimrukia Kita akataka kumzaba makofi. Kumbe wale mabwana aliokuwa nao walikuwa askari kanzu. Walimzuia asimpige mtoto; walilisaka banda lake la nyumba na kuona vipande sita vya misokoto ya bangi chini ya sanduku la mbao lililokuwa na suruali moja iliyojaa viraka na fulana moja kuu kuu. Kisheta alitiwa pingu na kupelekwa kwenye kituo cha polisi. Alipokuwa akitolewa mle nyumbani, aliropoka laana kwa mwanawe Kita. Mama Kita matumbo yalimsokota akamkabili mumewe na kumsuta. "Msalie mtume? Usinilaanie mwanangu? Malipo ni hapa duniani. Jambazi we! Umepata stahili yako!"

(a) Toa fasili ya kigumba katika kisa hiki. (alama 2)
(b) Eleza uhusiano kati ya Kisheta na mkewe katika hali yao ya maisha. (alama 3)
(c) Ni kitu gani kilichopandisha mori Kisheta hata akawa karibu kumuumiza mkewe? (alama1)
(d) Taja sababu zilizomfanya mtoto Kita kutoboa kuwa mamaye alikuwa na pesa na babaye alivuta sigara. (alama 2)
(e) Ni mafunzo gani tunayoyapata kutokana na kisa hiki? (alama 3)
(f) "Kutojua ni usiku wa giza." Fafanua msemo huu ukilinganisha na makala uliyosoma. (alama 2)
(g) "Jambazi we! Umepata stahili yako!" Fafanua. (alama 2)

2. **MUHTASARI**: (alama 15)

*Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.*

Katika kipindi cha miaka iliyopita, kumekuwa na mfumko wa bei ya bidhaa muhimu hivi kwamba idadi kubwa ya raia wanalala njaa. Uchunguzi uliofanywa na mashirika ya kijamii kuhusu bei ya bidhaa hizo umeonyesha kuwa familia za kawaida zinatumia nusu ya mapato yao kununua chakula. Bila shaka yoyote, hili ni janga linaloendelea kutokota. Tunafahamu kuwa kupanda kwa bei ya petroli kimataifa kumechangia kuongezeka kwa bei hiyo ya vyakula, kwa namna moja au nyingine.

Mbali na vyakula, gharama ya kupanga nyumba, maji, stima na mafuta imepanda kwa muda wa miezi mitatu iliyopita kati ya Desemba na Januari 2017. Kwa mujibu wa Benki ya duniailiyozinduliwa hivi majuzi, kupanda kwa bei ya vyakula kumesukuma familia nyingi katika lindi la umaskini.

Ingawa serikali haina uwezo wa kudhibiti baadhi ya sababu zinazochochea kuongezeka kwa bei ya chakula nchini, haipaswi kutulia tuli ikisubiri suluhisho litokee kisadfa. Inasikitisha kwamba viongozi wetu wanatumia muda mwingi kuchapa siasa huku raia wa kawaida wakiendelea kuumia. Iweje basi katika vikao vyao vya hadhara wanasiasa wanatumia muda mwingi kuzungumzia maswala ya kugawanya wananchi na kufichua njama za kuwaangamiza wapinzani wao badala ya kueleza namna watakavyokabiliana na janga lililopo la njaa. Ni lini watafahamu kwamba hauwezi kumtawala mtu mwenye njaa?

Kwa muda mrefu, baa la njaa limekuwa likihusishwa na maeneo ya kaskazini mwa nchi yetu; lakini kama uchunguzi ulivyoonyesha, familia nyingi nchini zinaumia na wengi hawawezi kumudu bei ya bidhaa muhimu kama sukari, unga, mafuta ya kupikia na kadhalika.

Wakati umewadia kwa serikali kuchukua hatua madhubuti kwa kuwa kama ilivyo ni vigumu kumtawala mtu aliye na tumbo tupu na ambaye hajijui wala hajitambui kuhusu atakapopata lishe.

for free revision past papers visit: www.freekcsepastpapers.com

(a) Ukizingatia taarifa uliyosoma, fafanua athari za mfumko wa bei kwa wananchi. (maneno 35 - 40) (alama 5)
(b) Eleza mambo muhimu anayoyazungumzia mwandishi katika aya za mwisho nne. (maneno 60-65) (alama 10)

3. **MATUMIZI YA LUGHA**: (alama 40)

(a) (i) Eleza maana ya shadda. (alama 1)
(ii) Weka shadda katika neno lifuatalo: (alama 1)
Dhambi
(b) (i) Eleza maana ya sauti mwambatano. (alama1)
(ii) Andika sauti mwambatano **mbili** zinazotamkiwa kwenye kaakaa laini. (alama 1)
c) Tunga sentensi **moja moja** kubainisha kubainisha:
(i) Chagizo kariri (alama 1)
(ii) Kiwakilishi cha pekee chenye maana ya 'bila kubagua'. (alama 1)
(d) Tunga sentensi **moja** sahihi ukitumia kitenzi 'pa' katika kauli ya kutendwa. (alama 1)
(e) Bainisha mofimu katika neno: (alama 3)
Nitakunywea
(f) Andika sentensi ifuatayo katika wakati uliopita hali ya kuendelea. (alama 1)
Mtoto amekunywa maziwa.
(g) Kanusha: (alama 1)
Kiongozi aliombwa kukubali uteuzi huo.
h) Tunga sentensi **mbili** kuonyesha matumizi mawili tofauti ya kistari kirefu. (alama 2)
i) Andika katika ukubwa wingi: (alama 2)

Kitoto hiki kinalia kwa sababu hakijala mkate.

(j) Tumia 'O' rejeshi tamati katika sentensi hii. (alama 2)

Mkulima anayelima ni yule anayepata mavuno mengi.

(k) Tunga sentensi kuonyesha maana **mbili** za neno **chupa**. (alama 2)

(l) Nomino zifuatazo zimo katika ngeli gani? (alama 2)

(i) Ungo

(ii) Mchanga

m) Andika katika usemi wa taarifa. (alama 2)

Mwalimu alimuuliza mwanafunzi, "Unaitwa nani na ulikuwa ukisomea shule gani?"

n) Tambua aina za virai vilivyopigiwa mstari katika sentensi ifuatayo: (alama 2)

Kasuku <u>mwenyekelelenyingi</u> amefukuzwa <u>namsasihodari</u>.

o) Ainisha vishazi katika sentensi ifuatayo: (alama 3)

Japo Jelimo ni mkimbiaji hodari, alishindwa na Kadas aliyekuwa mbele yake.

p) Ainisha shamirisho zilizomo katika sentensi ifuatayo: (alama 3)

Swaleh ameinulia mwanawe baiskeli kwa mkono.

q) Eleza matumizi ya 'na' katika sentensi ifuatayo:

Juma na Yusufu wanasoma kitabu. (alama 2)

(r) Changanua sentensi ifuatayo kwa njia ya mistari.

Maria na kanini wamekuwa mtoni tangu jana. (alama 4)

(s) Andika kisawe cha 'kifungua mimba.' (alama 1)

(t) Andika kinyume cha sentensi ifuatayo:

Baba amekomea komeo hilo. (alama 1)

4. **ISIMUJAMII**: (Alama 10)

(a) Eleza maana ya ujozilugha. (alama 1)

(b) Huku ukitoa mfano **mmoja mmoja**, eleza tofauti kati ya kuchanganya ndimi /msimbo na kubadili ndimi/msimbo. (alama 4)

(c) Kwa nini watu wengi wana mazoea ya kuchanganya na kubadili ndimi/msimbo katika mazungumzo yao? (alama 5)

for free revision past papers visit: www.freekcsepastpapers.com

**MTIHANI WA PAMOJA WA SUKEMO**
**102/3**
**Kiswahili**
**Karatasi ya 3**
**Fasihi**
**July/ August 2017**
**Muda: Saa: 2 ½**
**SWALI LA LAZIMA**

**1. MSTAHIKI MEYA : TIMOTH M. AREGE**

Lazima wawepo nd'o ndege zitue ? Uwanja haukufungwa !

a) Eleza muktadha wa dondoo hili (al. 4 )
b) Eleza sifa mbili za msemaji na mbili za msemewa ? (al. 4 )
c) Eleza maudhui yafuatayo kama yanavyojitokeza katika tamthilia kwa kutoa mifano mitatu mitatu. (al. 12)
i) Usaliti
ii) Ubadhirifu

**RIWAYA : KIDAGAA KIMEMWOZEA**

2. « Lakini bila matumaini hatuwezi kwenda mbele na « Revolution »
a) Eleza kuktadha wa dondoo hili (al .4 )
b) Taja mbinu ya lugha katika dondoo hili (al. 2 )
c) Fafanua ni kwa nini TOmoko ilihitaji « Revolution » ili isonge mbele. (al. 14 )

3. Fafanua umuhimu wa barua zozote tano katika riwaya. (al. 20)

**HADITHI FUPI : DAMU NYEUSI**

4. Kwa kurejelea hadithi zifuatazo tano kutoka Diwani ya Hadithi fupi onyesha jinsi NDOA nyingi zinavyotumbukia katika doa. (al. 20)
a) Mke wangu
b) Kanda la usufu
c) Maeko
d) Tazamana na mauti
e) Mwana wa darubini

5. « Hakutaka afikiriwe 'mtu matata'. Pia hakuwa na azma ya kufanya kazi hapo daima. Hiyo si kazi aitakayo »
a) Fafanua muktadha wa dondoo hili (al. 4)
b) Eleza kichocheo kilichomchochea mhusika anayerejelewa kahamia anakoishi sasa. (al. 2)
c) Fafanua sifa za mhusika anayerejelewa (al. 4)
d) Anwani « shaka ya mambo » inaafiki hadithi husika. Thibitisha. (al. 10)

**6. USHAIRI**

***Soma shairi kasha ujibu maswali***

Lau kama ingakuwa, madhali tuna uhuru
Watu kodi kutotowa, na kuifanya kufuru
Vije nchi ingakuwa, taifa bila nduruु
Taifa halingakuwa, bilashi bila ushuru

Hivi taifa kumea, na kuendelea mbele
Kwamba hajitegemea, haliwatege'I wale
Yataka kujitolea, ushuru bila kelele
Taifa halingakuwa, bilashi bila ushuru
Wafanyikazi wa umma, mfano mwema walimu
Wauguzi mahashuma, daktari wahadimu
Bila hizi darahima, vipi wangalihudumu?
Taifa halingakuwa, bilashi bila ushuru.

Si vyema kuombamba, kwa wageni kila mara
Huwa twajifunga kamba, na kujitia izara
Adha zinapotukumba, kujitegemea bora
Taifa halingakuwa, bilashi bila ushuru.

Miradi ya maendeleo, yahitaji darahima
Nd tufike upeo, ulio dunia nzima
Wadogo na wenye vyeo, bila kodi tutakwama
Taifa halingakuwa, bilashi ushuru.

Ushuru si kwa wanyonge , wasokuwa na uwezo

for free revision past papers visit: www.freekcsepastpapers.com

Watozwe hata wabunge, na wengine wenye nazo
Yeyote asijitenge, kodi akalipa bezo
Taifa halingakuwa, bilashi bila ushuru

Kwetu kutoa ushuru, ndiko kujitegemea
Pasiwepo na udhuru, usio wa kulea
Huwa ni kama kiguru, asenao kutembea
Taifa halingakuwa, bilashi bila ushuru

**Maswali**

a) Lipe shairi anwani mwafaka? (al.1)
b) Weka shairi hili katika bahari mbili tofauti. (al.2)
c) Eleza muundo wa ubeti wa tatu. (al.3)
d) Fafanua uhuru wa mshairi. (al.3)
e) Andika ubeti wa sita katika lugha tutumbi. (al.4)
f) Taja nafsi nenewa katika shairi hili. (al2)
g) Tambua toni la shairi hili. (al.1)
h) Eleza ujumbe unaojitokeza katika ubeti wa tano. (al2)
i) Eleza maana ya msamiati ufuatao kama ilivyotumika katika shairi. (al. 2)
   i) Twajifunga kamba
   ii) Bezo

**7. Soma shairi kisha ujibu maswali yanayofuatia**

Mgomba umelala chini hauna faida tena
Baada ya kukatwa na kufanya kazi
Wa bustani kwa kusita
Watoto, kwa wasi wasi wanasuburi wakati wao
Watoto hakuna kitu
Isipokuwa upepo Fulani wenye huzuni
Unaotikisa majani na kutoa sauti ya kilio

Hivyo ndivyo ufalme wa mitara ulivyo
<u>Mti wa mji umelala chini</u> hauna faida tena
Baada ya kukatwa na wafanyikazi
Wa bustani kwa kusita
Chumbani hakuna kitu
Isipokuwa upepo Fulani wenye huzuni utingishao
Wenye hila waliozunguka kitanda na kulia
Machozi yenye matumaini ya iga
Mbiu ya hatari ya magomvi nyumbani.
      Magmvi
Kati ya wanawake
      Magomvi
Kati ya watoto wa ajili ya vitu na uongozi
Ole! Miliki ya 'Lexanda imekwisha!

Vidonda vya ukoma visofunikwa
Ambavyo kwa muda mrefu vilifichana
Sasa viko nje kufyonzwa nzi kila aina
Na vinanuka vibaya
Lakini inzi kila mara hufyonza wakifikiri
Nani watamwambukiza.

**Maswali**

a) Lipe shairi hili kichwa mwafaka (al. 2)
b) Taja wahusika wanaojitokeza katika shairi (al. 3)
c) Yataje mambo manne yanayotendeka baada ya mgomba kukatwa. (al. 4)
d) Tambua sifa zinazofanya utungo huu kuwa shairi (al. 5)
e) Fafanua kwa bahari mbinu katika shairi hili ukiondoa mifano mwafaka (al. 2)
f) Andika methali tatu zinazoweza kurejelewa katika shairi hili. (al. 3)
g) Kwa kutolea mifano taja na ufafanue mbinu mbili za Uhuru wa ushairi katika shairi hili. (a. 4)
h) Eleza maana ya mafungu yafuatayo yaliyotumiwa kama mafumbo katika shairi (al. 2)
1. Vidonda vya ukoma
2. Mti wa mji umelala chini

for free revision past papers visit: www.freekcsepastpapers.com

**8. FASIHI SIMULIZI**

Asiyemjua mjua alionwe atamjua
Namjuza kwa sifa zake alizokuwa nazo
Alisimika ufalme uliosifiwa
Akawa shujaa asiyetishwa

a) Tambua kipera hiki (al. 1)
b) Fafanua sifa tano za kipera hiki (al. 5 )
c) Tambua aina ya miviga katika jamii ya kisasa (al. 3 )
d) Fafanua njia za kuimarisha fasihi simulizi katika ulimwengu wa kisasa. (al. 5 )
e) Kwa kurejelea vigezo vitatu onyesha umuhimu wa fani katika kufanikisha usimulizi wa hadithi za fasihi simulizi. (al. 6)

for free revision past papers visit: www.freekcsepastpapers.com

**SHULE YA UPILI YA SUNSHINE**
**102/1**
**KISWAHILI**
**INSHA**
**KARATASI 1**
**2017**
**MUDA: 1 ¾**

**1.** Umepata habari kwamba binamu wako anayeishi uholanzi ameanza kutumia mihadarati. Mwandikie barua pepe ukimweleza kuhusu athari hasi za tabia hiyo.

**SHULE YA UPILI YA SUNSHINE**
**KARATASI 102/2**
**KIDATO CHA NNE**
**IDARA YA KISWAHILI**
**SARUFI NA MATUMIZI YA LUGHA**
**2017**
**SAA: 2 ½**

**UFAHAMU ( AL 15 )**
**Soma taarifa ifuatayo kisha uyajibu maswali yaliyoulizwa.**

Miaka na dahari iliyopita katika nchi ya Uyunani aliishi mtaalamu anayefahamika kama Aristotle. Mtaalamu huyu anachukuliwa na watu wengi lama kitovu cha utaalamu nyingi. Msingi wa msimamo huu ni kuwa kauli, matamko na maandishi yake mengi yameishia kuwa kama msingi ambako majengo mbalimbali ya kitaalamu yamejengwa. Aristotle alisema kuwa binadamu au mja kimaumbile kuvutwa na hisia za kuishi katika jamii. Hisia hii ya kuishi katika jamii ndiyo msingi mkuu wa kushirikiana kwa njia anuwai, mathalani, maisha ya jamaa, vijijini, shuleni, serikali ha hata tawala mbalimbali.

Maisha yoyote ya jamii humjuzu binadamu ashirikiane na wenzake pamoja na kuvishirikisha vyake ili kuimarisha na kuyakomaza maisha au jamii yenyew. Yaani kuimarika na kokomaa kwa maisha ya jamii hutegemea kwa kiasi kikubwa mchango, japo ukufi, wa kila mwanajamii hiyo. Mchango huo hutokana na nia ya kutaka kuyaona maendeleo makubwa yamefikiwa siyo kwa nia ya kujinufaisha kama mtu binafsi bali kwa faida ya umma. Katika ushirikiano huo, ni lazima pasiwe na ubaguzi wala kutengana kwa misingi yoyote ile; ya rangi, maumbile, dini au hata hali ya maisha. Inahalisi kuikumbuka maana ya msemo kuwa rangi na ngozi ni utambuzi si ubaguzi.

Waja hushirikiana katika hatua mbalimbali. Binadamu anazaliwa katika jamaa na pale pale hujiunganisha na majirani. Ujirani huu wa binadamu wenzake pamoja na mazingira yao huiunda tabia yake. Kadiri anavyokua ndivyo anavyoanza kujihisi mmoja wa watu wanaomzunguka, jamii ile, kabila lile au hata taifa lile. Ile kukabiliana na mazingira yake, binadamu huhitaji msaada na hata ulinzi wa watu wengine. Huu hasa ndio msingi wa methali ya kuwa mtu ni watu. Tangu akiwa mwana mkembe, mja huhitaji msaada wa watu wengine kupewa chakula, kusimama na kutembea, kufundishwa jinsi ya kujielezea, kupata matunzo wakati wa magonjwa, kuelekezwa jinsi ya kupambana na mazingira yake, kusoma na kuilewa jamii yake na hata kufuata Imani Fulani. Binadamu hutamani kufanya mambo ya kila nui ambayo hawezi kuyatimiza peke yake. Kwa mfano, mia hutegemea haki zake zilindwe na wengine, mathalani, serikali.

Popote binadamu alipo, ana haki ya kushirikiana na wenzake katika jamii yake. Haki ya kuishi maisha ya kijamii ni mojawapo katika haki za kimsingi katika maisha ya binadamu. Haki hii inaenda sambamba na uhuru wa binadamu wa kuchagua kikundi au tapo la wanajamii analotaka kujihusisha nalo. Haki hii ni ya lazima na inapaswa kulindwa isipokuwa pale tu inapokwenda kinyume na sharia za jamii Fulani. Kwa mfano , ikiwa kujihusisha na kikundi Fulani kunaelekea kuwa tishio kwa usalama wa jamii, basi haki hii huwa imetumiwa vibaya. Pili, binadamu anayeishi katika jamii anaweza kujipatia ali kutokana na kazi au juhudi zake. Hii ni haki yake. Hata hivyo, huruhusiwi kuiba ili aweze kuipata mali hiyo.

Ushirikiano kati ya binadamu au ushirikiano katika jamii ni msingi imara wa kuwepo kwa maendeleo katika jamii Fulani. Kila tutumiapo neo ‘maendeleo’, humaanisha kujielekeza lengo maalum tulilochagua na ambalo litayakuza maisha yetu. Maendeleo huhusisha kupiga hatua mbele. Mtu anayesonga mbele hana budi kuwa na kitu au lengo analoliendea huko mbele ikiwa hana lengo, basi takuwa anawayawaya kama kuku aliyedenguliwa kichwa na anapaswa kujitathmini. Maendeleo yanahusisha kutoka hatua Fulani duni hatua nyingine afueni.

Katika zama kongwe za kisayansi yamefikia ngazi za juu sana katika awamu hii kumesahilisha mambo mengi sana. Kuna mambo mengi chanya ambayo yametokana na maendeleo ya kisayansi kama vile: kurahisisha mawasiliano, kuharakisha na kuboresha uzalishaji mali, kufanya usafiri bora na mwepesi miongoni mwa wengine. Hata hivho, kuna maendeleo hasi kwa kuwepo kwa silaha za haki zinazoweza kuuangamiza ulimwengu mzima. Nchi ambazo zina satua kubwa huweza kutumia uwezo wao wa kiuchumi na kimaendeleo kuzidhalilisha jamii nyingine. Hata hivyo, ni vizuri maishani binadamu, mkubwa kwa mdogo, mwenye uwezo kwa asiyekuwa nao atambue kuwa mja anahitahi jamii.

for free revision past papers visit: www.freekcsepastpapers.com

**Maswali**

a) Je, ina maana gani kusema 'Aristotle anachukuliwa kama kitovu cha taaluma nyingine? (alama2)
b) Taja haki mbili kuu za binadamu (alama2)
c) Je, kwa mujibu wa kifungu hiki, maana ya maendeleo ni nini? (alama 3)
d) Kulingana na taarifa na taarifa hii, ni kwa nini huhitaji jamii. (alama 3)
e) Kifungu hiki kinatoa ushauri gani kubwa binadamu? (alama 2 )
f) Eleza maana ya maneno na kifungu kifuatacho kama kilivyotumiwa katika taarifa hii. (alama 3 )
   i) Satua
   ii) Anawayawaya

**2. UFUPISHO** **( ALAMA 15)**

**Soma kifungu kisha uyajibu maswali yanayofuata.**

Nidhamu ni kitu cha maana sana maishani mwa binadamu. Kila mwanafunzi anapaswa kuwa na nidhamu ya hali ya juu sana. Akiwa na nidhamu, atakuwa mtu mwadilifu anaweza kustahiwa na kusadikika katika mambo, shughuli na hali tofauti.

Kwanza, motto mwenye nidhamu huwa kama anga au nuru nyumbani, shuleni na pia katika jamii. Watu wote wanampenda na kumheshimu. Wazee kwa vijulanga wale wanamtegemea kama msimamizi wa mambo nyeti ya maisha yao. Kwa hivyo, ni dhahiri shahiri kwamba mwadilifu hunufaika sana, kinyume cha mkaidi ambaye wahenga walimwambia kwamba atakosa kufaidi hadi siku ya Idi.

Pili huwadia nyakati ambapo huwa kuna jambo la busara, mathalani jukumu ana dhima Fulani ambayo huhitaji tu mwakilishi mmoja darasani, shuleni au katika jamii. Bila shaka watu watamteua yule mwadilifu kuchukua nafasi kama hiyo. Ndio maana viranja wanaoteuliwa shuleni, huwa ni wanagenzi ambapo tayari wamekwishatiwa katika mizani na kupigwa msasa madhubuti.

Vile vile, mwadilifu daima atajiepusha na shutuma na manjanga yote yanayoweza kuchipuka.

Kuna msemo maarufu kwa busara yake iliyobusarisha mwadilifu kwamba, "aliye kando haangukiwi na mti. Pia waliambiwa kwamba, " Pilipili usiyoila yakuwashiani?"

Ni bayana kutokana na misemo hiyo miwili kwamba mwenye nidhamu hawezi kuhusishwa na majanga hatari yanayoweza kuwakumba watu.

Walakini ni vyema kujiuliza, je, nidhamu huanzia wapi, na kwa nini kuna baadhi ya ' watoro ambao ni watovu wa nidhamu? Utovu wa nidhamu huanzia awali sana maishani mwa mja. Mtoto anapozaliwa, anategemea miongozi na mielekeo ya watu wazima ambao mazingirane mwake. Ndipo wa kale wale waliokaramka walisema kwamba mtoto akibebwa, hutazama kisogo cha nina.

Hivi ni kusema kwamba, nidhamu au utovu wa nidhamu huanzia nyumbai hadi shuleni, kisha hupanuka hadi kutikia kiwango ambapo mja anatangamana na watu katika maisha yake ikiwa sehemu moja ya ukuaji wa nidhamu maishani mwa mja itasambaratika, basi hawezi akawa mkamilifu kinidhamu maishani mwake.

Kwa vile ni bayani kwamba mabaya yote wayatendao duniani hulipwa na Mola papa hapa duniani, watovu wa nidhamu wote huishia kuangamia, ama kujuta mno kwa amali zao potovu. Ni heri mja kujihidi mwenyewe, kwani huhalifu haulipi chochote.

for free revision past papers visit: www.freekcsepastpapers.com

**Maswali**

a) Kwa kurejelea aya tano za kwanza, eleza madhara yanayoweza kumpata mtu kwa kutokuwa na nidhamu. ( maneno kati ya 50 – 60 ) (al 6, 1 ya mtiririko)
b) Bila kubadilisha maana, fupisha aya nne za mwisho. (Tumia maneno 55-60) ( al 7, mtiririko 1)

**3. MATUMIZI YA LUGHA ( ALAMA 40 )**

1. Kwa kuzingatia hali y a mtetemeko wa nyuzi za sauti, taja aina mbili kuu za sauti. (alama 2 )
2. Fafanua muudno wa silabi ya neno <u>Ngwena.</u> (alama 2 )
3. Tunga sentensi moja kwa kutumia neno hili ' walakini' (alama. 2 )
4. Taja vipashio vikuu vya lugha kuanzia kikubwa hadi kidogo. (alama. 2)
5. Tunga sentensi moja kudhihirisha maana mbili tofauti ya maneno haya: (alama 2)
   Shaba
   Shamba
6. Taja kwa kutolea mifano matumizi mawili ya kinyota. (alama 2)
7. Ikarabati sentensi hii: (alama 2 )
   Mgeni ambaye aliyekuja atarudi jana
8. Taja miundo mine ya ngeli ya A-WA. (alama.2)
9. Tunga sentensi kwa kutumia kihisishi cha dharau. (alama. 2)
10. Ainisha mofimu katika neno: (alama. 2)
    yanyweka.
11. Taja sifa mbili za vitenzi vya asili ya kigeni. (Alama. 2)

12. Onyesha kiima na kiarifa katika sentensi. (alama. 2)
13. Eleza miundo yoyote tatu ya kirai Nomino. (alama. 3)
14. Taja sifa zozote mbili za kishazi tegemezi. (alama. 2)
15. Tunga sentensi yenye muundo huu: (alama. 2)
    Kitondo, kiarifa, kipozi, ala.
16. Tofautisha kati ya chagizo na kijalizo. (alama. 2)
17. Changanua sentensi hii kwa njia ya matawi. (alama. 4)
    Alifika jana alipotarajiwa.
18. Tunga sentensi kwa kutumia kiambishi cha masharti yanayowezekena. (alama. 2)
19. Ainisha matumizi ya ji katika sentensi hii: (alama. 1)
    Jitu lililojitokeza limeuawa

**4. ISIMU JAMII (AL. 10)**

1. Eleza maana ya istilahi zifuatazo (alama. 6)
   a) krioli
   b) Jamii ------------------------------------------------------------------------------------------------------------------
   c) Linguo Franka -----------------------------------------------------------------------------------------------------------
2. Fafanua mambo yanayochangia mtu kuwa na wingi lugha. (alama. 24

for free revision past papers visit: www.freekcsepastpapers.com

**SHULE YA UPILI YA SUNSHINE**

**102/3**
**KISWAHILI**
**FASIHI YA KISWAHILI**
**2017**
**MUDA: 2 ½**

**1. SEHEMU YA A: KIDAGAA KIMEMWOZEA** **( ALAMA 20)**

Walemavu katika jamii wametengwa badala ya kupendwa. Fafanua kauli hii kwa kurejelea Riwaya ya Kidagaa Kimemwozea. (alama 20)

**2. SEHEMU YA B: TAMTHILIA ( ALAMA 20)**

1. **"**Ya mwananti kiuvunda nti!"
a) Weka dondoo hili katika muktadha wake.
b) Tambua tamathali za usemi katika dondoo. (alama 2)
c) Fafanua ukweli wa "Ya mwananti kiuvunda nti!" kwa kurejelea tamthilia nzaima. (alama. 14)
2. Fafanua hali ya matibabu katika mi wa Cheneo (alama. 20)

**3. SEHEMU Y A C: HADITHI FUPI - Damu Nyeusi**

**i)** Vijana hukumbana na changamoto nyingi katika maisha Jadili kauli hii kwa kurejelea hadithi hizi. (alama. 20)
a) Damu nyeusi
b) Danda la usafi
c) Samaki wan chi za joto
d) Tazama na mauti
e) Shaka ya mambo

**ii)** "Leo ni siku ya siku , siku ya nyani kufa ambapo mtiti yote huteleza.
a) Eleza muktadha ya dondoo hili . (alama. 4)
b) Eleza sifa mbili za mrejelewa. (alama 2)
c) Fafanua changamoto zinazowakabili waafrika wasomi ughaibuni. (alama 14)

**4. SEHEMU YA C: USHAIRI**
**Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.**

1. Haki ya mtu thawabu Kuidai sitasita
Hata 'nipatishe tabu muhula mimi kukita
Kulitenda la wajibu liwe hai au mata
Nitafanya majaribi na inapobidi matata
Haki yangu 'taidai hata iwe ni kwa vita

2. Haki ha mtu u'ngwana siseme mimi nateta
Sitaukiri ubwna na jeuri unoleta
Na ikiwa ni kuwana sitajali sitajuta
Sikiri kuoneana na kupakana mafuta
Haki yangu 'taidai hata iwe ni kwa vita

3. Haki ifukie chini ipige na kubuta
'tumbukize baharini 'tazamia kufwata
Ukaifiche jangwani nitakwenda kuileta
Itundike milimani nitawana kuileta
Haki yangu 'taidai hata iwe ni kwa vita

4. Haki ijingee ngome izungushe na kata
Na fususi isimame iwe inapitapita
Tainuka nishikame haki yangu kukamata
Sifa kubwa mwanamume kuenda huku wasota
Haki yangu 'taidai hata iwe ni kwa vita

5. Uungwana siuuzi kwa njugu au kashata
Ahadi za upuuzi na rai kuitaita
Kwa kila alo maize hawi mithili ya bata
Tope yake makaazi na chakula cha kunata
Haki yangu 'taidai hata iwe ni kwa vita

for free revision past papers visit: www.freekcsepastpapers.com

**Maswali**

a) Bainisha dhamira ya mshahiri (alama. 2)

b) Eleza umuhimu wa mbinu zozote mbili ambazo mwandishi ametumia kutosheleza mahitaji ya kiarudhi. (alama. 4)

c) Andika ubeti wanne kwa lugha tutumbi. (alama. 5)

d) Fafanua aina tatu za urudiaji zilizotumiwa katika shairi hili. (alama. 3)

e) Ainisha shairi hili kwa kuzingatia vigezo vifuatavyo. (alama. 2)
   i) Idadi ya mishororo
   ii) Mpangilio wa vina

f) Fafanua toni ya shairi hili (alama. 1)

g) Taja nafsineni katika shairi hili (alama. 1)

h) Tambua na ueleze maana ya mshororo ufutao (alama. 2)

for free revision past papers visit: www.freekcsepastpapers.com

for free revision past papers visit: www.freekcsepastpapers.com

for free revision past papers visit: www.freekcsepastpapers.com

for free revision past papers visit: www.freekcsepastpapers.com

for free revision past papers visit: www.freekcsepastpapers.com

**MOKASA**
**102/3**
**KISWAHILI**
**2017**
**Karatasi ya 3**
**FASIHI**

**SEHEMU A: TAMTHILIA**
**Timothy Arege:** *Mstahiki Meya*

**1. Lazima**

"Acha nimfuate mara moja hii."

(a) Weka dondoo hili katika muktadha wake. (alama 4)
(b) Fafanua sifa zozote **nne** za msemaji. (alama 4)
(c) Ubarakala unalemaza maendeleo katika Cheneo. Jadili. (alama 12)

**SEHEMU B: RIWAYA**
**K. Walibora :** *Kidagaa Kimemwozea*
*Jibu swali la 2 au la 3*

**2.** Usaliti umeitawala jumuiya ya Kidagaa Kimemwozea. Thibitisha ukweli huu ukirejelea wahusika mbalimbali katika riwaya. (alama 20)

**3.** 'Sijawahi kumwona kibogoyo akiguguna mfupa. Siku moja isiyokuwa na jina siri zako zitafichuka na hila zako zikutokee puani.'
(a) Eleza muktadha. (alama 4)
(b) Taja na ueleze mbinu zozote mbili zinazodhihirika kwenye dondoo. (alama 4)
(c) Huku ukirejelea riwaya hii, fafanua kwa kutoa hoja sita namna anayelengwa na kauli hii, siri zake zilivyofichuka na hila zake kumtokea puani. (alama 12)

**SEHEMU C: USHAIRI**
*Jibu swali la 4 au la 5*

**4.** Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali yafuatayo.

**LONGA**

Longa longea afwaji, watabusarika
Longa uwape noleji, watanusurika
Longa nenea mabubu, sema na viduko

Longa usichachawizwe, tamka maneno
Longa usitatanizwe, mbwa aso meno
Longa usidakihizwe, kishindo cha funo

Longa yote si uasi, si tenge si noma
Longa pasi wasiwasi, ongea kalima
Longa ukuli kwa kasi, likate mtima

Longa zungumza basi, liume ja uma
Longa japo ni kombora, kwa waheshimiwa
Longa liume wakora, kwani wezi miwa

Longa bangu na papara, hawakuitiwa
Longa bunge si kiwara, si medani tawa
Longa ni simba marara, wanaturaruwa.

**Maswali**

(a) Tambua na ueleze nafsi neni katika shairi hili. (alama 1)
(b) Onyesha vile kibali cha utunzi wa mashairi kilivyotumika kukidhi mahitaji ya kiarudhi. (alama 4)
(c) Kwa kutoa maelezo mwafaka, tambua bahari nne zilizotumika na mtunzi kwenye shairi hili. (alama 4)
(d) Eleza aina tatu za urudiaji katika shairi. (alama 3)
(e) Tambua na kueleza toni ya shairi. (alama 2)
(f) Eleza maana ya msamiati ifuatayo kama ilivyotumika katika shairi. (alama 2)
(i) Afwaji
(ii) Tenge
(g) Eleza umbo la shairi hili. (alama 4)

for free revision past papers visit: www.freekcsepastpapers.com

**5.** Soma shairi lifuatalo kisha uyajibu maswali.

Jiji Juani
Jiji
Lililojaa fahari na vinyume

Maghorofa
Yatishayo kupasua ngozi ya mawingu
Viumbe na magari
Waliobanana barabarani.

Jiji la
Waliostaarabika
Ya kidunia
Mafukara.

Lililojaa mfano na mwambatano
Wa majalala ya taka na waokotezaji
Wa ombaomba na waliotakata
Wa polisi na dereva
Wa waliopujuka na wanaostahi.
Jiji la :
majengo ya aushi na mioyo ya mawe
jua linalooka viumbe
jua linalotekenya ngozi za watalii – wakimbiao ganzi ya
maji baridi
jua lichomalo wavuja jasho
Huku wakizumbua riziki.

La viwanda
Vijazavyo vibeti vyenye mimba vya wenye viwanda
Vinavyofuka moshi kwenye Madongoporomoka
Vinavyosumu maisha machanga na kuua wasiozaliwa.

Jiji
La wazururao na manamba
Wanaotia kitanzi staha
Wanaotoa kauli na maneno
Yanayouma na kukereketa.

La wazee na vijana
Ambao taadhima yao
Imemezwa na jiji juani.
Jiji litandalo mashariki na magharibi
Kaskazini na kusini
Mbuga zitandazo
Katikati ya tanuri hili.

Litengalo sehemu kwa baadhi
Majumba vilimani
Vyumba visivyodari
Na mabanda yaso dirisha
Kusugua mikono laini ya mwenye nyumba.

**Maswali**

(a) Fafanua maswala **matatu** makuu aliyoyashughulikia mshairi tungoni. (alama 6)

(b) Jadili jinsi mtunzi alivyotumia jazanda kufanikisha ujumbe wake. (alama 6)

(c) Mishata ni nini ? Bainisha matumizi mawili katika shairi. (alama 4)

(d) Shairi hili ni la kukatisha tamaa. Dhihirisha. (alama 4)

**SEHEMU D: FASIHI SIMULIZI**

**6.** **(a)** Fafanua sifa za matambiko katika jamii. (alama 4)

(b) Eleza tofauti kati ya maigizo ya kawaida na maonyesho ya sanaa. (alama 10)

(c) Taja shughuli zozote mbili zinazoonyesha matumizi ya ulumbi katika jamii ya kisasa. (alama 2)

for free revision past papers visit: www.freekcsepastpapers.com

(d) Tofautisha dhana zifuatazo :

(i) Miviga na maapizo (alama 2)

(ii) Ngoma na ngomezi (alama 2)

**SEHEMU E: HADITHI FUPI**

**K. Walibora** na **S. A. Mohamed:** *Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine*

**7.** Upungufu wa maadili ni suala linaloangaziwa katika Diwani ya *Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine*. Jadili kauli hii kwa kuzingatia haditi zozote tano. (alama 20)

for free revision past papers visit: www.freekcsepastpapers.com